

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SABA

Kikao cha Saba - Tarehe 10 Novemba, 2004

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mafundi wetu wamenihakikishia kwamba vyombo vyetu leo vinafanya kazi vizuri hatutapata tatizo kama tulilolipata jana.

Kikao kinaanza Kikao cha Saba cha Mkutano wa Kumi na Saba, Katibu.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) kwa mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2003 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Cooperative Audit and Supervision Corporation for the year ended 30th June, 2003*).

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa Mwaka 2002/2003 (*The Annual Report and Accounts of the Tanzania Harbours Authority for the year 2002/2003*).

NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa na Baraza la Taifa la Ufundji kwa Mwaka 2002/2003 (*The Annual Report and Audited Accounts of the National Council for Technical Education for the year 2002/2003*).

MASWALI NA MAJIBU

Na. 84

Usimamizi wa Uchaguzi Nchini

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (k.n.y. MHE. MOHAMED JUMA KHATIB) aliuliza:-

Kwa kuwa nchi nyingi duniani hasa Afrika zimekuwa zikikabiliwa na machafuko na vita vinavyosababishwa na kupingwa kwa demokrasia kama vile kuvurugwa kwa uchaguzi kutokana na Tume za Uchaguzi kuwatangaza washindi wasio halali; na kwa kuwa hali hiyo imewahi kujitokeza Zanzibar na kusababisha maafa makubwa:-

(a) Je, Serikali inaelewa kuwa iwapo chaguzi zinazokuja hapa nchini zitavurugwa na Tume ya Uchaguzi au vyombo vya dola hali inaweza kuwa mbaya zaidi na kuleta ugumu kuvisawazisha kuliko ilivyokuwa kwa mwaka 2000?

(b) Je, hali hiyo ikitokea Serikali haitawajibika kubeba lawama kwa kuwa yenye we ndiyo huandaa mazingira mazuri au mabaya katika chaguzi zetu kama ilivyokuwa kwa uchaguzi wa mwaka 2000 na uchaguzi mdogo wa mwaka 2003?

(c) Je, kwa mujibu wa demokrasia, Serikali inazichukuliaje kauli zinazotolewa humu Bungeni na baadhi ya Wabunge kama vile: “Haiwezekani na wala haitawezekana CCM kushindwa na ile: “Ili Muungano udumu CCM lazima ishinde Zanzibar?”

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB) alijibu :-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, Mbunge wa Chonga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haina taarifa kuwa Tume ya Uchaguzi hutangaza washindi wasio halali pamoja na Zanzibar. Jambo lililo wazi na sahihi ni kwamba Tume ya Uchaguzi inaendesha Uchaguzi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na Sheria za Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1995 na Na. 4 ya mwaka 1997. Utaratibu huu ndio ulioliweka Bunge hili Tukufu kutokana na kazi nzuri ya usimamiaji wa Uchaguzi vizuri wa mwaka 2000. Tulioshinda tulitangazwa na sasa ndiyo viongozi wa Taifa hili. (*Makofî*)

(b) Mheshimiwa Spika, katika uchaguzi mgombea aliyepata kura nyingi kuliko wagombea wengine ndiye anatangazwa kuwa mshindi. Tume imekuwa ikizingatia hivyo katika chaguzi zote ikiwemo chaguzi ndogo za mwaka 2003 ambaa muuliza swalii alitangazwa kuwa mshindi, nampa hongera. Serikali inaridhika kabisa kwamba chaguzi zilizopita ziliandaliwa katika mazingira mazuri, hivyo ni usoefu unaofaa kwa ajili ya

kuboresha uchaguzi unaofuata, ikiwa ni pamoja na uchaguzi wa mwaka 2005. Tume itahakikisha kwamba chaguzi zote zinaendeshwa kwa uhuru na haki jambo ambalo Serikali inaamini linaimarisha demokrasia nchini.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kuwa amani na utulivu vinadumishwa nchini, kwani hayo ni mionganoni mwa mambo muhimu sana katika kuweka mazingira bora ya uchaguzi na kujenga demokrasia ndani ya jamii.

Wakati wote Serikali inatimiza azma hiyo na kuwezesha wananchi na vyombo mbalimbali kutekeleza haki yao ya kidemokrasia na kutoa mawazo. Wabunge ni wawakilishi wa wananchi na kauli wanazozizungumza Bungeni ni za haki na ni sehemu ya uhuru wao. Bunge lenyewe kwa kutumia kanuni zake ndilo lenye haki ya Mamlaka ya kuamua kauli ipi inayokubalika na ipi isikubalike.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, nashukuru, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa katika chaguzi hizi mara nyingi kunakuwa na utashi wa baadhi ya watu ili kuingilia maamuzi ya Tume na mfano ni kama ilivyotokea Pemba katika uchaguzi wa mwaka 2000 ambapo wanasiasa fulani waliwashawishi askari kuchukua visanduku vya kura na kuvipeleka kwa Mkuu wa Wilaya kinyume na utaratibu, je, hali hii ikitokea Serikali itasemaje? Hilo moja.

(b) Lakini la pili, kwa kuwa masuala ya uchaguzi hayaangaliwi na sisi wenyewe tu tunaoshiriki kwenye uchaguzi, watu wengine pia huwa wanatazama masuala haya na huwa wanatoa maeleo yasiyordhisha kulingana na suala zima la uchaguzi kama uchaguzi wa mwaka 2000 ulivyokuwa walifikia kiasi cha kusema kuwa uchaguzi mzima wa Zanzibar ni *node and void* na unastahidi kufanya upya, je, Serikali inasemaje juu ya jambo hili?

Kwanza nafikiri Sheikh Khalifa Suleimani Khalifa, suala hili angewauliza katika Baraza la Wawakilishi kwa sababu wao ndiyo wenyewe Mamlaka ya kujua hili na ninaamini anayemwakilishi wake wa chama chake kwa hiyo angepata majibu sahihi kabisa. Sisi tunavyojuu ni kwamba uchaguzi ulikuwa halali na si kweli kwamba askari walichukua visanduku hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili sisi ni nchi huru kabisa kwa hiyo, maamuzi yetu ni maamuzi ya mwisho hatufuati maelekezo kutoka nje, jambo ambalo nafikiri ni muhimu kwa vyama vya siasa tatizo kubwa ni kwamba wao wanafikiri kwamba nchi yetu bado haiko huru wanataka kufanya vyama vyao vyama vya ukombozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili nafikiri ni muhimu wafuate utaratibu wa nchi za Magharibi kwamba wakishindwa wanakubali kushindwa. (*Makofi*)

Ugawaji wa Viwanja Dodoma

MHE. HAROUB SAID MASOUD aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni Serikali imezidisha jitihada zake za kuiendeleza Miji yetu ukiwemo wa Mji wa Dodoma kwa kupima na kugawa viwanja vingi vipyta kwa wananchi ili waweze kujijengea nyumba bora na za kisasa za kuishi pamoja na maofisi.

(a) Je, Serikali inaweza kulijulisha Bunge hili kwamba kuendelea kugawa viwanja bila kusimamia vile viwanja vilivyotolewa miaka kumi iliyopita itasaidia nini katika dhamira yake hiyo nzuri?

(b) Je, ni viwanja vingapi vilitolewa huko *Area A, C* na *D* ambavyo havijaendelezwa hadi sasa na vimeshapindukia muda uliowekwa wa kuviendeleza?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ina nia na dhamira nzuri ya kupima na kugawa viwanja vingi kwa wananchi hapa Dodoma ili kukidhi mahitaji ya nyumba bora za kuishi na matumizi mengine kama biashara, viwanda, huduma za jamii na kadhalika. Hata hivyo katika utekelezaji huwa kunajitokeza sababu za msingi zinazozua ufanisi wa utekelezaji wa dhamira iliyopo kwa kiwango cha asilimia mia kwa mia. Mapungufu ya utekelezaji yanapotokea, huwa sheria zinachukua mkondo wake ambapo asiyeeendeleza hatimiliki yake, hubatilishwa ikibidi na kiwanja kupewa mwanachi mwingine ambaye yuko tayari kutekeleza masharti ya uendelezaji wa viwanja mijini.

(b) Mheshimiwa Spika, tathmini ya viwanja visivyoendelezwa katika maeneo ya *Area A,C* na *D* ni kama ifuatavyo:-

(i) *Area A* Dodoma, viwanja vilivyopimwa na kugaiwa ni 792, Viwanja visivyojengwa kabisa ni 10, ni asilimia 1.3.

(ii) *Area C* ni viwanja vilivyopimwa na kugaiwa ni 965, viwanja visivyojengwa kabisa ni 33 ni asilimia 3.4.

(iii) *Area D* viwanja vilivyopimwa na kugaiwa 786, viwanja visivyojengwa kabisa ni 76 ni asilimia 9.7.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika sehemu ya (a) hapo juu, wale ambao hawajaendeleza baadhi yao waeshapewa *notice* na hatua nyingine za ubatilishaji zitachukuliwa ikiwa wenye viwanja hivyo hawatachukua hatua yoyote.

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa amekiri katika *Area A, C* na *D* viko viwanja ambavyo havijaendelezwa na viwanja hivyo vimeshapindukia miaka kumi, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba ifikapo Januari viwanja hivyo kama havijaendelezwa hati zao zibatilishwe na kupewa wale amba wanataka kujenga katika maeneo hayo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI): Mheshimiwa Spika, kabla ya mwaka 1999 kwa mujibu wa sheria ya Namba 4 ya ardhi ambayo imefanyiwa marekebisho hivi karibuni sisi kama *CDA* hatuna Mamlaka ya kufanya ubatilishaji wa viwanja hapa Dodoma kabla ya marekebisho hayo *CDA* yenye ilikuwa ina uwezo wa kubatilisha na *ku-effect* yaani na kufanya uamuzi wa haraka wa kumpa mtu mwingine kwa hivi sasa si rahisi kukiri hapa kwamba mwezi Januari tayari viwanja hivi vitakuwa vimebatilishwa kwa sababu mwenye uamuzi wa mwisho sasa ni Mahakama ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, sisi tumeshapeleka orodha hii Mahakama ya Ardhi kwa hiyo itategemea na Mheshimiwa Jaji wa Mahakama wa Ardhi hapa kama ana uwezo au Mahakama inayosikiliza kesi hizi za ardhi hapa Dodoma kama watakuwa wamemaliza na kutoa uamuzi kuhusu viwanja hivyo

Na. 86

Barabara ya Mnenia - Madege

MHE. KHALID S. SURU aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Mnenia - Masange - Itololo - Kisese - Kikore - Madege ni ya Halmashauri na kwamba ni mbovu sana na tena ina urefu wa zaidi ya kilometra 57; na kwa kuwa upembusi yakinifu uliofanywa na wataalamu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Mkuu wa Mkoo na wale wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya walibaini kwamba gharama kamili ya kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe, madaraja na makalvati yote muhimu ni zaidi ya shilingi milioni 900 kwa wakati huo wa miaka mine iliyopita:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hao kuondoa kero hiyo ikizingatiwa kwamba Halmashauri pekee haiwezi kumudu gharama hizo?

(b) Kwa kuwa barabara hiyo ni muhimu sana kiuchumi na kiusafiri na kwamba ni madai ya wananchi ya wakati wote na ni siku nyingi, je, Serikali inaweza kutoa maelezo ya jinsi ilivyoshiriki kulitattua tatizo hilo?

(c) Je, kwa umuhimu wa barabara hiyo na urefu wake, pia uharibifu mkubwa uliopo, isingefaa barabara hiyo ichukuliwe na Serikali Kuu au itengewe fedha za kutosha kuitengeneza na kuikabidhi kwa Halmashauri kuiendesha?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika barabara ya Mnenia - Madege yenye urefu wa kilometa 57 ni ya Halmashauri ya Wilaya na inaunganisha Kata za Kikore, Kisese, Masange, Bumbuta, Mnenia na Kolo. Barabara hii ni muhimu sana kiuchumi, kwa kuwa inapitia kwenye maeneo yenye rutuba na skimu za umwagiliaji za Kisese, Kikore, Hurui, Madege, Mkurumuzi na Mnenia.

Serikali inaelewa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa haiwezi kumudu gharama za matengenezo ya barabara hiyo, hivyo ili kupunguza kero iwapatayo wananchi kutokana na ubovu wa barabara hiyo, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imekuwa ikifanya matengenezo ya sehemu korofi ili kuwezesha barabara hiyo kupitika wakati wote.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii Serikali imekua ikiifanya matengenezo kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kama ifuatavyo:-

Mwaka 2001/2002 barabara hii ilifanyiwa matengenezo ya kawaida ya urefu wa kilometa 18 kazi kubwa ikiwa ni ujenzi wa madaraja madogo 16 kwa gharama ya shilingi 16,000,000/. Mwaka 2003/2004 barabara hii ilipangwa kufanyiwa matengenezo ya kuimarisha sehemu korofi na kujenga madaraja madogo 12, *Drifts* 2 na kuchonga barabara kilometa 14. Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa iliingia mkataba wa matengenezo na Mkandarasi *M/S Kondoa Investment* kwa gharama ya shilingi 36,900,000/. Matengenezo hayo yalishaanza na mkandarasi anategemea kukamilisha kazi hiyo mwezi huu Novemba, 2004.

Aidha, ili kuendeleza matengenezo ya barabara hii, Halmashauri ya Wilaya imeiorodhesha barabara hii kwenye mapendekezo ya Mpango Maalum wa Matengenezo ya Barabara za Halmashauri kwa miaka mitatu (*Three years Road Rehabilitation Plan for the Councils*) ambao utaendeshwa na Mfuko wa Barabara fedha zitakapopatikana . Inakadirisha jumla ya shilingi milioni 1, 140 zitahitajika ili kukamilisha matengenezo katika kilometa 57 za barabara hiyo.

(c) Ili barabara hii ichukuliwe na Serikali kuna taratibu za kufuata na sifa za kuzingatiwa kama vile barabara kuhudumia zaidi ya tarafa moja , wingi wa magari yanayotumia barabara hiyo na kuwepo kwa shughuli muhimu za kiuchumi. Wilaya ilishawasilisha maombi Serikalini ya kutaka barabara hii ihudumiwe na Mkoa, kwa barua Kumb. Na. MB/MW/2/121 ya tarehe 19 Mei, 2003 na Kumb. Na. BS/MW/2/2006

ya tarehe 7 Desemba, 2003 zilizowasilishwa kwa Waziri wa Ujenzi. Maombi haya yanashughulikiwa.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza, lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri pamoja na kwamba tatizo hilo bado halijaisha.

(a) Mheshimiwa Spika, kikwazo kikubwa ni madaraja na madaraja hayo ni Tandaga, Kisese, Mitati ambayo Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa haiwezi, je, Serikali Kuu haiwezi ikasaidia ikatatua tatizo hilo ambalo ni kero kabisa kwa wananchi badala ya kusubiri hizo fedha za mfuko wa barabara?

(b) Urefu wa barabara hiyo na umuhimu wake na hivi ni kweli kabisa Serikali yetu adilifu kabisa ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa, inashindwa hata kuchangia kutoka hazina kuondoa tatizo hilo ambalo ni la muda mrefu kabisa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo ya awali, matatizo ya barabara hii yanafahamika na Serikali na ni kweli kabisa kwamba tatizo kubwa lililopo katika barabara hiyo licha ya yale mengine niliyoyaeleza ni madaraja mabovu ambayo yote yanahitaji kutengenezwa. Mheshimiwa Khalid Suru, mimi nakuomba tu tuendelee kusukuma jambo hili polepole kwa sababu kwa kweli kikwazo ni fedha, tungekuwa nazo tusingesita kutekeleza matakwa haya.

Lakini pili, Serikali hii ni kweli ni makini na ni adilifu sana, Mheshimiwa Khalid Suru, naomba kwanza nikupongeze katika kujitahidi kwako kujaribu kutafuta ufunguzi wa barabara hii, wewe mwenyewe ni shahidi, umeandika barua mpaka kwa Rais ukiomba aingilie kati jambo hili lakini bado tulipata kigugumizi kwa sababu sungura tunayegawana ni kidogo mno.

Lakini tuendelee na hizi jitihada za mfuko wa barabara kutengeneza eneo korofi na pengine madaraja kidogo kidogo tutaelekeza nguvu zetu kwa kadri nafasi itakavyopatikana.

Na. 87

Mabaraza ya Kata

MHE. STEPHEN M. KAHUMBI aliuliza:-

Kwa kuwa kuanzishwa kwa Mabaraza ya Kata kutasaidia sana kupunguza misongamano ya mashauri katika Mahakama za Mwanzo na pia zitasaidia kusukuma mipango ya maendeleo ya Vijijini na Kata; na kwa kuwa kinachopunguza nguvu ya Mabaraza haya ni udogo wa adhabu zinazotolewa na Sheria iliyoanzisha Mabaraza haya.

(a) Je, ni lini Serikali italeta Bungeni marekebisho ya adhabu hizi?

(b) Je, kuwalipa posho Wajumbe wa Mabaraza haya hakutengui umurua wa lengo la adhabu zenyewe na kuzijengea hoja kuwa wajumbe wanaadhibu ili watape posho zao tu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a), na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Kata yameanzishwa kwa Sheria ya Mabaraza ya Kata yaani *The Wards Tribunals Act No.7/1985* kwa madhumuni ya kupunguza msongamano wa kesi katika Mahakama za mwanzo na hivyo kurahisisha utoaji wa haki kwa wananchi. Kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanywa na Sheria Namba 12/1990 kwenye Sheria ya Mabaraza ya Kata, adhabu kwa makosa yaliyo ainishwa katika sheria hii ni faini isiyozidi shilingi 10,000/=au kifungo kisichozidi miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, adhabu hiyo, kwa mazingira ya vijiji siyo ndogo kwa sababu madhumuni ya Mabaraza haya ni kufanya usuluhishi na kuleta amani na utulivu na siyo kutilia mkazo kuwafunga gerezani wananchi.

Aidha kupitia sheria Namba 2 ya mwaka 2002 ya Mabaraza ya migogoro ya ardhi yaani *The Land Distributes Contract No 2 of 2002*, Mabaraza ya Kata yameongezewa jukumu la kusimamia vile vile migogoro ya ardhi.

Hata hivyo Ofisi yangu imeanza mchakato wa kupitia Sheria mbalimbali zinazohusiana na suala hili kwa lengo la kuona na kubaini kama kuna mapungufu yoyote na kama yatabainika tutawasilisha marekebisho kupitia Bunge lako hili Tukufu.

(b) Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba hatua ya kuwalipa posho Wajumbe wa Mabaraza ya Kata inatenga lengo la adhabu na kujenga hisia kuwa Mabaraza haya yanatoa adhabu ya faini ili wapate posho. Utaratibu wa kuwalipa posho Wajumbe wa Mabaraza ya Kata umeelezwa vizuri katika kifungu cha 27 cha Sheria ya Mabaraza ya kata ambapo mapendekezo ya kiasi cha posho yanaanza katika kamati ya Maendeleo ya Kata na kuidhinishwa na Halmashauri husika na kwamba Sheria haiagizi kwamba posho za Wajumbe zitokana na faini zinazotozwa na Mabaraza.

MHE. ANATORY K. CHOYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali lifuatalo:-

Kwa kuwa Wajumbe wa Mabaraza wanapoteuliwa huanza kazi mara moja kabla ya kupata elimu yoyote inayohusu kazi yao na hivyo kusababisha mapungufu mengi katika utendaji kazi wao, je, Serikali inachukua hatua gani katika kurekebisha kasoro hii kubwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, nina hakika Mheshimiwa Mbunge atakumbuka wakati Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, alipokuwa anawasilisha Bajeti yake hapa Bungeni mwaka huu hata mwaka jana alitoa kwa kirefu sana maelezo kuhusiana na juhudi za Serikali za kutoa elimu kwa maeneo yote katika ngazi za Kata, Vijiji na Halmashauri ili kuwawezesha viongozi hawa kuwa na upeo wa namna ya kuteua wajumbe.

Mheshimiwa Spika, juhudi zinaendelea katika kila Kata kwa hivi sasa ili hao wajumbe nao waweze kuwa wanapata semina na maelekezo mengine ambayo yatawasaidia kuweza kufanya kazi zao vizuri zaidi. Kwa hiyo, nina hakika tutaendelea kuongeza kasi ili madhumuni yake yaweze kufikiwa bila matatizo makubwa.

Na. 88

Gari - Kituo cha Polisi Sanya Juu

MHE. AGGREY D. J. MWANRI aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu nimekuwa nikiwasiliana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi nikiomba tupatiwe gari katika Kituo cha Polisi cha Sanya Juu ili kiweze kutafutiwa gari jipya ambalo linaweza kuhimili hali ya barabara za Siha ambazo nyingi ni mbovu sana; na kwa kuwa wimbi la ujambazi linazidi kuongezeka kwa kasi kubwa.

Je, ni kwa nini Serikali isikubali kutupatia gari lingine kwa sababu lile lililopo ni bovu sana na mara zote liko juu ya mawe?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba nina mawasiliano na Mheshimiwa Mbunge kuhusu ombi la kukipatia gari Kituo cha Polisi Sanya Juu. Kutohana na mawasiliano hayo, nimewahi kukitembelea kituo hicho na kujionea mwenyewe hali halisi. Ni kweli pia kwamba kituo hicho kina usafiri usio wa kuaminika kutohana na gari lake kuwa kuukuu. Hali hiyo niliyoiona Siha inavikabili vituo vingi sana nchini mwetu vikiwemo hata vya Wilaya ambapo vingi vyake havina kabisa hata hilo gari bovu.

Mheshimiwa Spika, kutohana na ukubwa wa tatizo ambalo haliwezi kutatuliwa lote kwa pamoa, Jeshi la Polisi lina mpango wa kulitatu hatua kwa hatua kama nilivyoeleza katika Hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2004/2005 ambapo tumeanzia kwa kutoa kipaumbele kwa vituo vya polisi vya Wilaya. Baada ya kupata ufumbuzi kwa vituo vya Wilaya, tutaanza kuvipatia vituo vya ngazi ya chini kikiwemo kituo cha Sanya Juu. Kwa wakati huu tutaendelea kushughulikia matengenezo ya magari makuukuu kama hilo la Sanya Juu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa kufuatilia kwa karibu suala la vitendea kazi kwa askari Jimboni kwake. Tunamwomba avute subira wakati Serikali inajenga uwezo wa kuboresha vitendea kazi katika Jeshi la Polisi.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa majibu mazuri aliyoyatua hapa japo anapo-conclude yanankatisha tamaa.

Kwa kuwa anathibitisha mwenyewe Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri kwamba alifika katika Jimbo la Siha na alikitembelea kituo hiki na aliona kabisa hali ya gari ilivyo; na kwa kuwa mwanzo wa mwaka huu Diwani wangu Mheshimiwa Daniel Sandewa, alivamiwa na majambazi katika eneo hili hili; na kwa kuwa mwananchi aliyeo katika kijiji cha Koboko alivamiwa na majambazi kwa kutumia silaha hili ni eneo la kijiji.

SPIKA: Hebu punguza kwa kuwa, uliza swali. (*Kicheko*)

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Spika, je, atakubaliana na mimi kwamba kituo cha Sanya Juu kinahitaji kipaumbele katika sula hili?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpe pole kwa haya matukio yaliyotokea kwa Diwani wetu kule, lakini vilevile naomba asikate tamaa maana yake anasema kwamba majibu yanakatisha tamaa, naomba asikate tamaa kwa sababu Bunge hili hili na ye ye akiwa mmojawapo mwaka huu wa fedha ametupishia kununua magari mapya ya polisi 174, haijapata kutokea. (*Makofî*)

Kwa jeshi polisi kwa mwaka mmoja kuwezeshewa kununua magari 174 na magari haya ndiyo tutakayogawa kwenye Wilaya mbalimbali pamoja na Wilaya ya Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa hiyo, *OCD* akishapata gari lingine la nyongeza nina hakika kabisa na ye ye atafanya utaratibu wa namna ya kuhudumia vituo vilivyo ndani ya Wilaya yake na nimesema tukishamaliza kutatua katika ngazi ya Wilaya tutakwenda katika vituo vya ngazi za chini hapo ndipo tutatoa kipaumbele kwa kituo cha Sanya Juu.

Na. 89

Hali ya Usalama Jimbo la Nanyumbu

MHE. ARIDI M. ULEDI aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Nanyumbu limekuwa likikabiliwa na matukio ya mauaji yakiwemo ya matumizi ya silaha; na kwa kuwa eneo la Jimbo hilo ni kubwa sana kwa Kituo cha Polisi cha Mangaka kuweza kulidhibiti kiusalama; na kwa kuwa Kituo hicho pekee kimekosa nyenzo muhimu kama gari la kuzungukia eneo lote la Jimbo.

(a) Je, ni lini Serikali itakipatia Kituo cha Polisi cha Mangaka gari ili kusaidia kuimarisha usalama wa Jimbo?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa kuna haja ya kufungua vituo vidogo vya polisi kwenye Kata za Nanyumbu na Napacho ili kuimarisha usalama?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka kudhibiti hali ya usalama wa Jimbo la Nanyumbu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aridi Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hali ya uhalifu katika Jimbo la Nanyumbu si mbaya; na kwa kuwa Serikali haina uwezo kwa sasa wa kuvipatia magari vituo vidogo. Hivyo Serikali haina mpango kwa sasa hivi wa kukipatia gari kituo cha polisi cha Mangaka.

Mheshimiwa Spika, kituo hicho kitaendelea kuhudumiwa na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Masasi ambaye ana magari mawili. Magari hayo yanatumika katika vituo mbalimbali Wilayani humo ikiwa ni pamoja na Mangaka yanapotokea matukio yanayohitaji usafiri wa gari.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kujengwa kwa vituo vya polisi katika Kata za Nanyumbu na Napacho kutaimarisha ulinzi wa maeneo hayo, hata hivyo miradi hiyo sharti ianzishwe na wananchi wenyewe na Serikali itawaunga mkono kwa kadri hali ya Bajeti itakavyoruhusu.

(c) Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba hali ya usalama katika Jimbo la Nanyumbu ni ya kuridhisha sana, Serikali itaendelea kuimarisha doria za askari polisi na kuwahamasisha wananchi vijijini katika Jimbo hilo ili washiriki katika ulinzi wa sungusungu kwa lengo la kudumisha hali ya amani na utulivu uliopo sasa katika eneo hili.

MHE. ARIDI M. ULEDI : Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jimbo la Nanyumbu linapakana na nchi jirani ya Msumbiji; na kwa kuwa wahalifu wengi wakishafanya uhalifu huo hutorokea nchini Msumbiji ili kukwepa kukamatwa na vyombo vya dola hasa pale wanapochelewa kuja katika sehemu ya tukio.

(a) Je, Serikali haioni kwa polisi kufika au kuchelewa kufika sehemu ya tukio ni kuwapa mwanya wahalifu hao kutoroka?

(b) Je, kwa hali hiyo wananchi wakiamua kujichukulia sheria mkononi nani atabeba lawama?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Jimbo la Nanyumbu linapakana na nchi ya jirani ya Msumbiji na hivi karibuni mwezi uliopita nilitembelea Jimbo lake na yeze ni shahidi na tuliona hali ya kule mpakani kwa jumla ni shwari. Lakini bado tumekubaliana na viongozi wa Mkoa na Wilaya kwamba tusogeze ulinzi wa polisi mpaka katika kijiji kinaitwa Mtambaswala.

Kwa hiyo, tunao mpango tukishirikiana na Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo hilo kujenga Kituo katika kijiji cha Mtambaswala ambacho kipo Mpakani kabisa na Msumbiji. Kwa hiyo, huo utaratibu tunao na tutaendelea nao. Vile vile katika Kituo cha Polisi cha Mangaka tumeongeza askari kufikia mpaka nane na tumewapa na *Radio Call* ya kisasa kabisa, hizi ni hatua mbalimbali za kuimarisha ulinzi katika eneo hilo.

Kuhusu sehemu ya pili ya swali lake kwamba je, wananchi wakijichukulia sheria mkononi nani alaumiwe?

Naamini wananchi wa Masasi, Nanyumbu ni wananchi watulivu na wasikivu. Sifkirii hata kidogo kwamba itafika wakati waanze kujichukulia hatua mkononi. Serikali wakati wote imekuwa ikiwataka wananchi sio wa Masasi tu, pote nchini kwamba tabia ya kujichukulia sheria mikononi ni ya hatari na inajenga utamaduni wa hatari. Kwa hiyo, tunawaomba waache likitokea tukio waviarifu vyombo vyaya dola na vitafanya kazi yake.

SPIKA: Baadhi ya maswali yaliyokosa nafasi jana yamewekwa kwenye orodha ya leo, kwa hiyo, naomba maswali ya nyongeza yasiwe mengi ili kusudi tuyatendee haki yale ambayo majibu yake yameandaliwa vizuri na Serikali.

Na. 90

Barabara ya Nyigo - Mgololo

MHE. BENITO W. MALANGALILA aliuliza:-

Kwa kuwa Kiwanda cha *SPM* - Mgololo kimebinafsishwa; na kwa kuwa ili kifanye kazi ipasavyo ni muhimu kwa barabara ya Nyigo - Mgololo, itengenezwe ili iweze kupidika kwa nyakati zote; na kwa kuwa barabara hiyo yenye urefu wa kilometra 60 ni mbovu na haipitiki kabisa nyakati za mvua:-

(a) Kwa kuwa Bodi ya Barabara Mkoa ilishaomba barabara hiyo ipandishwe daraja toka barabara ya Wilaya kuwa ya Mkoa tangu mwaka 1996; je, kwa nini mpaka sasa Serikali haijakubali ombi hilo?

(b) Kwa kuwa Serikali kwa upande wa Wizara ya Ujenzi katika hotuba yake imekuwa ikisema kuwa itazingatia sana kutengeneza barabara kwenda kwenye maeneo yenye viwanda vikubwa, *SPM* - Mgololo ikiwa mojawapo; je, kwa nini sasa Serikali hajakubali maombi hayo?

(c) Kwa kuwa nimepewa maombi rasmi na mwekezaji pamoja na wananchi wa Mgololo kwa Wizara ya Ujenzi iichukue na kuitengeneza barabara hiyo kwa manufaa ya kiuchumi ya nchi; je, Serikali inatoa kauli gani?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikipokea maombi mengi yenye lengo la kuzipandisha hadhi ama daraja barabara kadhaa za Wilaya hapa nchini ili ziwe za Mkoa na hivyo kuhudumiwa na Serikali Kuu moja kwa moja. Barabara hii ya Nyigo hadi Mgololo yenye urefu wa kilomieta 60 ni mfano mmojawapo wa maombi ya aina hiyo. Pamoja na kuwa ni kiungo muhimu kati ya Kiwanda cha Karatasi cha *Southern Paper Mills (SPM)* na Barabara Kuu ya *TANZAM* sehemu ya Nyigo, umiliki wa barabara hii bado upo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inakamilisha mapitio ya sheria ya barabara (*Highway Ordinance*) ambayo ndani yake barabara zote nchini zitawekwa kwenye makundi ama madaraja yanayostahili kulingana na vigezo vilivyokubalika. Katika zoezi hilo, baadhi ya barabara za Wilaya zinazokidhi vigezo vya kupandishwa daraja zitapandishwa. Mapitio ya sheria hiyo yatakapokamilika, barabara zote nchini zitawekwa kwenye madaraja yanayostahili.

Mheshimiwa Spika, hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Iringa wavute subira juu ya ombi hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mojawapo ya vigezo vya kuipandisha daraja barabara ili iwe na hadhi ya Mkoa ni kule kuwapo kwa mtandao wake katika maeneo yenye viwanda vikubwa vya uzalishaji. Ni matarajio yangu yote hayo yatazingatiwa wakati wa kukamilisha mapitio ya sheria ya barabara, kama nilivyoelezea kwenye sehemu (a) hapo juu.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu maombi ya mwekezaji kwenye Kiwanda cha Karatasi cha Mufindi pamoja na wananchi wa Mgololo ni vema wakasubiri matokeo ya mapitio ya *Highway Ordinance*. Hata hivyo, wakati sheria inaendelea kufanyiwa mapitio, mwekezaji na wananchi waendelee kutumia Barabara Kuu ya Mafinga - Mgololo inayounganisha Kiwanda cha Karatasi cha Mufindi na Barabara Kuu ya

TANZAM pale Mafinga. Barabara hii inahudumiwa na Wizara yangu kuitia Wakala wa Barabara na inapitika majira yote ya mwaka.

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninalo swali dogo la nyongeza kwamba barabara hii Nyigo-Mgololo ilipasuliwa na Wizara ya Ujenzi na kwa zaidi ya miaka kumi imekuwa ikihudumiwa na Wizara ya Ujenzi mpaka Wizara hii ilipoitelekeza barabara hii. Sasa swali langu ni lini Serikali Kuu yaani Wizara Ujenzi itaichukua barabara yake ambayo iliipasua na iliendesha kwa miaka mingi?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, barabara hii ilipasuliwa na Wizara ya Ujenzi miaka kumi iliyopita kwa sababu Wizara iliombwa kufanya hivyo kwa sababu Wilaya haikuwa na mitambo ya kuweza kupasua barabara hiyo na Wizara ilikubali kutengeneza hiyo barabara na waliomba tena Wizara iihudumie. Lakini Wizara ilihudumia kwa kiwango mpaka pale ilipoikamilisha, ikaikabidhi kwa Wilaya ya Mufindi na wao ilikuwa ni jukumu lao sasa kuchukua wajibu wa kuikarabati barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba tungoje basi maombi ya Mkoa pale tutakapoleta sheria ya barabara hapa Bungeni pengine maombi yake yatakuwa yamefikiriwa kupandishwa hadhi.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumeelezwa kwamba mapitio ya Sheria hii yalikuwa yanafanyika tangu mwaka 2001, ni lini sasa Wizara italeta Muswada huo ili ujadiliwe hapa Bungeni ili suala hili lisiendelee kuwapo hapa kila siku? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, sheria hii ni kweli tumezungumza kwa muda mrefu sana na tumeitengeneza kwa muda mrefu sana na bado hata hivyo maombi yanakuja kila wakati kutoka Mikoani kwa sababu ni sheria ambayo iko nyeti kabisa inagusa mpaka wanakijiji. Kwa hiyo, tunataka wadau mpaka Mikoani itakapokamilika tuipeleke huko kwanza kabla ya Waheshimiwa Wabunge kuanza kujadili mkaja mkalaumiwa kwamba mmeamua peke yenu. Sasa tumeitengeneza wadau wengine wanaishughulikia na baada ya hapo hatua inayofuata ni kupeleka sheria hii kwenye Bodi za Mikoa ili waione huko halafu tuilete Bungeni. Kwa hiyo, subira yavuta kheri.

Na. 91

Ujenzi wa Barabara za Lami

MHE. SOPHIA M. SIMBA (k.n.y. MHE. SALOME J. MBATIA) aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi imejitahidi sana katika kuondoa kero mbalimbali za wananchi wake mojawapo ikiwa ni ujenzi wa barabara kadhaa za lami nchini:-

(a) Je, ni hali gani inasababisha baadhi ya sehemu za lami kwenye barabara hizo kuchakaa haraka na kusababisha migongo ya barabara kwa mfano sehemu ya Chalinze karibu na makutano ya barabara ya Tanga, sehemu za baada ya *Salender Bridge* ukielekea karibu na Ubalozi wa Ufaransa, sehemu za milima ya Kitonga (zamani) na kadhalika?

(b) Je, ni nini tofauti za kiufundi na kigharama kati ya barabara zilizojengwa zamani kwa mfano iliyokuwa barabara ya Arusha-Moshi, Moshi - Marangu, ambazo kingo zake zilikuwa zinaimarishwa kwa mawe, na ujenzi wa sasa ni kama hamna kingo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya *TANZAM* ambayo inajumuisha Milima ya Kitonga ilijengwa mwaka 1972. Sehemu ya Milima ya Kitonga ina miinuko mikali ambayo inafanya magari mengi yatumiayo barabara hiyo kwenda pole pole wakati wa kupanda milima hiyo hasa yanapokuwa na mizigo kutoka bandarini Dar es Salaam kuelekea maeneo y Kusini.

Kitendo cha magari yenyenye mizigo kupanda pole pole kinaongeza mkandamizo mkubwa kwenye barabara hiyo hivyo kuifanya iharibike haraka. Hali hii ndiyo iliyofanya maeneo kadhaa ya barabara kwenye Milima ya Kitonga na sehemu ya barabara ya Chalinze karibu na makutano ya barabara ya Tanga kuharibika haraka na baadhi ya sehemu zingine.

Aidha matumizi mabaya ya barabara kwa mfano magari yanayobeba mafuta yanapopanda sehemu za milima, mafuta humwagika hivyo kufanya lami kuyeyuka na kupunguza uimara wake kwenye baadhi ya maeneo kwenye barabara husika. Hii inachangia kuchakaa kwa barabara kabla ya muda wake uliokadiriwa kitaalamu.

(b) Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa kingo za barabara za lami kwa kutumia zege au mawe hufanywa sehemu ambayo utafiti umeonyesha kuwa pana uwezekano mkubwa wa kutokea mmomonyoko wa udongo (*soil erosion*). Kwa kuwa ujenzi huu ni aghali sana, mapendekezo ya kuimarisha kingo za barabara hutolewa na kufanyiwa kazi katika maeneo yenyenye matatizo tu.

MHE. SOPHIA M. SIMBA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Ninalo swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inajitahidi sana kufanya kazi nzuri ya kutengeneza barabara za lami; na kwa kuwa juhudhi hizo wananchi wote tunaziona na nia kubwa ni kupunguza ajali za barabarani. Sasa swali hivi yale mapipa yaliyopangwa katika Daraja la Ruvu kwa zaidi ya mwaka mmoja ule ni utsalamu gani? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wanakumbuka kwenye Bajeti yetu tumetenga fedha za kutengeneza Daraja la Ruvu jipya kwa sababu Daraja lile la Ruvu sasa hivi haliruhusu magari mawili ya mizigo kupishana.

Baada ya kuleta wataalam na kuchunguza, wamekataza kabisa gari mbili zisipite pamoja kwa sababu Daraja hilo haliwezi kubeba uzito huo tena, linaweza likavunjika ndio maana tumeponga mapipa na kuweka matuta ili kuzuia magari mawili kupita pale. Kwa hiyo, wanapishana gari moja baada ya lingine mpaka hapo tutakapojenga Daraja jipya.

Na. 92

Ukosefu wa Umeme - Lindi

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE (k.n.y. MHE. BERNARD K. MEMBE) aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Lindi wameachwa kwenye njia panda juu ya ukosefu wa umeme japokuwa Mkoa huo unazalisha umeme wa Songosongo; na kwa kuwa Serikali ilitamka katika Mkutano wake wa Bunge wa Kumi na Tano, kuwa inaangalia uwezekano wa kuupatia Mji wa Mtwara, Lindi na Masasi umeme kutoka *Mnazi-Bay*.

(a) Je, Serikali inaweza sasa kutamka kwa uhakika chanzo cha umeme wa Mkao huo kitakuwa kipi kati ya hivyo viwili?

(b) Je, ni lini wananchi wa Mkao huo wataanza kupatiwa umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe, Mbunge wa Mtama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kati ya vyanzo hivyo viwili vya uzalishaji umeme Mji wa Lindi umepangiwa kupatiwa umeme utakaotokana na mradi wa gesi ya *Mnazi Bay* ifikapo mwezi Desemba, 2005.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi wa *Mnazi Bay* unaendelezwa na mwekezaji binafsi kutoka Canada anayeitwa *Artumas Group Inc.* Makubaliano ya kuendeleza mradi huo yalisainiwa kati ya mwekezaji na Serikali mwezi Julai, 2004. Mradi utatekelezwa kati awamu mbili zifuatazo:-

(i) Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza inahusu kutathmini iwapo kiasi cha gesi kilichopo hapo *Mnazi Bay* kinatosha kwa ajili ya mahitaji ya umeme unaohitajika kwa megawati 15. Maandalizi ya utekelezaji wa awamu hii yamekwishaanza na kazi ya kutathmini inategemewa hivi karibuni na yanatarajiwa kuchukua kipindi cha miezi mitatu.

(ii) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa awamu ya pili utaanza baada ya kuthibitika kuwa kiasi cha gesi kilichopo *Mnazi Bay* kinatosha. Awamu hii ambayo utekelezaji wake utachukua pia muda wa miezi sita kukamilika inahusu ujenzi wa bomba la gesi lenye urefu wa kilometra 27 kutoka *Mnazi Bay* hadi Mtwara, kituo cha kuzalishia umeme chenye uwezo wa Megawati 15 hapo Mtwara, laini ya umeme wa msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilometra 78 kutoka Mtwara hadi Mingoyo na kukarabati laini iliyopo ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometra 25 kutoka Mingoyo hadi Lindi.

MHE. ABDILAH O. NAMKULALA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja ndogo la nyongeza. Kwa kuwa tulipokwenda *Mnazi Bay* na Mheshimiwa Waziri Mkuu tulikuta tatizo kwamba watu wa *Marine Park* wamekwamisha kwa miezi sita shughuli za uchimbaji wa gesi, je, Serikali ipo tayari kuzungumza na watu wa *Marine Park ili wasikwamishe uchimbaji* wa gesi hiyo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, Serikali ni moja na inafanya kazi kwa pamoja. Hao wawekezaji hawakukwamishwa, walitakiwa wafuate taratibu fulani na sisi katika Wizara ya Nishati na Madini tulishazungumza na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, hakuna tatizo la kwamba wataendelea au wamekuwa wakikwamishwa kwa maana hiyo ambayo amezungumza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua nafasi hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wa maeneo husika na Bunge lako Tukufu kwa ujumla kwamba kazi hii itaendelea kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa na tusubiri matokeo ya tathmini hii ambayo imepangwa kufanyika.

Na. 93

Umeme Nanyamba

MHE. ABDILAH O. NAMKULALA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeshaniahidi kuwa wanatafuta fedha ya kupeleka umeme mji mdogo wa Nanyamba na kuvipatia vijiji vya kwenye Jimbo langu swali hili nalifuta ili kuipa nafasi Serikali kunifanya shughuli hizo ilizoniahidi. (*Makofsi/Kicheko*)

Na. 94

Zao la Nazi

MHE. RAMADHANI H. KHALIFAN aliuliza: -

Kwa kuwa Waziri wa Kilimo na Chakula alipojibu swalii namba 357 katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge alilifahamisha Bunge kwamba uzalishaji wa nazi nchini umeongezeka kutoka nazi milioni 555 mwaka 1979 hadi zaidi ya nazi milioni 850 hivi sasa; na kwa kuwa, bei ya nazi moja katika masoko ya hapa nchini ni kati ya shilingi 100/= na shilingi 200/= au zaidi: -

(a) Je, zao hilo limetoa mchango halisi (*net*) kiasi gani kwa Pato la Taifa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita?

(b) Je, katika pato hilo, ni kiasi gani cha fedha za kigeni?

(c) Kati ya nazi zinazozalishwa ni kiasi gani hutumika hapa nchini kama chakula?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu: -

Napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ramadhani Hashim Khalifan, Mbunge wa Bagamoyo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba takriban nazi milioni 850 huzalishwa na kuuzwa nchini kila mwaka. Kutokana na kiwango hicho cha uzalishaji; na kwa kuwa wastani wa bei ya nazi moja ni shilingi 150, kila mwaka wakulima wa nazi hujipatia shilingi bilioni 127.5 kutokana na mauzo ya nazi.

Kwa hiyo, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita wakulima wa nazi walijipatia jumla ya shilingi bilioni 637.5 kutokana na zao la nazi zilizozalishwa nchini. Kiasi hicho cha mapato hakijumuishi mapato yanayotokana na mazao ya mti wa mnazi kama vile makuti, makumbi, vifuu vya nazi, samani na pombe ya mnazi. Aidha, yapo mapato mengine yanayotokana na ajira kama vile ukwezi, ufuaji wa nazi na uuzaji wa madafu.

(b) Kila mwaka wastani wa nazi milioni 42.5 huuzwa nje ya nchi, hususan katika nchi za Kenya, Uganda, Visiwa vya Comoro na nchi za Ghuba. Inakadiriwa kwamba mauzo ya nazi hizo hulipatia Taifa wastani wa dola za Kimarekani milioni 6.3 kwa mwaka.

(c) Nazi milioni 807.5 sawa na asilimia 95 ya nazi zote zinazozalishwa, hutumika hapa nchini kama kiungo cha chakula.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swalii moja ndogo la nyongeza. Kwa kuwa yapo malalamiko kwa wakulima wengi nchini kwamba minazi hii mifupi uzalishaji wake wa nazi ni mdogo na unatia hasara wakulima. Ipo miche mingine ya minazi mirefu inaitwa *African tall* inachukua muda mrefu na hiyo ndiyo inazaa nazi nyingi, je, Wizara ya Kilimo na Chakula ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba tunapata mbegu bora ya miche mizuri ili wananchi wa Tanzania waweze kupata nazi nyingi zaidi? (*Makofsi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, ni kweli Wizara ya Kilimo na Chakula iliendesha utafiti kuhusu minazi mirefu nchini hapa na baada ya miaka kumi imegundulika kuwa minazi mifupi haina sifa bora kama ile minazi mirefu. Kwa hiyo, lile zoezi la utafiti limeisha. Kwa hiyo, tutegemee sasa kupata mbegu bora ya minazi mirefu kutoka shamba letu la Chambezi huko Bagamoyo. (*Makofi*)

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja ndogo tu la nyongeza. nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inakiri kwamba zao la nazi ni moja ya zao ambalo linaleta faida kubwa sana katika nchi hii na kwa wananchi. Lakini ukiangalia hali ya wakulima wa nazi hapa nchini ni duni kuliko wakulima wa mazao yote duniani. Sasa ili waweze kuona mwelekeo kuwa zao hili litakuwa na manufaa kwa nini Serikali inasita mpaka leo kuanzisha Bodi ile ambayo imetamkwa kwamba itakuwemo katika yale mazao ya pamoja, pamoja na nazi ili wakulima wa zao hili waweze kusemea na kuona umuhimu wa zao lao?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, kwa kweli Serikali imedhamiria kuendeleza mazao yote nchini sio zao la nazi peke yake. Mazao haya ni yale ambayo kwa hadi sasa hayana Bodi kama vile ilivyo kwa mazao maalum ya biashara kama vile pamba na mengineyo. Serikali inaendelea kuboresha maandalizi ya kuunda hiyo Bodi ya mazao mchanganyiko. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira hili suala litapata ufumbuzi hivi karibuni.

Na. 95

Uchunguzi wa Mradi wa Maji - Matwiga

MHE. NJELU E. M. KASAKA aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali ilituma wataalam kwenda kuchunguza mradi wa maji wa Matwiga uliopo Wilayani Chunya, mradi ambao ulikusudiwa kutoa maji kwenye Kata za Matwiga na Mtanila ambazo hivi sasa zina shida kubwa sana ya maji.

(a) Je, uchunguzi huo ulibaini nini?

(b) Je, ni hatua gani zimechukuliwa za ama kufufua mradi huo au kuchimba visima vyta kutumia pampu za mkono katika Kata hizo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA
(k.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba tu nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Njelu Kasaka, kwa kushinda kesi. Hatimaye sasa atakuwa ametulia na kufanya kazi ya kuwawakilisha wananchi wa Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, naomba kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo: -

Mradi wa Maji wa Matwiga ulibuniwa mwaka 1972, ukiwa na lengo la kuhudumia Vijiji 7 vya Kata za Matwiga, Mtanila, Lupatingatinga na Mamba. Ujenzi wa mradi huu uligharamiwa na fedha za Benki ya Dunia kuititia Mamlaka ya Tumbaku Tanzania (*TAT*). Benki ya Dunia ilisitisha kugharamia mradi huo mwaka 1977 wakati vijiji vyote vilikuwa vimeanza kupata huduma ya maji isipokuwa kijiji cha Mamba. Mradi uliendelea kutoa huduma hadi mwaka 1992 wakati uliposimama kabisa kutokana na wizi wa mitambo yote ya kusukumia maji na bomba. Kutokutumika kwa miundombinu hiyo kwa muda mrefu kulisababisha uharibifu zaidi uendelee kufanyika hasa matanki ya kuhifadhi maji, vituo vya kuchotea maji na chanzo cha maji viliharibika zaidi.

Kutokana na ghamama za kukarabati mradi kuwa kubwa, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark (*DANIDA*), iliweza kuchimba jumla ya visima 23 katika vijiji vya Mamba, Nkungungu na Lupatingatinga ambavyo viliwawezesha wananchi wa vijiji hivyo kupata huduma ya maji kwa mara nyine.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Mbunge, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, tathmini ya mradi wa maji wa Matwiga imebaini kwamba wingi wa maji wa Kijito cha Mkowiji ambacho ndio chanzo cha maji cha mradi mzima yamepungua sana na wakati mwingine hukauka kabisa kutokana na shughuli za binadamu ndani ya eneo la chanzo hicho. Hivyo panatakiwa uchunguzi mpya wa kutafuata vyanzo vya maji mbadala vinavyoweza kukidhi mahitaji ya mradi wa Matwiga.

(b) Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya tathmini hii ni kuchimba visima au kujenga bwawa. Inakadirwa kuwa jumla ya shilingi milioni 212 zinahitajika kwa ajili ya utafiti wa maji chini ya ardhi, uchimbaji visima na kuweka pampu za mkono katika visima 25 kwa ajili ya wananchi wa Kata za Matwiga na Mtanila. Aidha, ujenzi wa bwawa kwenye Mto Mkowiji utagharimu shilingi milioni 260. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kutekeleza mapendekezo hayo.

MHE. NJELU E.M. KASAKA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa hawa wananchi hivi sasa wana tatizo kubwa la maji na Serikali inasema bado inaendelea kutafuta fedha. Kuna hatua gani za haraka basi za kuwawezesha hao wananchi kupata maji. Kwa sababu kwa sasa hivi wakati wa kiangazi hakuna maji, je, Serikali haiwezi kutafuta fedha kwa ajili ya kuchimba visiwa vya haraka haraka ili wananchi waweze kupata maji katika maeneo hayo? (*Makofî*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (k.n.y WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO): Mheshimiwa Spika,

nimeeleza katika jibu la msingi kwamba hata hatua hiyo ya kuchimba visima bado inahitaji kufanyiwa utafiti. Tulichosema ni kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kutekeleza mapendekezo hayo pamoja na kuona hatua za haraka zinazoweza kuchukuliwa kujaribu kupunguza tatizo.

Na. 96

Taarifa ya Hesabu za *AICC* kwa Mwaka 2002

MHE. LEONARD N. DEREFA aliuliza:-

Kwa kuwa nilipokuwa nikisoma Taarifa ya Mwaka ya Hesabu za Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (*AICC*) iliyoishia tarehe 30 Juni, 2002 nilibaini kwamba katika ukurasa wa 15 kuna *depreciation fund* ya mali yenye thamani ya shilingi 4,643,158,501/=.

(a) Je, fedha hizo ziko kwenye *sinking fund* au ni tarakimu tu kwenye vitabu vya taarifa hiyo?

(b) Kwa kuwa *depreciation* ni vema ikawa kwenye fedha taslimu ili kufidia baadhi ya mali endapo zinahitaji kufidiwa na kama fedha hizo haziwekwi kwenye *sinking funds*, je, inamaanisha nini kuonyesha thamani hiyo kwenye hesabu za Kampuni?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, zinazoonekana katika ukurasa wa 15 wa Taarifa ya Hesabu za Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (*AICC*) iliyoishia tarehe 30 Juni, 2002 hazipo kwenye *sinking fund* na wala Shirika halina mfuko huo. Shirika pia halina *depreciation fund* na katika taarifa hiyo fedha hizo zipo kwenye kifungu kiitwacho *Accumulated Depreciation* yaani mkusanyiko wa gharama za uchakavu. Hizi ni tarakimu zinazoonyesha thamani ya jumla ya uchakavu wa mali isiyoondosheka ya shirika.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Leonard Derefa, kwamba njia mojawapo ya kufidia uchakavu wa mali isiyoondosheka ni kuweka fedha taslimu katika *sinking fund*. Njia nyingine ni kutumia Bajeti ya shirika kugharamia uchakavu huo wakati itapohitajika kufanya hivyo. Shirika la Kituo cha Kimataifa cha Arusha linatumia njia ya pili.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, thamani ya uchakavu kuonyesha katika hesabu ili kutambulisha thamani halisi ya mali isiyoondosheka iliyopo wakati huo ili kurahisisha uamuzi na hatua stahili kuchukuliwa kwa wakati muafaka.

Shule ya Msingi Mtoni - Mary Ibrahim Institute

MHE. RHODA L. KAHATANO aliuliza: -

Kwa kuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni inayo dhamana ya kutunza mambo ya kale na kuweka historia ya mambo muhimu yaliyotendwa na Watanzania waliopo na wale waliokufa; na kwa kuwa shule ya msingi Mtoni ilianzishwa na Marehemu Mama Mary Ibrahim ikiitwa *Mary Ibrahim Institute*; na kwa kuwa mama huyo aliwakusanya vijana waliokuwa hawajui kusoma na kuandika akawafundisha bila kulipwa na Serikali na baada ya kukosa nguvu aliikabidhi shule hiyo kwa Serikali.

(a) Kama hivyo ndivyo, je, kwa nini Serikali ilipokabidhiwa shule hiyo haikuendelea na jina la mama aliyeanzisha shule hiyo na kujitolea mali, muda wake kuwafundisha Watanzania?

(b) Kama shule ya Mtoni haikuachwa na Mary Ibrahim, je, shule ya Mama Ibrahim iko wapi na inaitwaje?

(c) Je, kuna shule ngapi zilizoanzishwa na wananchi na majina yao yamefutwa bila sababu na kwamba kwa kutowakumbuka walimu waliojitlea kufanya kazi kwa vipawa vyao katika mazingira magumu kunaua moyo wa wale wanayoyaona hayo na Serikali inalo la kusema kuhusu kufisha mioyo ya watumishi wake waliostaafu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa utangulizi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Shule ya Msingi Mtoni au *Mary's Institute* kama ilivyokuwa ikiitwa wakati ilipoanzishwa ipo katika Manispaa ya Temeke katika Mkoo wa Dar es Salaam. Shule hii ilianzishwa mwaka 1959 na Mama Mary Ibrahim. Ilianza ikiwa na jengo moja na wanafunzi 7 ikiitwa *Mary's Institute*. Mwaka 1971 ilikabidhiwa kwa Serikali na kuitwa Shule ya Msingi Mtoni. Hadi sasa imekuwa ikiendeshwa na Serikali chini ya Manispaa ya Temeke kama ilivyo kwa shule za Msingi za Serikali. Mwaka 2002 shule hii iligawanywa na kuwa shule mbili. Shule ya Msingi Mtoni na Shule ya Msingi Bokorani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Rhoda Kahatano, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Mama Mary Ibrahim kwa hiari yake aliikabidhi shule hiyo kwa Serikali. Wananchi walimwomba shule hiyo iitwe Shule ya Mtoni kwa Mama Mary lakini kwa ridhaa yake, kabla ya kifo chake akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Shule alisema jina litakuwa refu mno hivyo aliomba iitwe Mtoni.

Mheshimiwa Spika, inaaminika aliomba hivyo ili kuondoa dhana ya kuwa ni shule ya mtu binafsi na kuwataka wakazi wa eneo hilo wajivunie kuwa ni shule yao ambayo inawapatia watoto wao elimu. Inaelekea mama huyu hakuwa na ubinafsi. (*Makofî*)

(b) Mheshimiwa Spika, shule ya Msingi Mtoni ndiyo ilioachwa na Mary Ibrahim na kijiografia ipo mahali pale pale shule ya zamani ilipokuwa imeanzishwa. Hata baada ya kuikabidhi shule kwa Serikali, Mama Mary Ibrahim aliendelea kushirikiana na wakazi wa eneo hilo katika mikutano, uhamasishaji na michango ya hali na mali katika kuendeleza shule hiyo. Mpaka sasa shule hiyo ina madarasa I hadi VII yenye jumla ya wanafunzi 2,264 na walimu 46.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haina rekodi ya shule zilizoanzishwa na wananchi ambazo majina yao waanzilishi hao yamefutwa. Kwa utaratibu wa kawaida mwenye shule anapoomba kuanzisha shule yake hutaja jina analopendekeza. Wizara yangu hutoa ushauri kwa mwenye shule kutumia jina lingine endapo analopendekeza limekwisha kutumiwa na shule nyingine au linakiuka masharti ya kutumika kama Mtakatifu, *Academy au International*.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na wazo la Mheshimiwa Mbunge kuwa inafaa kuendelea kuyatumia majina ya waanzilishi wa shule hizo ili yawe sehemu ya kumbukumbu zetu za kihistoria.

MHE. RHODA L. KAHATANO: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa amekiri kwamba ni vizuri kwa kuwakumbuka watu ambao walifanya kazi njema katika nchi, je, Wizara itakuwa tayari sasa kuita shule ile Mary Ibrahim kumkumbuka kwa sababu tumeona kwamba ni mtu alikuwa hana ubinafsi basi sisi tukamhenzi? (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI): Mheshimiwa Spika, Wizara ingependa kukubaliana na wazo la Mheshimiwa Mbunge lakini kwa sababu mwanzilishi wa shule hii ni marehemu na yeze mwenyewe kabla ya kifo chake hakutaka iitwe kwa jina lake tutakuwa hatumtendei haki kwa sababu hana nafasi ya kujitetea wala kujieleza.

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri alisema mama aliyeanzisha ile shule alikataa jina kwa madai kuwa lilikuwa ni refu, hoja ilikuwa ni kwamba jina litakuwa refu na kwa jibu kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Rhoda Kahatano, angeomba sasa muiite Mary Ibrahim haliwezi kuwa refu, sasa kwa nini anasema hawamtendei haki? (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI): Mheshimiwa Spika,

wakati wa uhai wa Mama Mary Ibrahim, mambo mawili aliyakataa. Jina kuwa refu na ndicho Wizara ilichotekeleza. Hili la pili kama nilivyosema sasa hivi Mama Mary Ibrahim ameshatangulia mbele ya haki, tutakuwa hatumtendei haki tukifanya kile ambacho hakupenda yeze kifanyike wakati wa uhai wake. (*Makofî*)

Na. 98

Uanzishwaji wa *Academy* na *International School*

MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA aliuliza: -

Kwa kuwa katika miaka ya hivi karibuni kumezuka mtindo wa kuanzisha taasisi zinazoitwa *Academy* na shule za Kimataifa (*International Schools*).

- (a) Je, ni sifa gani zinazotakiwa kwa taasisi kuwa *Academy* na *International*?
- (b) Je, ni taasisi na shule zipi zinakidhi sifa hizo na ni zipi hazikidhi sifa husika?
- (c) Je, Serikali inao utaratibu wa kuanzisha taasisi kama hizo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, hakuna sifa yoyote ya taasisi kuandikishwa jina la neno *Academy* lakini Afisa Elimu Kiongozi amezuia utumiaji wa jina hilo kiholela katika majina ya shule. Neno *International* linaloruhusiwa kuwemo katika jina la shule ambayo ni mwanachama wa mojawapo ya mashirika ya shule Kimataifa kama vile *Association of International Schools in Africa (AISA)* na *European Council of International Schools (ECIS)*.

(b) Mheshimiwa Spika, zipo shule 17 zifuatazo zilizosajiliwa na Wizara yangu kuwa za Kimataifa baada ya kutambuliwa na *AISA* au *ECIS* ambazo ni *St. Constatines's School*, Arusha; *Braeburn School*, Arusha; *International School of Tanganyika*, Dar es Salaam; *Academic International School*, Dar es Salaam; *Laureate International School*, Dar es Salaam; *Haven of Peace Academy*, Dar es Salaam; *Esacs Academy International*, Dar es Salaam, *St. Mary's Academy*, Dar es Salaam, *St. Mary's International School-Mbezi Beach*, Dar es Salaam; *Kwanza International School*, Dar es Salaam; *Canon Andrea Mwaka International School*, Dodoma; *Iringa International School*, Iringa; *Morogoro International School*, Morogoro; *International School Moshi*, Kilimanjaro; *Isamilo International School*, Mwanza; *Tanga International School*, Tanga na *International School Moshi Arusha Camps*, Arusha.

Aidha zipo shule sita zilizosajiliwa kwa kutumia neno *Academy* kabla ya Wizara kutoa mwongozo wa kutotumika kwa neno hilo kiholela na shule hizo ni *Naasha Junior Academy*, Arusha; *Moshi Academy*, Kilimanjaro; *St. John Bosco Academy*, Mara; *Kilimanjaro Academy* (Mama Clementina), Kilimanjaro; *Mwenge Open Academy*, Dar es Salaam na *Tanzania Cambridge Academy*, Dar es Salaam.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekwisha kutoa utaratibu wa kutumia maneno *International, Saint* na *Academy* kupitia nyaraka mbalimbali. Neno *Saint* linaruhusiwa kwa uthibitisho wa idhini kwa maandishi ya Baba Askofu wa dhehebu la dini lililosajiliwa na Serikali. Neno *Academy* linawenza kuruhusiwa kuwemo katika jina la shule kwa sababu maalum inayozingatia maana sahihi ya neno hilo.

MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa amekiri kwamba kuna shule ambazo zinajiita *Academy* bila utaratibu, je, Serikali imechukua hatua gani kuzifunga au wabadili jina?

Je, kuna tofauti gani kati ya hizi *Academy* na *International Schools* na shule za Serikali za vipaji maalum?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA k.n.y WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI): Mheshimiwa Spika, kwanza pengine ni vizuri tukajua chimbuko la neno *Academy*.

Neno *Academy* kwa lugha ya Kifaransa ni *Academ - academy* na kwa Kilatini ni *academia* lakini ukitaka kupata maudhui yake ukisoma katika *dictionary* ya *Short Oxford English* ambayo nilikuwa naangalia asubuhi hii inasema: “*Academy is the name of the garden where Plato thought.*” Ni jina la bustani ambako yule mwanafalsafa Plato alikuwa anafundisha. Ndiyo imezaa neno *academy* wale wanaosoma wakatafuta kuboea katika fani wanayosomea.

Sasa kwa maana inavyotumika kwa shule zetu, kitabu hicho hicho yaani hiyo *dictionary* inasema: “*Academy is the school claiming to rank between a college and an ordinary school,*” yaami ni shule inayosema ni zaidi kidogo kuliko shule nyingine inakaribiana na Chuo Kikuu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, haya si maandishi yangu ni maandishi ya wana taaluma. Sasa Mheshimiwa Mbunge ameuliza hivi baada ya Wizara kusema imegundua hivyo hizi shule zinazotumia neno hili imechukua hatua gani kuzifuta. Tulichokisema ni kwamba hatupendi kuzifuta lakini kama wanaelewa maana ya neno hili basi watatafuta kuboresha shule zao ziwe katika kiwango hicho. Kilichozuiliwa ni kuendelea kutumia neno hili kiholela. (*Makofi*)

La pili kwamba sasa hizi shule *academy* zina tofautiana vipi na shule za Serikali zenye vipaji maalum. Mimi nadhani kwanza ni vizuri ikaeleweka shule hazina vipaji maalum isipokuwa wanafunzi ndiyo wenye vipaji maalum. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika katika hizi shule za vipaji maalum ni kuendeleza vipaji maalum vya wanafunzi wale.

Na. 99

Reli ya Musoma - Arusha

MHE. JOEL N. BENDERA (k.n.y. MHE. IBRAHIMU W. MARWA)
aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika siku zilizopita ilifanya utafiti na kubaini umuhimu wa kiuchumi wa kujenga reli kati ya Arusha na Musoma ili kuunganisha nchi yetu kiuchumi na nchi za Maziwa Makuu ikiwemo Uganda, DRC, Rwanda na kadhalika; na kuwa reli hiyo itawezesha Bandari ya Tanga kufanya kazi kwa kiwango cha faida hapo baadaye kuliko hali ilivyo kwa sasa; na kwa kuwa miundombinu ya reli ni muhimu sana kwenye ujenzi wa uchumi wetu; na kwa kuwa Serikali ya Uganda chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Yoweri Museveni, imeonyesha nia ya kushiriki katika ujenzi wa reli hiyo kwa kuchangia gharama za ujenzi: -

- (a) Je, ni gharama kiasi gani kinahitajika kuweza kujenga reli hiyo?

(b) Je, Serikali inakiri kuwa kuna faida kubwa za kiuchumi ambazo zinapatikana endapo reli hiyo itajengwa; na kama hivyo ndivyo, kwa nini tuchelewe kuanza wakati wenzetu wa Uganda wapo tayari kushirikiana nasi?

(c) Je, kama *TRC* ikibinafsishwa, jukumu hilo litafanywa na chombo kipi?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Ibrahimu Wankanga Marwa, Mbunge wa Musoma MJini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, għarama ya kujenga reli hiyo itajulikana baada ja kufanya na kukamilika kwa upembuzi yakinifu. Upembuzi huo umechelewa kufanyika kutokana na kusubiri fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika ambayo ndiyo ilioonyesha nia ja kufadhili. Kwa hiyo, kukamilika kwa upembuzi yakinifu ndiko kutatoa dira ja mradi huo. *TRC* itakapokodishwa jukumu la kuendeleza reli litafanywa na *Reli Assets Holding Company* kama tulivyopitisha na Bunge lako kwa niaba ja Serikali.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ilikwishaamua muda mrefu kujenga reli hii na wenzetu wa Uganda wameshatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli hii kwa kushirikiana kati ya Tanzania na Uganda na Mheshimiwa Waziri amesema bado wanashubiri na katika kipindi hiki ambacho nchi yetu imeingia katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga reli hii kwa uchumi wa nchi?

La pili, bandari ni uchumi, mimi naamini kabisa kwamba reli hii ya kutoka Arusha - Uganda kwa maana ya Tanga ikitumia bandari ya Tanga, Serikali haioni kwamba ni muhimu reli hii kuwepo hasa kipindi hiki ambacho ni wakati muafaka tukiwa tunafufua uchumi wa nchi yetu hasa kwenye kuboresha bandari ya Tanga?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwanza labda nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba hapo awali Serikali ya Tanzania na Uganda zilikuwa zichangie nusu ya jumla ya fedha za stadi ambazo zilikuwa ni *US\$ 4.5 million* na fedha hiyo Tanzania tukaweka kwenye Bajeti lakini kwa bahati mbaya Uganda hawakuweka kwenye Bajeti yao.

Mara ya pili, ikawa vile vile lakini baadaye tukakubaliana Tanzania na Uganda tulifanya suala hili kwa pamoja kwa sababu ni *interest* ya Tanzania na Uganda kwa reli hii na ndiyo maana tukalizumza na tukalipeleka suala hili kwenye *East African Community* na *through East African Community* ndiyo hivi sasa fedha zinatafutwa za kufanya stadi ya reli kutoka Arusha kwenda Musoma.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana nae Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna umuhimu wa kuboresha reli hii ili bandari ya Tanga iweze kufanya kazi zake ipasavyo na kama atakubaliana nami tulikubaliana kwamba si hilo tu ni pamoja ikiwezekana na kuihamisha bandari pale ilipo kupeleka kule Mwambani kama hali itaruhusu ambapo kina kikubwa cha maji na kutoka Mwambani kutahitaji kutengenezwa reli itakayounga na ile nyininge pale hayo yote ni masuala ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi.

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba bandari ya Tanga imboreshwa vya kutosha na hivi sasa inatoa huduma afadhali zaidi kuliko ilivyokuwa. Lakini hapo nyuma licha ya uboreshaji, *capacity* yake ilikuwa ni kubwa lakini huduma waliyokuwa wanatoa ni ndogo. Mimi naamini tutajitahidi tuweze kuboresha shughuli hizi na wananchi wa Tanga watafufua zao la katani na zao la chai na mazao mengine ili reli hii itakapokamilika iweze kubeba shehena hiyo. (*Makofi*)

MHE. ALLY A. KARAVINA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa sababu muundombinu huu ni muhimu sana katika kuhakikisha nchi inavuna uchumi wake wa jiografia na kwa bahati mbaya ni kwamba inashindana na reli iliyoko Kenya pamoja na miundombinu iliyoko Kenya kwa sababu nchi yetu ndiyo itafaidika na uchumi huo basi Serikali haioni kwamba *time is no essence* ya kwamba muda wa kufanya haraka ni muhimu ili tusiweze kushindwa na kunyang'anywa ile *comparative advantage* tuliyonayo kwa kutumia *competitive advantage* ya Kenya?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye *time is no essence* kwa masuala haya na ni suala la fedha kama tungkuwa tuna fedha masuala unayozungumza ambayo na sisi yanatukereketa, uchumi wa kijiografia ni muhimu sana katika karne hii tuliyonayo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, labda nikupe tu kidogo, kujenga reli bila ya Daraja kilometra moja ni dola laki sita, kutoka Arusha kwenda Musoma ni kilometra 548, ni kiasi gani kwa Tanzania hatuwezi kumudu bila kupata ufadhili au kufanya kwa pamoja.

Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge hilo lipo na hata kwenye Ilani yetu ya uchaguzi limewekwa, ni juu yetu kuona angalau *feasibility study* tunaweza kufanya na pesa itakapapatikana reli ya Arusha - Musoma inajengwa na tutaweza ku-open up kwa upande ule na ushindani utakuwa ni mzuri kwa sababu na sisi tutaweza kuitumia Bandari yetu ya Tanga ipasavyo. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na yamekwisha kabla ya wakati wake lakini ni jambo zuri kwa sababu kalenda ya mwezi Mtukufu wa Ramadhanina inaonyesha kwamba mwezi 29 utakuwa Jumamosi kwa hiyo tulikuwa wengine tuna mawazo kama tunaweza kumaliza Mkutano huu Ijumaa asubuhi ili wale wanaokaa mbali kama Zanzibar ili waweze kwenda na kuwahi kuwa na familia zao lingekuwa jambo zuri. Kwa hiyo, nitaendesa shughuli kwa lengo hilo. Ahsante sana.

Sasa utambulisho wa wageni kwanza nawatambulisha wageni wa Spika ambao wako kwenye *gallery* ya Spika. Waliokaa kwenye *gallery* ya Spika ni Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. (*Makofi*)

Wamekuja Dodoma kwa madhumuni ya kucheza mpira siyo na timu yetu na timu nyingine lakini wamepata nafasi ya kuja kututembelea, tunawakaribisha. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kuna mgeni wa Kimataifa ambaye naye amekaa kwenye *gallery* ya Spika yeze ni mgeni wa Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, anatoka *International Fellowship Foundation, Washington DC.* (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, anao wageni hapa Bungeni leo ni wanafunzi wa *Chikuyu Secondary School*, Manyoni na mwalimu wao mmoja wamekuja hapa kama sehemu ya somo lao la Uraia (*Civic Education*). (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Eliachim Simpara, hawa ni wajumbe wa *University Students Representative Council* wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, naamini wamekuja hapa nao katika juhudii zao za kuijendeleza katika suala la *Civic Education*.

Mgeni wa Mheshimiwa Venance Mwamoto, ni mwenyekiti wa Baraza la Wazee Kilolo, Ndugu Amos Kisoma. (*Makofi/Kicheko*)

Matangazo ya vikao vya Kamati, leo tuna Kamati zifuatazo ambazo zitafanya vikao vyake kwanza ni Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wake anaomba wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii wakutane chumba namba 133 saa tano asubuhi hii.

Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba wajumbe wa Kamati wakutane leo saa sita mchana katika chumba namba 227.

Kamati ya Hesabu za Serikali, Mhehsimiwa Profesa David Mwakyusa, Makamu Mwenyekiti wake anaomba wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali wakutane leo saa tano asubuhi chumba namba 219.

Kamati ya mwisho ni Kamati ya Fedha a Uchumi, wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo saa tano chumba namba 231.

Mwisho wa matangazo, Katibu endelea na *Order Paper*.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Taratibu za Kuwaenzi Waasisi wa Taifa wa Mwaka 2004
*(The Founders of the Nation
(Honouring Procedures) Bill, 2004)*

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Katika orodha ya walioomba kuchangia Muswada huu ninao Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Eliachim Simpasa, watatu wa mwanzo wengine watafuata baadaye. Namwita Mheshimiwa Leonard Derefa.

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Muswada huu.

Kwanza napenda niunge mkono kwamba hoja hii ni nzuri na itatusaidia kutatua matatizo mbalimbali ambayo tumekuwa nayo.

Katika Muswada huu nilikuwa naomba vile vile Serikali na nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri aongeze kifungu kimoja hapo hasa kuhusu mazishi ya viongozi wetu wakuu na mimi nikiwa nashauri kwamba kifungu kiwepo cha kuhakikisha kwamba viongozi wetu wakuu wanapokufa wajulikane mahala wanapozikwa na nilikuwa nashauri kwamba viongozi wakuu wazikwe katika eneo la Bunge na mtindo uliopo wa sasa hivi kila kiongozi mkuu anapokufa anapelekwa kwao hatuiwekei mikakati mizuri ya kuwa na viongozi wetu na mimi nilikuwa nashauri kwamba hata ukienda nchi nyingi utakuta kwamba viongozi wengi wanazikwa katika maeneo ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, viongozi wakuu kwa mfano kama Rais anafanana kama *Bishop* kwenye Kanisa na mara nyingi *Bishop* anapofariki mahali pa kuzikwa ni Kanisani kwake kwa *Bishop*.

Mheshimiwa Spika, vile vile nilikuwa nashauri kwamba kwenye zile sanamu nilikuwa nashauri kwamba tufuate utaratibu kwa mfano wa kule Amerika sehemu za *South Dakota* kuna pale wanaita *Mountain Rushmore National Park* nilikuwa nashauri kwamba katika mlima wa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mlima ulioko maeneo ya *Area D* ichongwe sanamu kama zilizochongwa pale *Mountain Rushmore Park* kule Amerika ninaamini kabisa kwamba kuna baadhi yenu mmewahi kufika pale na mkaona na kwenye ule mwamba mkubwa pale wangeweza wakachonga, wakaweka ile sanamu ya Baba wa Taifa, halafu kwenye lile jiwe dogo wangeweza wakachonga tukaweka sanamu ya Karume na sanamu hizo zingependeza sana sababu zingeuangalia mji wa Dodoma na kwa kuwa Baba wa Taifa ndiyo mwanzilishi wa Mji huu ingekuwa ni vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, lingine nilitaka nishauri ni kwamba tutakapoanzisha sheria hii, Serikali iwe inatenga hela za kutosha katika kuhudumia, tusije tukapata aibu kama tulioipata mahali alipofia Waziri Mkuu, Marehemu Edward Sokoine. Sehemu hiyo inaonekana kwamba Serikali pamoja na kwamba ilianzisha, haipatunzi vizuri maana yake pamechakaa sana na tusije tukaanzisha sheria hii halafu tukapata aibu ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, lingine nilikuwa nataka niseme kwamba katika hizi sanamu zile *stack use* zinapotengenezwa lazima zifanane na waasisi wetu kwa mfano ile *stack use* iliyotengenezewa huko Mwanza ilionekana inahitilafu sana, nilikuwa nashauri kwamba mahali popote ambapo tunatakiwa tufanye hii kazi lazima patengenezwe vizuri na kwa heshima zote na hii itatuwezesha kuwaenzi vizuri waasisi wetu pamoja na viongozi wetu wakuu.

Mheshimiwa Spika, vile vile nilikuwa nasema kwamba maeneo haya yatakapotengenezwa hasa ya kutunza zile nyaraka lazima yatengenezwe kwa umahili sababu nakumbuka hata hapa sisi Bungeni pale baada ya Bunge kuhamishwa kutoka Dar es Salaam, *library* yetu kuna vitu vingi sana viliharibika hasa wakati *library* ilipokuwa pale mjini ambako sasa hivi kuna TAMISEMI sababu ile *roof* ilikuwa inavuja na naamini kabisa kwamba tutakopofanya vitu hivi tuhakikishe kabisa kwamba mahali pa kutunza nyaraka hizi panakuwa pazuri na kwamba nyaraka zisiwe zinaharibika.

Mheshimiwa Spika, waasisi wetu vile vile ni vyema tukawaenzi kwa kuhakikisha kabisa kwamba kila kitu hasa hasa nilikuwa naomba fedha za kutosha ziwe zinatengwa kwa ajili ya kuhudumia maeneo haya. Ukienda kwa mfano kama Washington kule utaona picha za viongozi *stack use* na sanamu za viongozi karibu wote wa Marekani wamewekwa na sisi kama Taifa hili ni vyema mahala ambako patachaguliwa kwa ajili ya kuweka *cord* na sanamu za viongozi wetu na sisi tukafuata mtindo kama huo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo machache ya kuongea katika Muswada huu na nitaomba nimkabidhi, nitampelekea Mheshimiwa Waziri picha ya *Mountain Rushmore National Park* aione inavyofanana. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, jiandae na Mheshimiwa Rosemary Nyerere, jiandae.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu kidogo kuhusu Muswada wa Sheria wa Taratibu za Kuenzi Waasisi wa Taifa letu wa mwaka 2004.

Awali kabisa napenda kumpongeza sana Waziri Mhehsimiwa Dr. Mary Nagu, kwa kuleta Muswada huu muhimu.

Vile vile napenda kumpongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Bwana Joseph Rugumyamheto, pamoja na wasaidizi wake kwa kumsaidia Waziri kuandaa Muswada huu ambaa kwa kweli ultaka watu wakae chini, wafikiri vizuri nini cha kufanya. Hili suala la kuenzi viongozi lilikuwepo, lakini utakuta tunadonoadonoa tu, kwenye sherehe labda watu wanazungumza na kadhalika, lakini kwa kweli hakukuwa na sheria rasmi ambayo inaeleza kwamba kifanyike hiki na hiki. Sasa imetufikisha mahali pazuri. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume, hatuwezi kuwalinganisha na watu wengine. Jana hapa wakati mwakilishi wa hoja za Upinzani alizungumza kwamba tunabagua, kuna waasisi wengi, jamani waasisi wa Taifa mimi nawafahamu, nawajua ni wawili, sijui wengine. Maana yake hapa lazima tuwe wazi, waasisi mimi ambaa nawafahamu na Serikali inawafahamu waasisi wa Taifa la Tanzania ni wawili, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume. Hawa waasisi wengine wanahitaji utaratibu mwingine na si vibaya litazamwe hilo. Katika hili nadhani kuna watu wengine watachangia waasisi wengine.

Kwa mfano, leo hapa mimi nilimsikia Mama Mary Ibrahim, ni mtu wa kuenziwa huyu kwa kweli. Kwa hiyo, hatukuchelewa ijapokuwa jibu la Waziri ni kwamba alikataa. Ni vizuri akatae kwa sababu alikuwa hajafa, lakini sasa hivi amekufa na sasa ndio tunatakiwa tumfikirie, kwa hiyo, wapo watu wengine. Baada ya sheria hii kwa kweli tungeangalia utaratibu mwingine wa kuwaenzi watu wengine maarufu katika Taifa letu ili tuwe na rekodi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kituo hiki ambacho kimependekezwa kuanzishwa mimi nakiunga mkono kabisa kianzishwe kwa sababu hapa ndio mahali ambapo tungeweza kufanya mambo mengi. Sasa ni vizuri baada ya sheria hii kupita tufanye *amendments* za kuongeza kuasiisi watu wengine. Tutunge sheria nyingine ya kuasiisi watu mbalimbali, viongozi mbalimbali katika Taifa letu. (*Makofî*)

Vile vile napenda kuunga mkono kabisa kuanzisha mfuko wa hifadhi. Nadhani ni hatua nzuri sana kwa sababu fedha ambazo nadhani Mheshimiwa Waziri baada ya sheria kupita ataleta *Supplementary Budget*, fedha hizo zikienda kwenye mfuko hazitahusika tena na kurudishwa rudishwa, zitakuwa ni kule kuendelezwa shughuli zao. Kwa hiyo, kama wamepanga mipango, wanajua tumetengewa kiasi hiki waweze kuendeleza hiyo azma ya kutunza na kuenzi kumbukumbu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika hizi kumbukumbu nadhani tuwe waangalifu, sio lazima kumbukumbu zote ziwe mahali pamoja. Kwa mfano, kumbukumbu moja muhimu sana ni kujua viongozi hawa waasisi wa Taifa letu walizaliwa mahali pa namna gani.

SPIKA: Samahani kidogo Mheshimiwa William Shellukindo, utaendelea baadaye.

Niliwatangazia Waheshimiwa Wabunge kutokuwepo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu Bungeni, sasa napenda kuwajulisha kwamba amesharejea Bungeni na ameshika nafasi yake. Endelea Mheshimiwa William Shellukindo. (*Makofi*)

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilikuwa nasema hizi kumbukumbu sio lazima zikusanywe mahali pamoja, ni vizuri ziangaliwe ni vipi zinaweza kwenda kwenye kituo na zipi ambazo zingetunzwa kule kule zilipo. Kwa mfano kitu cha kwanza kabisa ni kuangalia waasisi wetu hawa walizaliwa kwenye mazingira gani. Kwa mazingira hayo ndiyo yaliyojenga fikra zao za kuwa waasisi wa Taifa hili. Kwa sababu mtu kama umezaliwa kwenye ghorofa hutamfikiria mtu aliyezaliwa kwenye kibanda hata kidogo wala kwako wewe haingii akilini. Lakini kama umezaliwa kwenye nyumba ya tembe basi hisia zako zote wakati wote utakumbuka watu wale walioko kwenye matembe kule.

Kwa hiyo, nadhani kitu cha kwanza kabisa cha kuangalia hiyo, Mwalimu alizaliwa mahali gani, nyumba gani kama hiyo nyumba imebomoka basi wako wazee wanaijua ilikuwaje, ijengwe ya namna hiyo hapo kuonyesha kwamba hapa ndipo alipozaliwa. Kwa hiyo, kumkuta Butiama ya sasa pale alipo sio mazingira aliyozaliwa, yale ni ya sasa hivi. Kule mwanzoni kumuenzi chanzo chake.

Nilikuwa nasema ni vizuri ahifadhiwe huko huko hii ni kulinda uhalisi wake kwa Kiingereza tunasema *preservation of the originality*. Kwa sababu nyumba iliyoko Butiama ukijengenja Dar es Salaam ni *out of place* haiwi *original*, inatakiwa kwenye mazingira yale ya mahali pale. Mahali alipozaliwa Sheikh Karume, ni tofauti na mahali alipokutwa wakati anafariki. Sasa turudi kule kwa sababu hayo mazingira ndiyo alioweka fikra za Taifa na kujitolea kwa Taifa kuliko tukiachachia hivi hivi juu juu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri Wizara hii jana Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha hoja yake alisema wametembelea Amerika, Canada nadhani na Uingereza. Sasa mimi napendekeza Mheshimiwa Waziri mtembelee India muangalie na kujifunza Wahindi walimuenzi vipi Mahatma Gandhi. Baba wa Taifa hilo wamemuenzi vipi na ni kumbukumbu zipyi, kwa sababu hao tuko karibu nao sana kwa sababu ya *struggle* ya Uhuru, ni tofauti kabisa na hizo nchi nyingine. Kwa sababu Gandhi kama mnakumbuka sana alikuwa na kipaji cha kuzungumza na wananchi wake na kuwatuliza na alikuwa na hisia za uvumilivu za hali ya juu. Kwa hiyo, aliwfundisha kitu kinaitwa *passive resistance* watu wanatembea hawachukui magongo wanapigwa hawapigi.

Kwa hiyo, huu ni urithi ambao umewaachia kuvumilia na kuvumiliana mpaka wamefikisha Taifa la Wahindi sasa hivi lina heshima kubwa sana. Huu ni urithi ambao pengine hatuwezi kuukuta mahali unaelewa hivi. Kwa sisi Watanzania Marehemu Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume, wametuachia urithi ambao ni vizuri tukatafute namna ya kuuenzi au kuutambua. Urithi huo ni uvumilivu na kupenda Taifa letu. Hayo mawili mimi kwangu nimeona wametuachia hayo, uvumilivu na kupenda Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Profesa Ali Mazrui, aliandika vitabu vingi sana kuhusu Afrika na mambo mengine ya Afrika ambayo nje hayajulikani. Kwa upande wa kitabu ulichoandika kwa Watanzania aliandika kitu fulani ambacho hakiko mahali pengine, aliandika kwamba ukifika Tanzania kuna aina ya ugonjwa hivi sio UKIMWI, hapana hatuzungumzii UKIMWI. Anasema ni kama ugonjwa hivi na akaita *TANZAFIRIA*.

Mheshimiwa Spika, *TANZAFIRIA* mimi kwangu niliona kwamba ni hali ya uvumilivu na uzalendo wa kupindukia. Tumepata taabu kubwa sana hapa lakini Watanzania walikuwa wanafurahi, wanacheka na wanafanya mipango, hali hii haipatikani mahali popote pengine. Sasa hayo yote yalitokana na Waasisi wetu lakini hivi vizazi vinavyokuja vitaijua hii *TANZAFIRIA*.

Mimi naona inaanza kupotea kwa sababu mimi nilishangaa sana watu wengine wanazungumzia kuwa na *double citizenship*, hawa ndio hawana ile *TANZAFIRIA*, kupenda Taifa lako. Sasa kama maendeleo ni madogo lakini tengeneza hapo kwako. Ambaye hajaingia kwenye kichwa chake hakijakaa sawa sawa akaingia na *TANZAFIRIA*, uvumilivu na kupenda Taifa lako kupindukia basi atataka awe na uraia wa pili. Hivi Mtanzania unataka uraia wa pili huu unawaza vipi?

Mheshimiwa Spika, uraia wa pili watu wengine hawajui wametoka wapi. Watu wako Canada kule hajui anatokea wapi, mtu yuko Uingereza hajui anatokea wapi. Mimi najua nilipotokea. Sasa uraia wa pili mimi utanisaidia nini? *TANZAFIRIA* kupenda Taifa lako huu ni urithi ambao tumeachiwa na Waasisi wa Taifa letu na ni vizuri tukauenzi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nilitaka kulidokeza hapa ni kwamba kuna Watanzania kwa kupenda hawa viongozi wetu hawa Marehemu wametumia kumbukumbu zao na wamezitumia, hakukuwa na mwongozo wowote. Baadhi wamezitumia vizuri na kuwaeleza vizuri, baadhi wamezitumia ovyo ovyo.

Sasa mimi naomba katika sheria hii tuseme hao wasibanwe na hii sheria, isipokuwa wale ambao wametumiwa ovyo ovyo waelekezwe, warekebishwe. Lakini sasa kuanzia sheria ikianza hizo kumbukumbu zitaongozwa na hizi taratibu ambazo zimeanza. Hili ni vizuri kulikumbuka. Kuna vitabu vingi tu vimetolewa na picha hizo mtu akachagua mwenyewe picha akaiweka pale, nyingine labda mke wake alipigwa na Mwalimu naye akaiweka pale kwa wao binafsi kwa mambo yao hayo. Sasa ni vizuri tukaangalia huko tunakokwenda kwamba huyu mtu anaitumia hii kwa ajili ya faida ya Taifa letu litumike vizuri.

Kuhusu eneo la ada, nimefurahi sana kwamba wameweka hizo ada, vitu vingi vya bure kwa kweli havina thamani. Ni vizuri hivi vitu ambavyo ni vya kuenzi Waasisi wetu wa Taifa viwekewe ada lakini ada yenyewe isiwe kubwa. Vile vile ada hiyo ingepambanua kati ya watu wazima halafu na wanafunzi na watoto wadogo. Tufanye hivyo kama tunavyoifanya kwenye Mbuga za Wanyama ili maeneo hayo kwa kweli yaweze kuwa ni maeneo ya kuelimisha vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo ambalo nilitaka kulichangia lakini mwenzangu Mheshimiwa Leonard Derefa, amelichangia.

Mimi napenda kusisitiza tu uniwie radhi, hili suala la kuweka mahali maalum pa kuzika viongozi wetu. Kwa kweli hili suala tungeliangalia mapema kwa sababu kipindi cha Urais na uongozi ni miaka kumi. Sasa tusiwape viongozi hawa matatizo ya kuanza kuangalia na kuandaa mahali atakapozikwa iwe hiyo hiyo ni kazi ya Taifa hiyo. Vile vile taratibu hizi zibadilike kwa sababu tukisambaza maeneo ya kuzika kila mtu mahali pake baadaye watapotea hawa hata utunzaji vile vile ni gharama kwa Taifa. Lakini kama kuna mahali pazuri ndio namna ya kuwaenzi, hapo wamefanya kazi nzuri atengenezewe mahali pazuri pa kupumzika, hili nadhani tusilionee aibu kwa kweli ijapokuwa Kiafrika kwanza kuzungumzia kumzika mtu unaonekana kama ni mtu wa ajabu, lakini tumefika wakati lazima tufikirie masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache napenda tena kumshukuru Mheshimiwa Waziri, nasema naunga mkono kwa asilimia mia moja Muswada huu. (*Makofii*)

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA: Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi nichangie katika Muswada huu. Kwanza naunga hoja mkono mia kwa mia. Niseme tu kwanza kwamba naipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao tumeungojea kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kimenifurahisha sana ni kwamba Serikali sasa inafikiria kujenga kituo cha kuhifadhi kumbukumbu mbalimbali za viongozi wetu wale Waasisi wawili, Mheshimiwa Marehemu Nyerere na Marehemu Karume. Wakati huo huo ningependa tu kusisitiza kwamba ili yale maeneo muhimu ambayo yatakuwa yameainishwa yaweze kutunzwa, kuendelezw na kuhifadhi vitu kama majengo na kumbukumbu zenywewo hizo. Kwa kweli ili yaweze kutunzwa, kuendelezw na kuhifadhiwa vizuri ni vyema kabisa Serikali ipewe mamlaka au madaraka ya kufanya hivyo. Wakishakuwa wanajua na hapa nasema wanafamilia watuelewe kwamba kama Serikali haiwezi kuweka suala hili katika sheria basi ni vigumu sana Serikali kuomba fedha kwenye Bajeti kwa ajili ya kutunza majengo hayo.

Kwa hiyo, kama Serikali yenyewe itahifadhi, itaendeleza maeneo yale na itaendelea kuyatunza, kwa vyovyote vile itahitaji fedha na kwa hiyo, naomba tukubaliane kwamba yaweze kutunzwa maeneo hayo na Serikali yenyewe. Lakini hii haikatazwi kwamba wanaohusika, wanafamilia waweze kuyatumia, kwa sababu watayatumia kama vile nyumba ya Serikali mtu anakaa lakini inatunzwa na Serikali. Hili lisitie hofu hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo mimi nilikuwa nafikiri ni zuri ni kwamba Serikali itaamua kukusanya kumbukumbu muhimu na maandiko mbalimbali na kuyatumia kuweka kwenye kituo hicho ambacho tunashauri wale watakaoteuliwa kuwepo pale wawe ni watu kwa kweli wamesomea na ni watu waadilifu na ni watu wenye moyo wa kutunza kumbukumbu, maana utunzaji wa vitu una tabia yake. Kuna watu wanatunza vitu na wengine hawatunzi.

Kwa hiyo, tunaomba wateuliwe watu ambao kwa kweli watafanya kazi kwa uadilifu na kwa utaalamu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kwamba maeneo ya sasa hivi hata huko nyuma tulikuwa tunakaa mahali fulani panajengwa jengo lakini bila kuwa na hatimiliki. Sasa kulingana na migogoro ambayo inatokea sasa hivi katika ulimwengu wa leo na ardhi imekuwa ni mali, basi tungependa maeneo hayo yaainishwe vizuri na yapewe hatimiliki ili kuepusha migogoro inayoweza kuibuka hapo baadaye watu pengine kuanza kuingilia yale maeneo huo ni ushauri tunatoa.

Nashukuru sana kwamba wenzangu wameongea juu ya ada nafikiri haiwezi kuwa ada kubwa na kweli ni vyema kutoa ada kidogo ni kuenzi, sehemu nyingi ukienda unatoa chochote pale kama vile kuenzi mtu aliyezikwa pale au aliyewekwa pale. Kwa hiyo, ni sehemu mojawapo ya kuenzi na kuonyesha moyo. Ukitsemia iondolewe mimi sikuafiki sana na upande wa Upinzani walisema iondolewe lakini nadhani itakuwa kwa vijana, watu wazima kiasi fulani na wageni kiasi kikubwa zaidi. Nafikiri iendelee kuwepo tu nafikiri na wenyewe wenzetu tunakubaliana kwamba ndio utaratibu uliopo.

Mheshimiwa Spika, mimi nimeshachangia mara nyingi sana na nimeshauliza maswali mengi kuhusu namna gani tunavyoenzi hawa viongozi wetu hasa Waasisi wawili na historia huwa inajirudia ukiweka kumbukumbu unakuta historia inajirudia yenewe. Historia sio mambo yaliyopita. Historia ni mambo yaliyopita lakini yanayorudia rudia na wanahistoria wanasema *history repeats itself*, huwa inajirudia yenewe. Kwa hiyo, unapoweka kumbukumbu hizi inafika mahali fulani unaweza kupata kiongozi anayefanana na mwingine anasema na fulani alikuwa namna hii.

Lakini nilichokuwa nasema mambo muhimu kwamba lazima tuweke historia vizuri kwa matukio na matendo makuu ambao Mwalimu Nyerere ameyafanya na Mzee Karume ameyafanya. Yale matendo makuu yawekwe vizuri kwa mfulululizo na kwa usahihi. Hatuwezi kuweka kila kitu kwa sababu Mwalimu Nyerere amefanya mambo mengi makubwa, Mzee Karume amefanya mambo mengi makubwa, lakini yako mambo ya muhimu ambayo ni ya manufaa kwa sisi na Taifa lijalo.

Zipo aina nyingi za kumbukumbu kama maandiko mbalimbali, matendo makuu, matukio mbalimbali na hali kadhalika watu kuweka picha au mikanda, kwa sasa hivi *video za speech* au kuweka sanamu.

Mheshimiwa Spika, kinachonitisha mimi sanamu za viongozi hawa mimi naiona moja pale Zanzibar pale Bwawani ya Mheshimiwa Karume. Wale waliipatia sana sanamu nayo ni kumbukumbu moja nzuri sana. Wameipatia jinsi walivyoiveka na inaonekana Mzee Karume anaonekana. Lakini visanamu ambavyo wamejaribu huku Tanzania Bara kuviweka vyote havifai. Kule Mwanza kuna kingine kako pale *proportionality* yake pamekaa kidogo kichwa kidogo cha Mzee Nyerere, mimi nafikiri wala haifai. Ukienda kwa mbali kwa kweli unaona hii sio sanamu inayomwonyesha mwenyewe Nyerere alivyo. Lakini kuna nyininge ilikuwa Tanga nasikia wao wameiondoa ile sanamu wamefanya vizuri. Ni kama vile hatuna watu wanaoweza kutoa sanamu vizuri ya viongozi hawa.

Kwa hiyo, mimi naomba kama kutakuwa na kuweka sanamu pengine mbele ya Bunge sanamu ambayo Mheshimiwa Mzee wetu Mwalimu Julius Nyerere na Mheshimiwa Abeid Amani Karume, walikuwa wanachanganya udongo kuanganisha nchi hizi. Hiyo ingekuwa ni sanamu moja kubwa ikawekwa mahali pazuri na inaonyesha jinsi vitendo walivyovifanya katika kuleta Muungano.

Mwingine amekaa huku na mwengine amekaa huku baadaye kuna ngao yetu kama anavyoiona hiyo sasa walichanganya. Ile sanamu tungepata hata wataalamu kutoka sehemu fulani wakachonga ikawa kubwa wakichanganya ule udongo ikasimishwa kwenye Ofisi pengine pale mbele ya Ikulu au pengine hata Uwanja wa Kimataifa au hata Mnazimmoja hata kwenye Ofisi za Bunge hii inaonyesha jinsi walivyoleta Muungano na ndio maana tunawaenzi kwa jinsi tulivyofanya kazi njema. Lakini sanamu hizi zinazochongwa sasa hivi hazina utaalamu na walinijibu hapa kwamba watajitatidi kurekebisha.

Mheshimiwa Spika, vile vile mimi *I am not comfortable* hasa hii ya kwenye noti ya shilingi 1,000/=. Mimi nikiangalia mdomo na kadhalika naona kwa kweli ni kama sio sanamu ya Mzee.

Mheshimiwa Spika, zipo sanamu nyingi sana tumeziweka hapa na zingine mwenyewe alizipenda nafikiri tungeweza tukawatumia wataalamu vizuri zaidi. Lakini tunasema yote hayo yatatendeka nadhani vizuri ili mradi Serikali imeamua kuweka kumbukumbu hizo. Mambo mengine ambayo yangeweza kutumika katika kuwaenzi hawa watu ni kuwapa majina ya vitu ambavyo nafikiri ni vikubwa zaidi. Ukitoa Uwanja wa Mpira wa Nyerere sijui nini unasema sawa.

Mheshimiwa Spika, mimi nilishauliza mara mbili au tatu, kwa nini hamuwezi mka sema hii ni *Nyerere International Airport*. Kwani kuna ubaya gani kwa sababu kuna *Kenyatta International Airport*, kuna *Kennedy International Airport*, kwa nini? Kwa sababu hii sasa jina la Nyerere au *Karume International Airport* ile ya Zanzibar kwamba watu wanatangaziwa kila siku ndege zitatua pale na *daily* jina hilo litatajwa. Kila siku dunia nzima litatajwa. *Now we are taking off to Nyerere International Airport* au *Karume International Airport* na itatajwa kila siku kwa sababu kila siku watataja kama vile Kenyatta wanavyomtaja.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nilikuwa napendekeza kwa nini hatuwezi kufanya hilo, hatuwezi kusema ni *University* kwa mfano *Nyerere University* au *University of Nyerere* ile ya Dar es Salaam kwa sababu vyeti vitaandikwa ulimwengu nzima *Nyerere University*. Lakini tunatoa vitu vidogo vidogo tu viwanja, sijui kitu gani haya majina ni *very parochial* yako humu humu tu ni hapa lakini tunataka yatajwe na dunia nzima. Hili tulikuwa tumelisema kwamba hayo ni mojawapo nayo ya kuwaenzi wakatamkwa wakatajwa kila wakati na wakaweka kama lisanamu sio kwenye Mabunge yetu tu na kwenye Uwakilishi kule.

Mheshimiwa Spika, kitendo hiki ni kikubwa kama kitafanywa vizuri na wenzetu katika kile kituo, nadhani kutakuwa na kundi la watu, watatembelea waone wenzetu

wamefanya nini katika vituo vyao katika nchi zingine katika kuenzi wale Waasisi au watu ambao wametenda matendo makuu. Wasifanye kwa haraka lakini tunataka kituo kile yule mtu akienda aione Tanzania kwamba hii ni Tanzania ambayo ni ya Muungano na kwa kweli na viongozi wameenziwa na kumbukumbu tunaomba ziwekwe kwa usahihi sio za kupotosha.

Kwa hiyo, tunaomba kile kituo kama nilivyosema awali kuwekwe wataalam na wataalam hawa wawezeshwe, watembee na nina hakika wewe umekuwa Mwenyekiti wa hiyo *Commonwealth Parliamentary Association* kuwa ulikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji, umetembelea Kisiwa kimoja kinaitwa *The Isle of Man* ukiingia kwenye ile *museum* yao yaani wale watu wako *proud* na utakuta kila kitu wewe mwenyewe ndio utakachokientesha mle ndani kuona maajabu yaliyomo jinsi walivyohifadhi historia ya yule mtu. *Man* alikuwa ni muasisi wa Taifa lile.

Man of the Man sasa wanasema *the Island of Man*. Yule mtu ameanzisha ile Jamhuri ya kile Kisiwa. Lakini jinsi walivyoenzi ukiingia mle mwenyewe umeshafika kule ukiingia mlangoni wewe mwenyewe utaelekezwa kwa sababu kuna mitambo itakuambia unataka kuangalia nini. Unaanza *ku-operate* wewe mwenyewe hapo uliposimama gusa kitu fulani, unagusa unamwona yule, unaona *speech*. Kuwe na utaalamu wa kisasa wa kuhifadhi haya mambo katika kile kituo. Tusiweke vitu ambavyo inakuwa ni vichekesho.

Kuna wakati fulani tuliweka kumbukumbu ya Mzee wetu hapo barabarani wakachora picha ndogo sana pale kuelekea Morogoro kwa Mzee Edward Sokoine, tukapiga kelele hapa tunashukuru wameweka rangi sasa hivi lakini bado pale palitakiwa sanamu kubwa tu, sio picha ya kuchora. Kwa hiyo, tunataka kitu hicho *serious*, kuwepo na watu wengine tunapenda sana mambo haya wateuliwe *group/team* ifanye mambo ya msingi sio mambo ya kuchekesha ndani yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kunipa nafasi napenda nikushukuru ahsante sana.

MHE. ROSEMARY H. K. NYERERE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nilikuwa na mengi ya kueleza lakini najua kwamba muda ni mfupi itabidi na mimi nijaribu kuchangia kwa kifupi sana. Kwanza kabisa ningependa kwa niaba ya familia ya Mwalimu Julius Nyerere, kutoa shukrani zetu za dhati kwa Rais Benjamin Mkapa na Serikali yake kwa azma yake ya kuwaenzi Waasisi wetu. (*Makofî*)

Kama familia kimsingi hatuna pingamizi yoyote kuhusu hoja hii ya kuwaenzi Waasisi wa Taifa hili. Wanafamilia pamoja na Serikali tulikaa kwa muda mrefu sana tukiwa na mazungumzo kwa muda mrefu sana kuhusu Muswada huu. Wakati Muswada huu unaletwa mbele ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kulikuwa bado kuna vifungu vingi ambavyo vilikuwa vina utata. Kwa hiyo, Kamati ya Bunge ikapata fursa ya kusikiliza hoja za familia na baada ya kuzielewa Kamati ya Bunge, iliishauri Serikali na wanafamilia tukae pamoja ili tuweze kuweka mambo sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, kweli tulikaa pamoja vikao viwili, wanafamilia pamoja na wataalamu wa Serikali kutoka Ofisi ya Rais, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali, Ofisi ya Rais, Utumishi, Makumbusho na pia kutoka nadhani ofisi zingine sizikumbuki vizuri na hata pia kulikuwa kuna mtaalamu wa hatimiliki hapa Tanzania. Tulizungumza kwa kirefu na kuna mambo mengi yalisahihishwa na mengine tulipewa maelezo na tukaridhika.

Mheshimiwa Spika, baadaye tukarudi kwenye Kamati ya Bunge kulikuwa kuna masahihisho ambayo yalikuwa yameshatayarishwa, tukaletewa mbele ya Kamati ya Bunge na tukaambiwa kwamba mengine hayajawa tayari kwa sababu muda wa kuyatayarisha ulikuwa ni mfupi, hiyo tuliambiwa mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa sababu baada tu ya kikao cha wataalam na wanafamilia haikupita muda mrefu sana tukaingia kwenye Kikao cha Kamati ya Bunge. Kwa hiyo, sisi familia kwa kuamini hilo kwamba marekebisho yataletwa tukawaambia Kamati kwamba tumeridhika, Kamati ikafurahi, sisi tukafurahi na Kamati ikaridhia Muswada. Hiyo ilikuwa ni Jumapili.

Mheshimiwa Spika, Jumatatu nikaulizia yale marekebisho kwa Waziri na pia kwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali. Mheshimiwa Waziri alinibu kwamba tutapata hayo marekebisho na niliuliza kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali aliniambia kwamba tusiwarudishe nyuma. Nikamwambia lakini si tulikubaliana na uliahidi mbele ya Kamati kwamba kutakuwa kuna marekebisho. Akanijibu kwamba Kamati sio Serikali. Nilishangazwa na hayo majibu, inawezekana Mwanasheria Mkoo wa Serikali alikuwa na *pressure* ya kazi, lakini kidogo hayo majibu yalinishangaza. Sasa Serikali imebadilisha mawazo.

Mheshimiwa Spika, sisi tulikuwa tumekaa na wataalamu wa Serikali tukiamini kwamba tunaongea na Serikali. Lakini hapa tunaambiwa hapana. Tulivyokaa na wataalamu waliskiliza hoja zetu na wakakubaliana na sisi wakaelewa kabisa kwamba hizi hoja zinahitaji kurekebishiwa, lakini tunaambiwa kwamba Serikali imebadili mawazo. Sasa Serikali ni nani na tulikuwa tumekaa na nani. Hii inatupa shida kidogo.

Mheshimiwa Spika, sisi tunakubali ya kwamba Baba wa Taifa ni Baba wa Taifa wetu wote. Lakini warithi halali na mali yake binafsi ni familia tu. Sio Serikali, siyo *Mwalimu Nyerere Foundation* wala siyo *Nyerere Art Gallery*, ni familia tu.

Muswada huu kwa sehemu kubwa unazungumzia kumbukumbu za Mwalimu Nyerere zake binafsi, mali binafsi. Sisi tunasema kwamba uandishi wa Muswada huu sisemi nia, nasema uandishi wa Muswada huu tunadhani kwamba unaweza kutoa mwanya mkubwa wa kunyang'anywa mali kidogo ambazo mzee wetu alituachia. Akitokea mtu mwenye nia mbaya anaweza akautumia huu Muswada vibaya. Naomba nirudie tena ni uandishi wa Muswada huu ambaa unatutia wasiwasi. (*Makofii*)

Nitatoa mifano michache, tulipendekeza kwamba kwenye Muswada ionyeshe wazi kabisa, liwepo jedwali linaloonyesha kwamba maeneo ambayo familia inapendekeza yawekwe kwenye kumbukumbu, tusingependa kwamba maeneo yote yawekwe kwenye kumbukumbu na tusingependa kwamba Muswada usiwe wazi uwe *general* tu. Kwa hiyo, tukapeleka *list* ya muda mrefu sana kwamba tungependa maeneo haya ndiyo yawekwe kwenye kumbukumbu. Kwa sababu ukiacha maeneo yote ambayo yawe kumbukumbu kuna tatizo la matumizi. Kuna sheria ya matumizi ya hayo maeneo. (*Makofi*)

Hiyo tulikubaliana katika Kamati ambayo tuliongea na wataalam. Lakini tunaona kwamba imebadilisha mawazo, hatujaambiwa sababu ingawaje kule tulikubaliana. Sisi tunasema kwamba kwa nini Serikali ndiyo ituamulie maeneo gani ya kuhifadhi? Sisi tumeshaamua, kwa nini yenyewe ituamulie? Sisi familia ndiyo wenyewe hofu, Serikali haina nia mbaya ya kutunyang'anya. Sasa kama haina nia mbaya na sisi ndiyo tuna hofu na tunaamini kwamba hofu yetu itatoka kama jedwali lile likionekana kwenye Muswada Serikali inaona shida gani kuingiza lile jedwali ndani ya Muswada jambo ambalo watalaam walikubaliana nalo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuliomba kifungu cha 21 kirekebishwe, hicho kilikuwa kinaruhusu *center* baada ya Muswada kuitishwa, *center* kuchukua mali ya Muasisi ambayo alikuwa ameipa taasisi nyingine kwa ajili ya matumizi umma (*for public use*), sheria hii ikishapitishwa *center* itachukua ile mali. Naona sasa umerekebishwa, tumepitishiwa jana *amendments*, sawa, ila unasema sasa kwamba inaweza ikazinunua zile *property* ikaziingiza katika *center*.

Sasa hivi ningependa kusema hiki kitu kimoja, tumekuwa tukizungumza kwa muda mrefu sana na Serikali kuhusu suala moja la umiliki wa hotuba za Mwalimu Nyerere zilizopo *Mwalimu Nyerere Foundation*. Mwalimu Nyerere alizitenga akiaamini kwamba ni mali zake binafsi akazikabidhi *Mwalimu Nyerere Foundation*. Lakini Serikali imekuwa ikituambia kwamba maandishi yote ambayo Mwalimu aliyatoa ni ya Serikali, ila maandishi kama vile ameyatoa sehemu binafsi, labda kwenye harusi ya binti yake, hayo siyo ya Serikali. Lakini maandishi au labda vitabu vya Julius Ceasar na vitabu vya *Merchant of Venus* na kile cha Binadamu na Maendeleo. Tumetoa *arguments* za muda mrefu na tuliwaeleza pia Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala walituelewa. Lakini Serikali mpaka sasa hivi ina kigugumizi kutueleza kwamba wana msimamo gani kuhusu hotuba ya *Mwalimu Nyerere Foundation*, ni za nani? Sisi tunaamini ni za kwetu, tunaamini hivyo, tunaamini hatimiliki ni ya kwetu, ilitoka kwa mzee sasa inakuja kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba unilinde, wakati tuna mazungumzo na Serikali bwana mkubwa alitushauri sisi na Serikali tuweke *definition* ya *legacy* ili iweze kutenganisha, shughuli za Serikali na shughuli za familia. Lakini *legacy* ilivyotafsiriwa haionyeshi. Kwa hiyo, hakuna *clear cut demarcation* kwamba mali ya familia ni ipi na shughuli za Serikali ni zipi, tusije kuweza kuingiliana. Itabidi niende haraka haraka nilikuwa nadhani kwamba nitaongea kwa kifupi kumbe naongea kwa kirefu.

Kitu kingine ambacho nilikuwa nataka kusema nilitaka kusema kwamba haya, kuna matumizi ya jina, kuna *Trust Fund* itaanzishwa na huu Muswada. Tungependa sisi iitwe *Found of the Nation Trust Fund* kwa sababu tatu.

Moja lifanane na jina la *center* na kuonyesha wazi kwamba hiki ni chombo cha Kiserikali, pili, ni kwa sababu kuna taasisi zingine ambazo zina jina hilo na zinafanya kazi kama hiyo na hata sisi wenyewe tunataka kuanzisha taasisi kama hiyo, kitu ambacho Serikali inajua, tunataka kuanzisha *Julius Kambarage Nyerere Trust Fund* kitu ambacho tumewaeleza taasisi. Sasa kama kuna *Karume Memorial Fund* nadhani familia ya Karume inaanzisha. Halafu kuna hiyo, *Mwalimu Nyerere Foundation*, halafu kutakuwa kuna *Julius Kambarage Nyerere Trust Fund*, sasa tena inakuja sasa *Julius Kambarage Nyerere and Sheikh Abeid Amani Karume Trust Fund*, kutakuwa kuna mchanganyiko, tutachanganya watu. Kwa hiyo, tunafikiria kwamba iitwe *Found of the Nation Trust Fund* na pia najua kwamba *estate* ya Mwalimu haijatoa kibali ya matumizi ya jina hilo. (*Makofî*)

Naomba niendelee haraka haraka, nilitaka kusema kwamba sisi yakichukuliwa majengo yote, maandishi, hata na jina tutafanya nini sisi? Sisi sasa hivi kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere pia mapenzi yake kwa Watanzania yako *fresh*, watu ambao mmefanya nao kazi wapo, wanamjua na mambo yetu hayathaminiwi, nia zetu hazithaminiwi, je, huu Muswada ukipita mawazo yetu yatathaminiwa? (*Makofî*)

Sikusimama hapa kuusimamisha Muswada, sikusimama hapa kuuzuia Muswada, ningesubiri wakati wa vifungu, nimesimama hapa kuwaeleza ili mpaka kujua msije mkasema kwamba mbona hukusema?

Mimi kuna vikao ambavyo naingia, naingia *NEC* huu Muswada umepita, naingia kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naingia katika hili Bunge, msije mkanisuta siku moja mkasema kwamba mbona hukusema Rosemary? Mimi pia ndiyo mwakilishi, familia imenitura pamoja na Madaraka Nyerere, tuje kuongea na Serikali kuhusu huu Muswada, wasije wakanisuta wakaniambia kwamba mlikuwa mnafanya nini huko? (*Makofî*)

Mimi pia nina watoto wasije wakanisuta, mama wewe ndiyo umetuuza, pia ni mali yao. Ahsante sana. (*Makofî*)

SPIKA: Tumesikia.

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Mimi kama wenzangu nataka pia kushukuru Serikali na Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na watalaam, wameweza kukaa na Kamati wakafikiria suala la kuwaenzi Waasisi. Suala la kuwaenzi Waasisi hawa lilikuwa na maana nzuri sana na bado lina maana nzuri sana na tunalihitaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nataka pia kumshukuru msemaji aliyepita, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, ambaye naye ameweza kusimama kutoa mawazo yake kwa niaba ya familia kama alivyosema. Sasa mimi pia naona kuwa bado naye na familia yake wana

haki ya kuendelea kuzungumza, labda ushauri wangu wa kwanza baada ya kusikia sasa hivi nitoe na mimi pia maoni yangu. Labda ingebidi Wizara ikae na Kamati na familia na *Foundations* zote mbili waweze kuliongelea jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, labda niendelee kutoa yale mawazo ambayo nilikuwa nimeandaa kwa ajili ya Muswada huu. Kuanzisha *center* ni kitu muhimu na ni kizuri. Lakini kuhifadhi nyaraka na vifaa inatakiwa iwe kazi iliyo thabiti kweli kweli. Kazi hii tunahitaji watalaamu waliobobea katika kazi hii. Kama Mheshimiwa Eliachim Simpasa, alivyosema tusije tukatia aibu tukatengeneza vitu vya ajabu ajabu tu. Hawa ni Waasisi wawili ambao wametuletea heshima katika nchi yetu. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe kuwa nyaraka zao na hifadhi zao kama vifaa na kadhalika kwanza zinalindwa vizuri, kwa hiyo, usalama uwe wa hakika kabisa na pia kuwe na siri ya hali ya juu kabisa. Naamini tukapotafuta watalaamu wenye sifa na maadili mema wataweza kukamilisha kazi hii. Kazi hii inaepusha kuweka *center* ambayo itajengwa kinamna isiyofaa. Inatakiwa nyumba ya kuhifadhi vifaa vingine kama vile tunavyoona katika nchi nyingine za China, Uingereza na kadhalika. (*Makofii*)

Ukichukua mfano mdogo kama wa Bagamoyo, Bagamoyo ni eneo dogo sana linalohifadhi vifaa. Lakini kwa bahati mbaya vifaa vimeanza kuharibika, karatasi nyingi zimeanza kuharabika kutokana na kuwa mwanga ni mwingi sana. Kawaida nyumba za kuhifadhi vifaa hutakiwa ziwe ndani ya giza, mnatumia mwanga wa kutosha wa taa na wala siyo mwanga wa kutoka nje. Ni lazima watalaam wahakikishe nyaraka zinatunzwa bila kupotea, bila kuibwa na wala bila kuliwa na wadudu wa aina yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo pia nilijiuliza nyaraka na vifaa hivi tunavipata kutoka wapi? Je, tunavipata kutoka Butiama pale ambapo vimehifadhiwa, vikachukuliwa kupelekwa kwenye *center* au vikawekwa kule kukaanzishwa na *center* nyingine?

Nimejiuliza vile vile je, tunatoa kutoka Zanzibar nyaraka na vifaa vya Mheshimiwa Sheikh Abeid Amani Karume, je, vifaa hivi vingine tunaamini vitakuwa bado viro Ikulu kama katika ofisi ya Rais na hata kulikuwa na nyaraka za siri za wakati ule, enzi za Baba wa Taifa na pia enzi za Sheikh Abeid Amani Karume? Je, nyaraka hizi na vifaa vinatoka katika familia zote mbili? Sasa limeongezeka lingine, je, zitatoka kwa ruksa ya familia? Pia je, vifaa hivi vitatoka na wananchi kwa sababu kama unavyoja kuna wananchi pamoja na hata mimi napenda sana mambo ya kale, nimehifadhi vifaa vingine ambayo vinahusu maisha ya Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nataka pia kuendelea kuhusu nyaraka hizi, naishauri Serikali inapotafuta hasa nyaraka na vifaa ihakikishe kuwa ni nyaraka zilizo sahihi. Kuna mtu anaweza akaghushi na wote tunaelewa kuna hasara hizi, lakini kuna mtu anaweza akadanganya, akaleta akasema hii nilipewa na Baba wa Taifa ina miaka 50, ina miaka 40. Kwa hiyo, lazima kuwe na uangalifu sana katika eneo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nilikuwa nikiomba popote pale Serikali itakapoamua kuweka *center* yake basi ihakikishe katika *center* ile kuwa wananchi wanapata nafasi ya kufika katika eneo lile na ingelikuwa vizuri kama wananchi watafika

bila kulipishwa malipo yoyote. Lakini pia tunategemea kupata wageni wa kutoka nchi za nje ambao tunategemea wao watalipishwa ili kusudi tuweze kupata fedha za kuendeleza kuangalia *center* hiyo ambayo ni ya muhimu sana. Pale pale nilikuwa nikishawishi kuwa kwa wale wananchi walio mbali na hiyo *center* itakapokuwa ama itakuwa Dar es Salaam au Dodoma ama Butiama ama Zanzibar ama Arusha, wananchi wengi watakuwa na hamu na nia ya kufika pale na kuona masalio ya nyaraka na masalio ya vifaa vya Waasisi wao. Basi labda Serikali ijaribu kuchukua jukumu pia la kuweza kutayarisha vifaa kama *cassettes*, vitabu, filamu ili kuziendeleza katika Majimbo mbalimbali ili wananchi wengine wote kwa ujumla waweze kufaidika na kuelimishwa kuhusu historia zote za Waasisi wote wawili. (*Makofi*)

Jambo lingine nilikuwa nataka kulielewa vizuri ni kuhusu ununuzi wa nyaraka. Kwanza kabisa kama nilivyosema ununuza wa nyaraka na wenyewe udhibitishwe vizuri. Pia ufanywe kwa makini vya kutosha. Lakini nilikuwa nataka kuelewa je wale ambao tayari wana vifaa vya Baba wa Taifa na Sheikh Abeid Amani Karume ambao walikuwa wamepewa labda wakati mmoja na yeYe na ukakuta vifaa vyenyewe vinafanana na vya Waasisi hawa wawili, je, hawa wananchi ambao walifaidika na kupata heshima hiyo ya kupata vifaa kama hivyo wataelewekaje mbele ya macho ya Serikali? Serikali itahitaji wavipeleke huko au itawaachia wavihodhi kama kumbukumbu yao wenyewe? (*Makofi*)

Jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kuuliza ni kuwa je, wananchi wengine waliokuwa na mapenzi kabisa na Waasisi wao na wengine hawapendi kuachana na vile vifaa kwa ajili ya kumbukumbu na wanafikiria hata wao kuanzisha *their own private museum* ndogo ndogo tu, *museum* ni nyumba ya mtu unaweza ukachukua vyumba vyako viwili ukaweka zile nyaraka zako ili familia yako na majirani na watu wanawenza wakapita wakaviona, nilitaka kujua Serikali inafikiria kuweka sheria yoyote kuhusu jambo hili ili kusudi mambo yasije yakawa magumu mbele yakagongana na familia za hao watu waliobarikiwa kupata hivi vitu wakawa katika matatizo? Nilikuwa naomba tuliangalie kwa umuhimu sana hilo, iwe ni kitu cha kufanyiwa kazi kwa makini na kuchunguzwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo niliwahi kulichangia humu Bungeni miaka kama miwili, mitatu, iliyopita na niliuliza na mpaka leo Serikali haijanipa jibu, ni kuhusu nyumba iliyohifadhi mwili wa Baba wa Taifa pale Dar es salaam kabla ya kwenda kuzikwa. Ninasikitika sana kuwa Serikali ilikuwa haijanijibu na mpaka leo tuko mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, tunaomba tujue mabaki ya nyumba hiyo yako wapi? Unasema unataka kuhifadhi vifaa vya Baba wa Taifa, ile nyumba lazima iwepo. Hata kama vile vioo vimevunjika basi tuvipate vioo vilivyovunjika vikawekwe katika *center* ile kama vioo vilivyovunjika ambavyo mwili wa Baba wa Taifa ulikuwa umewekwa, hicho ni kitu muhimu sana hatuwezi kujua, sisi tuna imani mbalimbali, tuna dini mbalimbali, kuna wanaoamini kwenye mizimu, basi kama wapo mimi nasema mzimu wa Baba wa Taifa bado uko hata ndani ya vile vioo. Kwa maana hiyo basi tunaomba vile vioo na vyenyewe virudishwe vitafutwe vilipopotea vikahifadhiwe katika center itakayoanzishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa pia naomba kutoa ushauri tu kuwa tunaomba baadhi ya wanafamilia waingizwe katika bodi ili wawe hapo siku zote waweze kuchangia mawazo yao.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwengine nilikuwa naomba hivi endapo hizi nyumba za Waasisi wawili ni nyumba za familia zao, endapo kwa miaka ijayo ya mbele wana familia watahitaji au watataka kuuza zile nyumba, ushauri wangu ulikuwa wao wanafamilia tuwaombe wauze nyumba hizi kwa Serikali. Vile vile nashauri Serikali ikubali kununua hizo nyumba na kuhifadhi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nadhani nimegongewa kengele ya pili muda umekwisha naomba hayo yasikilizwe na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja muhimu katika maisha yetu na mimi nataka kusema kuanzia mwanzo ya kwamba naiunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

Kwanza nataka nitumie nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Rais wetu Benjamin William Mkapa, kwa mambo makubwa ambayo amefanya katika nchi hii siwezi kuyasema yote ni mengi lakini hili amefunga dimba. Amefunga dimba kwa sababu katika kipindi chake cha uhai wa uongozi wake ameona hawezu kuacha madaraka bila kuwa na utaratibu maalum wa kuwaenzi viongozi wetu na Waasisi wakubwa. Hii ni heshima kubwa kwa sababu ni yeye mwenyewe aliyetamka haya wakati wa mazishi ya Baba wa Taifa pale Butiama kwamba atahakikisha katika kipindi chake anatumia nafasi yake hiyo kuhakikisha kwamba anaenzi mahali pote wazee wetu walipokaa na makazi yao ili angalau iwe ni mahali pa kumbukumbu kwa historia, vizazi vinavyokuja. Heshima hii ametekeleza leo kwa kuleta Muswada huu kupitia Waziri wake Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na Katibu Mkuu ambao wamefanya kazi nzuri sana nawapongeza sana kwa kazi hiyo. (*Makofî*)

Napenda pia niungane na Waheshimiwa Wabunge, kwa wasiwasi ambao mmeuonyesha. Lakini wasiwasi huo ultokana na hali ya mazingira ambayo tulikuwa nayo wakati huo. Baada ya miaka mitano baada ya mzee wetu Baba wa Taifa kufariki na baada ya miaka 33 ya Sheikh Karume kufariki hatukuwa na mwongozo wowote wa jinsi ya kuwaenzi wazee wetu. Hiyo ndiyo maana kila mmoja alikuwa anatafuta utaratibu wake wa kuwaenzi.

Mheshimiwa Spika, haya yaliyozungumzwa na wenzangu yalitokana na mazingira ambayo yalikuwa kila mmoja anaangalia atamuenzi vipi kiongozi, wengine walihakikisha hata majina ya shule au mitaa yanatumika kwa majina ya viongozi wetu. Lakini kwa bahati mbaya, ni kweli baadhi ya mitaa iliyopewa majina ya viongozi wetu haifanani na viongozi wenyewe. Baadhi ya shule hazifanani na majina hayo. Unatoa hati baadhi ya baa mahali ambapo watu wanakwenda kuburudika unatoa jina la kiongozi na anaandikishwa rasmi. Mimi nadhani sasa wakati umefika tuenze kuyamaliza na kufikiria upya namna ya kuanza kujenga heshima kwa viongozi tuliokuwa nao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa leo nataka nizungumzie mambo makubwa matatu. La kwanza ni haya ambayo Mheshimiwa Rosemary Nyerere, ameyazungumza ni mambo mazito na ni vizuri Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane ya kwamba yaliyozungumzwa tutapenda Mheshimiwa Waziri atupe majibu ya kuridhisha. Tusingependa wakati sheria inatoa nafasi ya sheria itakapopita maamuzi yoyote hayafanyika bila kushirikisha familia za pande zote mbili.

Ukichukua sheria yenyewe kifungu cha 8 (2) kinasema wazi kwamba maamuzi yoyote, hatua yoyote itakayochukuliwa itabidi ishirikishe pande zinazohusika. Hii ndiyo maana inanipa faraja ya kwamba bado Muswada haujazuia familia ya Waasisi wetu wawili kuendelea kushirikiana na Serikali ili kupata muafaka katika maeneo yale ambayo yana wasiwasi, imetoa mwanya huo. Lakini pia inazidi kunipa nafasi nzuri ya kwamba bado kuna vifungu vingine ambavyo vinasema kuna maeneo ambayo itabidi yaangaliwe, kama ni kweli ni mali ya Serikali au ni mali ya familia itabidi wakae na kuliangalia kwa undani wake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nasema hiyo imenipa faraja kwa sababu hata mimi nilikuwa na wasiwasi, kwa sababu najua ukichukua mfano familia ya Baba wa Taifa ni maskini kwa ujumla, hawana kitu wale, mimi bahati nzuri nawafahamu wote. Ukiamua kuchukua mali zote hizi ndiyo umewaacha hohehahe, hawatakuwa na chochote na wataishi maisha ya ajabu.

Kwa mfano, tungependa siku moja Nyumba ya Butiama ya Baba wa Taifa iwe ni kumbukumbu ya vizazi vyetu kujua Baba wa Taifa alikuwa anaisha namna gani. Nyumba yake ilikuwa namna gani na watalii pamoja na wanafunzi wetu wangejua hata alipokuwa analala, kitanda chake kilikuwaje? Lakini katika mazingira ya sasa wakati familia na yenyewe inakaa humo ndani huwezi kufanya kitu kama hicho itakuwa ni bugudha. Watalii kila siku wanaingia chumba cha mama kwenda kuangalia mzee alikuwa anakaa wapi, alikuwa anapita kona ipi, kuingia huwezi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Uchina nyumba ya *Chairman Mao* ambayo sasa imekuwa ni kumbukumbu ya Kitaifa alikuwa anakaa binti yake mkubwa na wameamua kumjengea nyumba nyingine makusudi mazima kwa sababu ilianza kuwa ni bugudha watu wanakwenda kila siku pale kumtembelea, mpaka hata anakosa nafasi ya kupumua. Wakaamua kabisa kwamba wamjengee nyumba nyingine.

Mimi ningemwomba Mheshimiwa Waziri, alione hilo kwa sababu kumbukumbu hii ni muhimu katika historia, hatutaki familia ikawa ni sehemu ya kupata bugudha ya kila siku ya wageni kuwatemebeza ili kwenda kuona shughuli mbalimbali. (*Makofî*)

La pili kuhusiana na ada. Ada lazima tuwe waangalifu, tunatoa ada kwa sababu ipi. Sitajali kutoa ada au kuwaambia wananchi wachangie kidogo kwa kwenda kuangalia kumbukumbu zote za Baba wa Taifa au kumbukumbu za Sheikh Abeid Amani Karume. Lakini pia nitasita sana na sitakubali mtu atoe shilingi 1,000/= kwenda kuona mahali alipolala yaani tunataka kufanya kaburi la Baba wa Taifa ni la biashara, tunataka kumwona Baba wa Taifa, alipolala alipie hela. Hilo kwa kweli nadhani ni vizuri tukaliangalia.

Hilo lilitaka kujitokeza pia China. Uchina watu walipokuwa wanakwenda kumuona *Chairman Mao* walikuwa wanalipa kiingilio, lakini baada ya kukaa ikaonekana sasa mwili wa marehemu unaanza kuwa ni biashara wakafutilia mbali ya kwamba haya mengine ni jukumu la Serikali kutoa fedha za kuhudumia mahali penyewe, siyo watu watoe ili kwenda kumwangalia Mao Tse-Tung, ni vizuri tukaliangalia. Mahali pengine tusitoze ada yoyote tutakuwa tunafanya makosa. Mahali pengine kwa ajili ya huduma kuweza kuhudumia kumbukumbu za Mwalimu tunaweza kutoa ada, mimi sijali tunaweza kutoa kiingilio, lakini mahali ambapo Baba wa Taifa amelala si vizuri ukawaambia watoto wa shule muwe mnatoa shilingi 1,000/= au shilingi 500/= tutakuwa tunakwenda kinyume na Baba wa Taifa, angeweza kufufuka siku moja akasema mnaniuza, mnanifanya mimi ndiyo biashara, angechukia. Najua hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, linalofuata yako maeneo mengine ambayo ni vizuri tukayaangalia, mara nyingi tumekuwa tukiangalia hivi mali zipi zitakuwa ni za Serikali na zipi zitakuwa za familia? Tulisema ni vizuri unaposhirikisha familia utapata faida kubwa mbili, zipo baadhi ya mali ambazo unasema ukizitoa zitakuwa ni mali ambazo kwa kweli wakati mwingine si kwa faida ya Taifa, lakini wakati mwingine unawenza kuwa unasema unamdhililisha Marehemu mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, nasema hilo kwa sababu kuna watalaan wanawenza kutaka nguo mbalimbali alizokuwa anavaa kiongozi wetu tangu Uhuru na nyingine labda zitakuwa zimechanika. Lakini watalaan wanasema ni kumbukumbu. Sasa lazima tufkie mahali fulani tukatae na familia itakuwa na haki ya kukataa ya kwamba hii hatutoi kwa sababu tutakuwa hatujengi heshima lakini tunavuruga na kumpunguzia heshima kiongozi wetu. Ndiyo maana nikasema hili tusililettee utani kwa sababu linawenza kutuharibia nia na madhumuni ya Muswada wenyewe ambao uko hapa.

Sasa lipo swalí lingine ambalo linahusiana na mali. Sheria inasema wazi kabisa, kifungu cha 4(3) kwamba zipo Taasisi ambazo zitakuwa zimeandaliwa au zimekuwepo hata kabla ya sheria hii. Sheria hii ipo wazi kwamba itaendelea kuzitamka na kuzitamka huko ni pamoja na kuzikubali ziendelee. Wasiwasi wangu ni hii Taasisi ya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, Taasisi pekee ambayo Mwalimu Nyerere aliiacha ni hii *The Mwalimu Nyerere Foundation* na aliiacha kwa mkono wake mwenyewe na maagizo yake mwenyewe. Ni kati ya Taasisi ambazo lazima Serikali ione namna ya kuzipa kila aina ya msaada ili iweze kufanikiwa katika majukumu yaliyokuwa yameletewa. Sasa Taasisi hiyo inasuasua na sijui Serikali inasaidia kiasi gani. Nimeona wanababaika, wanaomba michango kwa wananchi, kila mahali, inakuwa ni kama haina mwenyewe. Hivi Serikali inafanya nini kuhusiana na Taasisi hii?

Sheria hii inasema nini kuhusiana na Taasisi ambayo Baba wa Taifa mwenyewe aliona ianze? Ziko Taasisi nyingi zitaanza na zipo nyingine zimekuwepo lakini nataka nipay maelezo, Mheshimiwa Waziri anisaidie njue Taasisi hii ambayo yeeye mwenyewe alianza na kutoa maagizo, hivi kwa nini tunataka tena tuanze kuinyang'anya baadhi ya

mali ambazo Baba wa Taifa mwenyewe alikuwa amewakabidhi? Hilo ningependa nieleweshwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ningependa kujua kwamba kila Wizara itashiriki vipi katika kuwaenzi viongozi hawa? Natoa mfano, kama unataka kumuenzi Baba wa Taifa pale Butiama, Wizara ya Maliasili na Utalii kazi mojawapo ni kuendeleza jitihada alizokuwa ameanzisha kama hifadhi ya misitu katika eneo lake. Alikuwa mpenda mazingira mzuri sana katika nchi yetu na mfano mzuri wa kuigwa na Tanzania na dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara inafanya nini kuendeleza jitihada katika eneo lake ili watalii na wananchi wanapokwenda kuangalia maeneo hayo waone kweli mazingira aliyokuwa ameanzisha Baba wa Taifa bado yanaendelea?

Mheshimiwa Spika, katika ujenzi, tunamsaidiaje Baba wa Taifa kumuenzi sehemu yake ili kuhakikisha hata kama watu wanapokwenda wakute barabara nzuri. Butiama bado barabara sio nzuri ya kuingia pale Butiama. Inakuwa ni kama unakwenda Kijiji gani huko! Lakini tunakwenda kwa Kiongozi wetu Mwanzilishi na Muasisi! Wizara ya Elimu na Utamaduni katika hali ya mazingira ya shule za pale inafanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningeomba kila Wizara sasa kutokana na sheria hii iweke mikakati wa jinsi ya kusaidia namna ya kuenzi viongozi wetu katika mahali pao ili angalau tusiiachie Taasisi hii peke yake ikaonekana kwamba imebaki ni ya mtu mmoja. Ningeomba kila mmoja ashiriki katika upande wake, tuna imani kabisa tutafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuunga mkono hoja hii na Mheshimiwa Waziri asaidie kurekebisha haya mambo ambayo yamejitokeza ili angalau pande zote za familia zote za Mama Maria Nyerere na Mama Fatma Karume, waridhike ya kwamba angalau Serikali imechukua mawazo na ushauri wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada wa Sheria ya Taratibu za Kuwaenzi Waasisi wetu wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na kuwaenzi viongozi Waasisi ila naomba upanuke uende mpaka Waasisi 17 wa *TANU* na Waasisi walioshiriki kikamilifu katika Mapinduzi ya Zanzibar kwani nao walishiriki wakiongozwa na hao viongozi wao yaani waliokuwa Wenyeviti wa *TANU* na *Afro Shiraz Party*.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, naomba nao waingie kwenye *list*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI

WA UMMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nyingine tena ya kuwasilisha hoja hii muhimu sana ambayo kila mmoja kutokana na michango iliyotolewa imeonyesha Bunge zima limekubali kwamba ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo yako, nitajitahidi sana kuyatoa maelezo haya kwa ujumla lakini nitajielekeza kuweza kutoa maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Rosemary Nyerere na vile vile kutolea maelezo mafupi Taasisi ya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuendesha Kikao hiki cha Bunge lako Tukufu kwa namna ambayo imeniwezesha kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Kuenzi na Kuhifadhi Kumbukumbu za Viongozi Waasisi wa Taifa letu.

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza kwa makini na kwa utulivu hasa ukizingatia unyeti wa Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukurani za pekee kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na hasa Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati hii kwa kuchambua Muswada huu na kutoa maoni yao ambayo yamesaidia kuboresha Muswada huu.

Aidha, napenda kukushukuru wewe, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kusema na wale wachache kwa maandishi. Waheshimiwa Wabunge waliochangia Muswada wa Kuenzi na Kutunza Kumbukumbu za Viongozi Waasisi wa mwaka 2004 ni kama wafuatao na naomba nianze kwa wale waliochangia kwa kauli.

Kwanza ni Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Janeth Kahama, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini. (*Makofî*)

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye aliwasilisha mawazo ya Kamati yetu ya Sheria, Katiba na Utawala, Mheshimiwa Grace Kiwelu ambaye aliwasilisha mawazo ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Khalid Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye hati yangu ya kuwasilisha Muswada huu ni kwamba lengo la Muswada ni kuweka misingi thabiti ya Kuenzi na Kuhifadhi Kumbukumbu za Viongozi Waasisi wa Taifa hili. Lengo hili linatokana na ukweli kwamba mchango wa Waasisi hawa ni wa kipekee na ambao hatuna budi kuuensi.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno ya Mheshimiwa Khalid Suru, Waasisi hawa walikuwa wakombozi wetu, walituondoa kwenye minyororo ya ukoloni na utumwa. Waasisi hawa sio rahisi kuwalinganisha na wengine, lakini vile vile tunakubali kwamba kuna viongozi na watu wengine Watanzania ambao vile vile kwa kweli wametoa mchango wao ambao ni vyema vile vile tukautambua, lakini Serikali itaangalia ni namna gani itafanya hivyo. Muswada utaiwezesha Serikali na vyombo vingine kufanya hili kwa utaratibu mzuri na ambao kizazi cha sasa na vijavyo vitaweza kufuatilia hekima, fikra na falsafa za Waasisi hawa na hivyo kuweza kuelewa msingi wa maisha yetu sisi Watanzania.

Aidha, Muswada huu utaweka utaratibu wa kuratibu, kuendesha, kusimamia na kushirikiana na wadau katika suala la kuenzi viongozi hawa na kuhifadhi vielelezo vya kumbukumbu zao. Serikali ina imani kwamba kwa kufanya hivyo itakuwa inatimiza jukumu kwa niaba ya Watanzania wote na kuendeleza na kutumia yale yote waliyotuandalia Waasisi wakati wa uhai wao.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata fursa ya kuusoma kwa kina Muswada huu na kuunga mkono hoja hii kuungana na Serikali katika suala zima la Kuenzi na Kuhifadhi Kumbukumbu za Viongozi Waasisi wa Taifa letu. Hii inatokana na ukweli kwamba sisi wote ni wawakilishi wa jamii ya Watanzania na tunatokana na juhudzi za Waasisi hawa wawili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa muda ambao tumekuwa tunaandaa Muswada huu na nina hakika ninyi wenyewe mmejionea, tumejjifunza kwamba kitu kizuri kinahitaji muda na kushirikisha wengi hasa wale wanaohusika ili kufikia muafaka. Nasema hivyo kwa sababu uandaaji wa Muswada huu ulianza mwaka 2000 na kama nilivyosema hapo awali, ulishirikisha wadau mbalimbali kutoka maeneo yote ya jamii ya Watanzania.

Pia, ningependa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuchukua muda watakapokuwa kwenye Majimbo yao kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa Muswada huu ili kuondoza dhana potofu ambayo inaweza kujengwa kutokana na kutokuelewa mantiki ya Muswada wenyewe kutoka kwa watu ambao hawakuusoma Muswada vizuri.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu hoja zilizojitokeza katika majadiliano ya Muswada huu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi yake, Katibu Mkuu wa Utumishi, Wakurugenzi, Kamati ya Wataalam, Makatibu wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala na wote waliohusika kwa namna moja au nyininge katika kufanikisha Muswada huu. Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati tena kwa familia ya Waasisi wetu ambao kwa kweli tumetumia muda wao na mimi naelewa *plaint* yao kwa sababu ni kweli wao ndio wadau wakuu wahusika. Kwa hiyo, kufanya kwetu kuenzi, kwao ni fahari lakini kwa vyovyyote vile vile kuna-*sacrifice* ambayo watatoa lakini *sacrifice* ambayo tutawasaidia kubeba.

Mheshimiwa Spika, naomba kuanza na hoja ya Kamati ya Bunge. Kamati ilitaka Kamati ambayo iko kwenye Muswada ifutwe katika Muswada na kazi zake zifanywe na

Bodi kwa sababu ni kazi chache. Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ndio ilitoa wazo hili. Bodi inasimamia, inabuni na kuhamasisha vyanzo vya mapato ya Mfuko na matumizi yake kama ilivyoainishwa chini ya kifungu Na.18 ambapo Kamati inatoa maamuzi kuhusu matumizi ya majina ya Waasisi kama ilivyoainishwa kwenye kifungu Na.16 na katika Kamati hii kutakuwa na Wawakilishi wa Waasisi na katika Bodi hii vile vile kutakuwa na Wawakilishi wa familia za Waasisi.

Kwa hiyo, kazi hizi mbili ni tofauti na ambazo haziwezi kufanywa na chombo kimoja. Muswada utenge kati ya vitu vya familia na vya Serikali. Lakini kabla sijafika huko, pengine ni vyema nikaelezea kuhusu ada ya kuingilia kwenye Kituo.

Mheshimiwa Spika, kanuni zitaweka ada ambazo hazitaumiza watumiaji na kwa baadhi ya makundi, taratibu zitaangaliwa namna ya kuweka viwango ambavyo havitamuumiza na kwa vyovypote vile havitakuwa vya biashara hata kidogo. Mchango utakaowekwa utakuwa ni sehemu ya Watanzania kumuenzi au kuwaenzi Waasisi wetu. Kuhusu kutofautisha mali za Serikali na za binafsi, sio nia ya sheria kutofautisha mali za Serikali na mali binafsi. Sheria inaweka utaratibu ambao utasaidia kutunza vitu vya watu binafsi na vya Serikali kama sehemu ya kuhifadhi kumbukumbu za kuenzi Waasisi wa Taifa letu.

Kwa hiyo, vitu binafsi vitaendelea kubaki kuwa vya binafsi. Sheria imetambua kuwepo kwa vitu binafsi na vya Serikali na imeweka utaratibu wa namna ya kuvitambua kwa vile vya watu binafsi sheria imeweka utaratibu wa jinsi ya kupata vitu ambavyo vina hadhi ya kihistoria na pia imeweka utaratibu wa namna ya kuvipata toka kwa watu binafsi aidha, kwa kuvinunua au kwa kuvinunza pale vilipo. Lakini nataka kurudia, hakuna kitakachochukuliwa bila ridhaa ya wahusika. (*Makof*)

Kwa upande wa familia, kama Waheshimiwa Wabunge walivyochangia, itakuwa ni fedheha kwa mfano kuona kwamba makazi ya Waasisi yanabaki bila kuangaliwa na bila kutunzwa. Hiyo itakuwa ni fedheha kwa familia, kwa Serikali na Watanzania kwa ujumla. Kwa hiyo, nia ya Muswada huu ni kuweza kuipa Serikali vile vile uwezo wa kufanya hivyo lakini bila kuingilia uhuru na pale ambapo wao watatuelekeza itakavyofaa kwa upande wao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madaraka ya kuharibu kumbukumbu kwamba yapate ridhaa ya mwenye kumbukumbu hiyo na sio Waziri kuwa na madaraka hayo, lengo la kipengele hiki sio kuharibu, kuvitelekeza au kuvitupa. Kama ingekuwa hivyo tungetumia neno la Kiingereza *to destroy*, lakini hapa hatujatumia *ku-destroy* bali *disposal* na kwa hiyo, tunachotaka kusema, kinachotakiwa hapa ni kubadili hadhi yake toka kwenye kuwa vitu vyenye thamani ya kuhifadhiwa kama kumbukumbu za kihistoria na kutokuwa na hadhi ya kuwa kumbukumbu zenye hadhi ya kihistoria. Kwa vyovypote vile, tutafanya hivyo kwa ridhaa ya wahusika na hasa ya familia ya Waasisi.

Kwa hiyo, hakuna atakayevitupa wala atakayeviharibu, isipokuwa kama vilikuwa kwenye hadhi ya kuhifadhiwa, sasa yule ambaye ni kitu chake anaweza kukichukua na kama akitaka tutashauriana namna ambavyo tutaeendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kuangalia uwezekano wa kuwaenzi Waasisi wengine, wazo hilo limepokelewa na litaangaliwa namna ya kulitekeleza ipasavyo. Hata hivyo ninavyoamini Waasisi hawa wawili, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, walikuwa wakifanya kazi na wengine. Hawakuwa wanafanya kazi wenyewe. Kwa vyovyyote vile katika kuwahusisha na wao kuwa Waasisi watakuwepo vile katika kumbukumbu lakini Serikali imelipokea wazo hili na italifanyia kazi na tutakuja kuleta matokeo ya kazi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano, kuchangia na kuunga mkono hoja muhimu katika historia ya Taifa letu. Pamoja na mchango mzuri na kuunga mkono hoja hii, sehemu ya mchango wao haionyeshi kuisaidia Serikali katika kutoa maamuzi ya msingi kuhusu kuwaenzi Waasisi wa Taifa hili. Wameunga tu mkono kwa kusema tunaunga mkono hoja, lakini yaliyokuwa yameandikwa kwenye mchango wao kwa kweli yalikuwa hayajatusaidia ila pengine kupotosha kwa sababu ya itikadi na hapa hatufanyi mambo kiitikadi, tunamuenzi Baba wa Taifa bila kujali itikadi zetu. (*Makofi*)

Maoni yangu haya yanajionyesha moja kwa moja kwenye maelezo ya awali yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani kabla ya kuunga mkono Muswada huu. Maoni haya yana nia ya kuhadaa wananchi ili kuonyesha kwamba kinachofanywa na Serikali kwa kuleta Muswada huu Bungeni sio jambo la msingi na la faida kwa wananchi. Pamoja na kwamba Mwalimu Nyerere alikuwa Muasisi wa CCM, pia alikuwa Baba wa Taifa letu na Taifa letu ni la CCM na wale wenye itikadi nyingine. Kwa hiyo, ni Baba yetu sisi wote na wapinzani waone wajibu na jukumu la kumuenzi, lakini sidhani maoni yaliyotolewa jana kama yalimuenzi Baba wa Taifa kama tulivyokuwa tunategemea. Kazi alizozifanya na ambazo tunazienzi kwenye Muswada huu zilikuwa ni za manufaa kwa Taifa zima bila kujali itikadi ya kisiasa. Muswada kama walivyosema, unakusudia kuchukua vitu na kumbukumbu za Waasisi bila kujali maslahi ya warithi.

Mheshimiwa Spika, kifungu Na.11(1) cha Muswada, kinaonyesha kwamba Serikali haina nia ya kuchukua mali ya Waasisi na kama ilivyoelezwa hapo juu, Muswada unaweka utaratibu wa namna ya kuhifadhi kwa maelewano na wenye kumbukumbu hizo za kihistoria na ambavyo vinastahili kuenziwa. Aidha, Muswada umetambua kuwepo kwa sheria ya hakimiliki na hatimiliki.

Mheshimiwa Spika, naweza nikaelewa hofu ya Mheshimiwa Rosemary Nyerere kwa sababu hofu inaweza ikamfanya mtu akaghafilika. Lakini ni kweli kabisa kwamba hakuna kitakachofanywa na Serikali bila ridhaa ya wanaohusika hassa familia ya Waasisi kutokana na kumbukumbu na vile vitu vinavyoshikika. Tumeelewana isipokuwa pale ambapo alitaka na alituletea siku mbili zilizopita orodha ya vitu ambavyo vingekuwa sehemu ya Muswada. Lakini tumesema kwamba ni vyema Serikali ikawa makini na familia ikawa makini katika kufikia ridhaa ya vitu gani ambavyo vienziwe na ambavyo havienziwi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mimi nina hakika na ninyi mtakubaliana kwamba linapokuja suala la shamba kwamba mfano ambalo linalimwa mazao ya chakula au hata ya biashara, lazima kunahitajika umakini. Lakini linapokuja suala la hifadhi kama la *forest* au msitu ambao Mwalimu alikuwa amehusika nao, hatutakuwa tunatoa hati zinazofanana katika haya mambo mawili. Ni kwa manufaa ya familia na kwa manufaa ya wananchi. Wananchi wa Tanzania wanaitezama Serikali yao na haitaruhusu Serikali kufanya jambo lolote linalofedhehesha familia au Waasisi wenyewe kwa sababu kwa namna nyingine ni kuwafedhehesha wananchi wanaotaka kumuenzi Baba.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla na hasa familia ya Waasisi wajue kwamba hakuna litakalofanyika na liko ndani ya sheria, ukisoma sehemu ya sheria Na.8 imeonyesha kabisa familia ilivyo na nafasi kubwa ndani ya Muswada huu. Kwa hiyo, sisi Waheshimiwa Wabunge tuungane kwa pamoja kuweza kumsemesha Mheshimiwa Rosemary Nyerere na wengine kuona kwamba kwa kweli ni hofu, lakini Serikali imezingatia rai ya familia kwamba lazima tuhusishe familia za Waasisi katika kuamua ni lipi la kuenziwa na hata kama wao wataona ni vyema lienziwe nyumbani, tutafanya hivyo kwa sababu Muswada nao umeliweka hilo badala ya kupeleka kwenye *Center*. (*Makofi*)

Sasa kulikuwa na suala ambalo Mheshimiwa Paul Kimiti, amelileta akasema kwamba kama ilivyofanyika China na sisi vile vile tuliliona kwamba pale China Makazi ya Mao Setung yamechukuliwa na Serikali na badala yake familia ikajengewa nyumba. Sasa hilo linawezekana lakini hatuwezi fukafanya hivyo bila ya kupata ridhaa ya familia. Ni pale wao watakopubali na watakapoona umuhimu, Serikali haitasita kufanya hivyo kwa sababu Serikali itafanya lolote linaloonekana kwa macho ya Watanzania na kwa macho ya familia ya Waasisi linamuenzi na linawaenzi Waasisi kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine lilishauri kwamba kama Serikali itaamua kuchukua nyumba za familia na za Waasisi, basi wajengewe nyumba nyingine kama itachukua hizo za zamani. Sasa kama nilivyoeleza, Serikali haikusudii kuchukua nyumba yoyote, bali inakusudia kuhifadhi nyumba ambazo zitaonekana kuwa na hadhi ya urithi wa kihistoria na pale tutakapokutana.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaopendekezwa unaeleza kuwa nyumba au vitu hivyo vitabaki chini ya miliki ya warithi wa Waasisi na iwapo kutakuwa na haja ya nyumba yoyote kuwekwa katika orodha ya hifadhi ya kihistoria, jambo hilo litafanyika kwa mashauriano na makubaliano kati ya warithi na Serikali na hili halina utata kwenye sheria. Hii sio mara ya kwanza kuwa na utaratibu huu. Kwa mfano, Sheria ya Mambo ya Kale inafanya hivyo na hapa hapajakuwa na madhara. Kwa mfano, *Saint Joseph Cathedral*, ni jumba ambalo linahifadhiwa lakini limebakia kuwa ni Kanisa Katoliki. *Saint Alban* kwa mfano, ni jumba la kihistoria lakini limebakia ni Kanisa la Kianglikana. Kwa hiyo, umiliki hauondolewi lakini pale ambapo inabidi, Serikali haitasita wala haitaona kwamba imepewa mzigo wa kuweza kuzimiliki nyumba hizo, lakini kwa ridhaa ya wahusika hasa familia ya Waasisi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilisema Serikali imekuwa na tabia ya kusema itahifadhi majumba ya Makumbusho lakini haifanyi hivyo. Kwa mfano, jumba lililokuwa linatumika kuhifadhi mwili wa Marehemu wakati wa msiba wa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere halionekani.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, Serikali ilijitahidi sana na kwa hadhi yake kuweza kumhifadhi na kumweka mahali ambapo alikuwa anastahili Baba wa Taifa. Lile jumba liliyyokuwa limetengenezwa lilikuwa ni kumuenzi na kwa hiyo Serikali hiyo hiyo haitakuwa ndio ya kuharibu ile nyumba ambayo tulimhifadhi Baba wa Taifa, Uwanja wa Taifa. Vifaa vya banda hilo bado vipo na vimehifadhiwa. Serikali ina nia ya kujenga upya kama kumuenzi Baba wa Taifa na sheria hii ndio imetoa utaratibu, kabla ya hapo tusingweza. Kwa hiyo, upande wa Upinzani usipende kuwahadaa wananchi kwa kuleta mambo ambayo itaonyesha Serikali yao haitendi haki kwa wananchi wa Tanzania. (*Makof*)

Lingine lilihusu utata katika utekelezaji wa sheria hii na Serikali ya Zanzibar kwa sababu nayo ilijitokeza kwa upande wa Upinzani.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wake hauna matatizo kwa sababu kwanza sheria hii inatambua sheria Na.10 ya mwaka 2002 ya kuwaenzi Viongozi wa Zanzibar na pia Serikali ya Muungano imeshakubaliana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar namna ya kutekeleza jambo hili. Hivyo hakuna utata hata kama Wapinzani wangetaka ionekane hivyo.

Mheshimiwa Spika, lingine lilisemwa kwamba kutakuwa na mgongano wa sheria katika Serikali mbili. Nawahakikishia kwamba hapatakuwa na tofauti za kisheria kati ya Serikali ya Zanzibar kwani kati ya sheria ile ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hii tutakayoipitisha leo zimeshafanyiwa ulinganishi. Sasa naomba nisemee kwa ufupi Taasisi ya Mwalimu Nyerere na kwamba Upinzani walisema kwamba itakuwa na uhakika gani wa kuendelea kumiliki nyaraka za Mwalimu Nyerere baada ya sheria hii kupita? Vile vile Mheshimiwa Paul Kimiti, naye alikuwa amelileta hilo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya kuwasilisha Muswada huu, sio nia ya Serikali kunyang'anya au kupora vitu au nyaraka kutoka kwa mtu au Taasisi yoyote inayomiliki vitu au nyaraka hizo. Muswada huu unatambua vyombo vingine ikiwemo Taasisi ya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, sheria inayopendekezwa katika Muswada huu, hususan kifungu cha tisa katika jedwali la marekebisho, unaheshimu umiliki wa vitu na nyaraka zinazomilikiwa na familia na vyombo vingine na inaweka utaratibu wa jinsi Serikali inavyoweza kuvipatia vitu au nyaraka hizo. Vile vile, Muswada umeonyesha kwamba Serikali itashirikiana na wale wote watakaomuenzi na kama namna nyingine ya kumuenzi Baba wa Taifa itasaidia pale inapobidi kusaidia na kwa kadri ya uwezo wake.

Sasa kuhusu Taasisi ya Mwalimu Nyerere, tulifikiria kwamba kutakuwa na watu ambao wangependa pengine kupitisha misaada yao kwenye Taasisi binafsi na wengine wangependa kupitisha misaada yao kupitia *Center* ya Serikali. Kwa hiyo, ili nchi au

Taifa letu liweze kunufaika, tumeona ni busara Taasisi ya Mwalimu Nyerere bado ibakie Taasisi binafsi ambayo inatambuliwa kama Taasisi nyingine ambazo zipo tayari na nyingine zitakapojitokeza na tulio gopa kwamba ni kweli Mwalimu ndio kazi yake ambayo aliiacha na ndio kazi ya mwisho aliyoifanya. Haitakuwa ni kumuenzi Baba wa Taifa kama Serikali haitaona hiyo.

Lakini nina hakika tutafanya vizuri hata ile *Center* ikibakia kama *Private Institution* au kama *Foundation* nyingine. Mheshimiwa Rosemary alisema kwamba Serikali kama itakuwa na jina linalofanana na *Foundation* ambayo wao wanataka kuanzisha kama Muswada unavyosema, hakuna litakalofanywa bila ridhaa na familia. Basi na hilo vile vile litakuwa moja ya masuala ambayo tutawasiliana na Mhehsimiwa Rosemary ambaye ni Mwakilishi wa familia katika kuona kwamba *Foundation* ya Serikali itapewa, haitaingilia uhuru wa *Foundation* ambayo imekwishaundwa ya kwao au inayotegemea kuundwa.

Mheshimiwa Spika, Wapinzani walisema CCM isitumie mwanya wa kuenzi Waasisi kwa madhumuni ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana kwamba Baba wa Taifa ni Baba wa Taifa na kwa hiyo ni wa Watanzania wote. Ni suala lisilopingika kwamba na yeze ni Muasisi wa CCM. Hii ni *fact* ambayo hatuwezi kuibadilisha na kwa hivyo CCM itamuenzi Baba na wana-CCM wataendelea kumuenzi na Serikali ya CCM itamuenzi ipasavyo na kama itailetea sifa, naona ni jambo la haki na wapinzani wasilionee wivu hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kuhusu sheria iwajumu ishe Waasisi wengine, hilo nimeshalitolea maelezo.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nia ya Muswada huu ni nzuri, tutaendelea kuongea na familia na wakati wa utekelezaji, ndio kutahitajika sasa ridhaa kutoka kwa familia ya Waasisi na Serikali haitaacha kufanya hivyo. (*Makofi*)

Tumejifunza mengi toka mwaka 2000 tulivyoanza kutayarisha Muswada huu na nimekiri kwamba pale ambapo tutaongea hakuna litakaloshindikana. Naomba kutoa hoja na ninawashukuru sana. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Taratibu za Kuwaenzi Waasisi wa Taifa wa Mwaka 2004
*(The Founders of The Nation
(Honouring Procedures) Bill, 2004)*

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 3

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 8

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 9

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 10
Kifungu cha 11

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 12

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 16

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 17

Kifungu cha 18

Kifungu cha 19

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 20

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunitambua. Nimesimama tu kuomba Kamati yako ifanye marekebisho ya *cross reference*, ikitumia *Schedule of Amendment* kama ilivyogaiwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *Clause (g)hiyo (g)* tunaenda kwenye *Clause 20* ilivyokuwa *re-numbered*. Mwisho pale kunasema *Sections 8 or 21* sasa tunapendekeza ile 21 kwa sababu tumeshaifuta na maudhui yake tunayoyataka tukayapeleka 9.

Sasa *cross reference* haitakuwa 21 lakini itakuwa 9. Halafu, kwenye mwisho wa sentensi hiyo, ukurasa unaofuata *does* ni Kiingereza tu, tunafuta neno *does* inakuwa *do not apply*. Nakushukuru sana Mwenyekiti.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 22

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 23

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 27
Kifungu cha 28

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko)

Kifungu cha 29

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye (k) napendekeza kwa sababu hizo hizo nilizotoa, tufute *cross reference* ya 21 na badala yake tuweke 9. Nakushukuru Mwenyekiti.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 30

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 31
Kifungu cha 32

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilitrudia)

Muswada wa Sheria ya Taratibu za Kuwaenzi Waasisi wa Taifa wa Mwaka 2004
The Founders of the Nation
(Honouring Procedures) Bill, 2004

(Kusomwa Mara ya Tatu)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima

imeupitia Muswada wa Sheria ya Kuenzi na Kutunza Kumbukumbu za Viongozi Waasisi wa Taifa na kuukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja kuwa Muswada wa Sheria ya Kuenzi na Kutunza Kumbukumbu za Viongozi Waasisi wa Taifa yaani *The Founders of the Nation (Honouring Procedures) Act, 2004* pamoja na marekebisho yake sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa*)

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2004 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, (No. 3), 2004

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria mbalimbali wa mwaka 2004 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, (No. 3), 2004* sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria mbalimbali zifuatazo:-

Sheria ya kwanza ni Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana ya mwaka 1974 yaani *The Government Loans, Grants and Grant's Act, 1974*. Sheria ya pili, ni Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya mwaka 1996, (*The Joint Finance Commission Act of 1996*).

Mheshimiwa Spika, sheria ya tatu, ni Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 (*The Forest Act, 2002*), Sheria ya nne, ni Sheria ya Alama za Kibiashara na Huduma ya mwaka 1986 yaani *The Trade and Service Marks Act, 1986*. Sheria ya tano, ni Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria za Nchi yaani *The Penal Code*. Sheria ya sita, ni sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano ya mwaka 2003 yaani *The Tanzania Communications Regulatory Act, 2003*, Sheria ya saba, ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafirishaji wa Majini na nchi kavu ya mwaka 2001 yaani *The Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, 2001* na Sheria ya nane, ni Sheria ya Chuo Kikuu cha Sokoine ya mwaka 1986 yaani *The Sokoine University of Agriculture Act, 1986*.

Sheria ya tisa ni Sheria ya Chuo cha Ushirika Moshi, Sura ya 560 ya Sheria za Nchi yaani *The Cooperative College Act, of 1964*, sheria ya kumi, ni Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma ya mwaka 1999 yaani *The Public Service Retirement Benefits Act*,

1999, Sheria ya 11 ni Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 yaani *The Public Service Act*, 2002 na mwisho ni Sheria ya Tume za Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka 2001 yaani *The Commission for Human Rights and Good Governance Act, 2001*.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya kwanza inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali. Itakumbukwa kwamba mnamo mwaka 2003 kupitia Sheria Na. 9 ya mwaka 2003. Sheria hii ilifanyiwa marekebisho ili kuweka utaratibu nzuri wa udhibiti wa madeni na pia kuhakikisha kuwa kunakuwepo na uwazi wa utendaji kazi wa Serikali katika suala zima la mikopo na misaada.

Kwa mujibu wa marekebisho hayo Waziri wa Fedha amepewa mamlaka ya kukopa na kupokea misaada kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Misaada hiyo, inaweza kuwa fedha au vifaa, pia Sheria imeanzisha Kamati ya Taifa ya kusimamia deni la Taifa yaani *The National Debt Management Committee* ambayo jukumu lake kuu ni kumshauri Waziri wa Fedha kuhusu ubora wa masharti ya mikopo au misaada inayotolewa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ulioainishwa katika Sheria kama ilivyorekeblishwa unamwajibisha Waziri wa Fedha kutoa taarifa za mikopo na misaada kwa watu na Taasisi nyingi ndani na nje ya nchi. Hautoi hifadhi kwa usalama wa Taifa letu. Taarifa ya mikopo na misaada inayotolewa hujumuishwa katika Taarifa ya deni la Taifa ambayo hutumiwa wadau mbalimbali pamoja na Taasisi za Fedha za Kimataifa. Taarifa hiyo huelezea madeni na mikopo, aina ya vifaa na mahali ilikotoka. Katika hali hii inakuwa rahisi kufuatilia aina ya misaada ambayo nchi imepata. Hivyo kuondoa usiri unaohitajika hasa kwa misaada iliyopokelewa na Serikali kwa matumizi ya vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. Kwa mantiki hiyo, Sheria hii inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 15 ili kuondoa sharti la kumtaka Waziri wa Fedha kutoa taarifa kwa misaada inayotolewa kwa vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya pili inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha yaani *The Joint Finance Commission Act* ya mwaka 1996. Maudhui ya Sheria hii kwa mujibu wa fungu la 15 pamoja na mambo mengine, ni kuweka uhalali wa vikao vya Tume ya Pamoja ya Fedha. Vikao vya Tume hiyo vinakuwa halali iwapo mahudhurio ya Wajumbe walio wengi yanawajumuisha Mwenyekiti wa Tume au Makamu wake iwapo Mwenyekiti hayupo. Hata hivyo, fungu hilo linatoa uhalali wa kikao cha Tume endapo haikidhi yaani quorum itatimia kuwepo kwa Wajumbe walio wengi tu bila kuzingatia uwakilishi wa pande zote mbili za Muungano.

Hivyo basi, kwa kuwa Tume hiyo, ni Taasisi ya Muungano ili kuondoa upungufu huu inapendekezwa kwamba iwapo Mwenyekiti na Makamu wake wote hawapo, akidi ya Kikao cha Tume itakuwa imetimia iwapo angalau Wajumbe wawili kutoka kila upande wa Muungano watakuwa wamehudhuria. Marekebisho haya yanatoa fursa ya Vikao vya Tume hiyo kufanyaika iwapo itabidi wakati Mwenyekiti au Makamu wake hawapo.

Mheshimiwa Spika, sheria tatu inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni sheria ya Misitu ya mwaka 2002. Sheria hii inafanyiwa marekebisho ili kuondoa mkanganyiko uliopo katika kugawa dhamana ya usimamizi wa misitu kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ambapo misitu iliyopo kwenye *general land* imeainishwa katika Fungu la 4(a)(iii) kuwa ni katika dhamana ya misitu ya Taifa na vile vile katika aya (b)(ii) ya fungu hilo la 4 kuwa ipo katika dhamana ya Serikali za Mitaa. Inapendekezwa kufuta kifungu cha 4(b)(ii) ili sasa misitu ya aina hii ibaki kama misitu ya Taifa chini ya usimamizi wa Serikali Kuu kama ilivyotarajiwa katika Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya 4 na 5 ambazo ni Sheria za Alama za Biashara na Huduma yaani *Trade and Service Marks Act No.12, 1986* na Kanuni ya adhabu zote zinafanyiwa marekebisho ili kuongeza adhabu kwa makosa ya alama za kibashara za bidhaa na huduma. Kumekuwepo na ongezeko kubwa la bidhaa haramu zinazoingizwa nchini au hata kutengenezwa hapa nchini kwa kutumia alama za biashara zinazoigiza yaani bandia zile zilizosajiliwa kwa ajili ya bidhaa halali zinazotengenezwa hapa nchini au kuingizwa nchini kihalali. Hali hii siyo tu inawakosesha mapato watengenezaji na waagizaji wa bidhaa halali, vile vile inaikosesha Serikali mapato yake halali.

Vile vile bidhaa hizo ni za ubora hafifu na za bei za chini hivyo kuleta ushindani usiyo wa haki na watengenezaji wa bidhaa halali hapa nchini. Inapendekezwa kuweka adhabu kali ya faini isiyopungua shilingi milioni 10 na isiyozidi milioni 50 au kifungo kisichopungua miaka minne na kisichozidi miaka 15 jela kwa makosa ya namna hii. Kwa ajili hii kifungu cha 59 cha Sheria ya *Trade and Service Marks Act* ya mwaka 1986 na kifungu cha 368 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu zinafanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya 6 inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni ya Mamlaka ya Udhhibit wa Mawasiliano Tanzania (*The Tanzania Communications Regulatory Authority Act, 2003*). Marekebisho yanayopendekezwa katika aya 2(1) ya Jedwali hilo la Sheria hii yana lengo la kuongeza idadi ya Wajumbe wa Bodi ya chombo hicho. Inapendekezwa kuongeza Wajumbe wengine wawili watakaotumikia Bodi ya Mamlaka hiyo kwa mtiririko uliyotajwa katika Jedwali hilo kwa kipindi cha miaka minne. Marekebisho haya yanalenga katika kuleta mlingano na masharti yaliyomo katika fungu la 7(b) la Sheria mama.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya 7 inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Mamlaka ya Udhhibit wa Usafirishaji wa Nchi Kavu na Majini ya mwaka 2001 yaani *The Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, 2001*. Sheria hii inafanyiwa marekebisho katika fungu la 13 kifungu kidogo cha 2 aya ndogo ya (e) na (f) ili kuondoa baadhi ya sifa za uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Udhhibit wa Usafirishaji wa Nchi Kavu na Majini yaani *SUMATRA*. Masharti yanayoondolewa ni yale yanayomtaka mhusika kukubali kuteuliwa katika nafasi hiyo kabla ya kuteuliwa na Bodi na ile inayotoa hiari kwa Mamlaka ya Bod kumteua mtu kama itaona anafaa kushika madaka hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hizi siyo sifa za watahiniwa wa nafasi hiyo bali ni hiari ya mteuliwa au mamlaka ya ziada ya Bodi ya *SUMATRA*. Hivyo inapendekezwa masharti haya yaondolewe.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linalopendekezwa kufanyiwa marekebisho katika Sheria hii ni aya ya kwanza, aya ndogo ya kwanza ya Jedwali la kwanza la Sheria hii. Marekebisho yanayopendekezwa yana lengo ya kuleta mlingano na maudhui yaliyomo katika kifungu cha 7 kifungu kidogo cha kwanza aya ya (b) ya Sheria mama, kinachotamka idadi ya Wajumbe wa Bodi amba siyo Wajumbe wa kudumu kuwa ni watano badala ya watatu. Vile vile aya ya pili aya ndogo ya kwanza ya jedwali hili inafanyiwa marekebisho kwa madhumuni hayo hayo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya nane inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ya mwaka 1984, inayopendekezwa Sheria hiyo ifanyiwe marekebisho katika fungu la 47. Inapendekezwa kufanya marekebisho kwa kufuta aya ya (c) ya kifungu kidogo cha 9 ili kuondoa maneno Chama Cha Mapinduzi katika tafsiri ya mashirika ya umma iliyotumiwa katika Sheria hiyo. Vile vile inapendekezwa kufuta kifungu kidogo cha 11 ili kuondoa sharti la kutaka amri ya Rais ya kuanzisha Chuo Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Sokoine au ya kutangaza Chuo au Taasisi yoyote ya elimu ya juu kuwa Chuo Kikuu kishiriki au Taasisi chini ya Chuo Kikuu cha Sokoine ambayo ni Sheria ndogo kupata ridhaa ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya 9 katika Muswada huu amba ni Sheria ya Chuo cha Ushirika Moshi ya mwaka 1964 inapendekezwa kufutwa. Sheria hii inapendekezwa kufutwa ili kuweka mazingira mazuri ya kuanzisha kwa Chuo Kishiriki cha Mafunzo ya Biashara na Ushirika chini ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Sokoine. Lengo la kuundwa kwa Chuo hiki ni kuongeza idadi ya watu wanaojiunga na Vyuo Vikuu katika kipindi hiki ambacho wako wahitimu wengi wanaoweza kujiunga na Vyuo Vikuu vyta elimu ya juu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya 10 inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni ya mafao ya watumishi wa umma Na. 2 ya mwaka 1999. Marekebisho yanayopendekezwa ni kwa ajili ya kuainisha vizuri zaidi, utaratibu wa kulipa mafao ya Majaji.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu litakumbuka kwamba Jaji Mkuu Mstaafu hulipwa mafao yake kwa mujibu wa fungu la 22 la Sheria hiyo na Majaji wa Rufani na Majaji wa Mahakama Kuu Wastaa fu hulipwa mafao yao kwa mujibu wa fungu la 20 la Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma. Mafungu hayo yanaelekeza kwamba watalipwa pensheni sawa na asilimia 80 ya mishahara anayopokea Jaji Mkuu aliye madarakani na Majaji waliopo madarakani.

Aidha, kifungu cha 5 cha fungu hilo la 20 kinaelekeza kwamba mafao ya Jaji yatalipwa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali na fungu la 21 fungu dogo la 3 linalelekeza hivyo hivyo kuhusu malipo ya mafao ya Jaji Mkuu Msataafu. Kimsingi kutokana na ukweli kwamba utumishi wa Majaji ni wa kudumu, pensheni yao ni ya kuchangia ambapo wao huchangia kama walivyo wanachama wengine wa Mfuko wa Pensheni ya Utumishi wa Umma, asilimia 5 ya mishahara yao na Serikali huchangia

asilimia 15. Kwa utaratibu huu wa kuchangia mfuko hupata jumla asilimia 20 ya mishahara ya Jaji Mkuu na Majaji. Michango hii huweza tu kulipia sehemu ya mafao yao. Sehemu ya ziada ya malipo ya mafao yao inapaswa kulipwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa katika mafungu ya 20 kifungu kidogo cha 5 na 21 kifungu kidogo cha 3 yanakusudia kueleza bayana wajibu wa Majaji na Serikali kuchangia mfuko wa pensheni.

Vile vile kutokana na marekebisho hayo Sheria itaeleza bayana kwamba tofauti ya pensheni itakayolipwa kwa mahesabu yatakayokokotolewa kwa kiwango cha asilimia 80 ya Pensheni ya Jaji Mkuu Mstaafu na Majaji wengine wastaa fu kwa upande mmoja na michango halisi iliyokusanywa na mfuko wa pensheni ya watumishi wa umma kwa upande mwingine italipwa kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Katika fungu la 22 ni ya kiuandishi ya kiufundi ambayo yanakusudia kuleta mtiririko wenye mantiki katika fungu hili na katika Sheria yenyewe kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya 11 inayofanyiwa marekebisho ni Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 yaani *The Public Service Act, 2002*. Kifungu cha 6 cha Sheria hii kinapendekezwa kufanyiwa tena marekebisho.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba mnamo mwaka 2002 wakati Muswada wa Sheria hii ukiwasilishwa Bungeni kiliongezwa kifungu kidogo cha 6 ili kuyapa mamlaka Mabaraza ya Madiwani kushughulikia masuala ya utumishi ya watumishi wa Serikali wa Mitaa.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta uwiano katika Mamlaka ya kuajiri, kuthibitisha kazini watumishi, kubadilisha vyeo na kuwachukulia hatua za kinidhamu, kwa watendaji wakuu, itakumbukwa kwamba mnamo mwaka 2003 Bunge lako Tukufu lilipitisha marekebisho katika Sheria hiyo na kukifuta kifungu hicho hivyo kuwapa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri, mamlaka hayo. Hali hii imeonekana kuziondolea Serikali za Mitaa jukumu na madaraka ya kushughulikia masuala ya watumishi wao katika Halmashauri zetu za Wilaya, Manispaa na Jiji na vile vile kuficha jitihada za uboreshaji wa Serikali za Mitaa kama inavyoendelea kama zoezi la uboreshaji wa Sekta hiyo inavyoendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hali hiyo, fungu la 6 limefanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu kidogo cha 6 ili kuyapata tena Mabaraza ya Madiwani Mamlaka ya kisheria ya kufanya maamuzi juu ya masuala ya utumishi badala ya kusimamiwa na watendaji wakuu wa Serikali hizo za Mitaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya 12 inayofanyiwa marekebisho ni Sheria ya Tume za Haki za Binadamu na Utawala Bora. Eneo linalofanyiwa marekebisho ni lile linalomtaka Waziri mwenye dhamana ya haki za binadamu kuwasilisha Bungeni Taarifa za mwaka kuhusu ukaguzi wa mahesabu, shughuli za Tume katika mwaka wa fedha uliopita na Taarifa zingine ambazo Waziri atazihitaji ili kujadiliwa na Bunge ndani ya miezi mitatu

baada ya kupokelewa na Waziri au katika Mkutano wa Bunge unaofuata baada ya Taarifa hiyo ya Tume kuwasilishwa kwa Waziri.

Kifungu cha 33 kifungu kidogo cha kwanza kinaliwajibisha Bunge lako Tukufu kutenga muda ndani ya muda maalum baada ya Waziri kupokea Taarifa ya mwaka kutoka Tume ya Haki za Binadamu. Hata hivyo, uzoefu unaonyesha kwamba ni vema Sheria iliachie Bunge lenyewe kujiwekea ratiba yake ya kushughulikia masuala yote yanayowasilishwa kwa Katibu wa Bunge kwa ajili ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufanya marekebisho katika kifungu cha 33 kifungu kidogo cha kwanza ili kuondoa sharti la kutaka Bunge lijadili Taarifa za Tume ya Haki za Binadamu ndani ya muda maalum na badala yake Sheria iliachie Bunge lenyewe uhuru wa kujiwekea ratiba ya kujadili Taarifa za Tume ya Haki za Binadamu zinazowalishwa Mezani na Waziri.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuchukua fursa hii kuishukuru kwa dhati sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala hasa Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa na Waheshimiwa Wabunge Wajumbe wote wa Kamati hiyo, kwa uchambuzi wao wa kina na ushauri nzuri walioutoa kuhusu maudhui ya Muswada huu na hivyo kuwezesha Muswada huu kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu sasa hivi. Nawashukuru sana wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda kukushukuru wewe na kupitia kwako niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa namwita Msemaji wa Kamati ili achambue Muswada huu atoe maoni ya Kamati.

MHE. RAMADHANI HASHIM KHALFAN (k.n.y. MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuwasilisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika kwa Mujibu wa Kanuni Na. (70) Kifungu kidogo cha (2) cha Kanuni za Bunge Toleo la 2004 naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala juu ya Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2004 (*The Written Laws Miscellaneous Amendment Bills 2004*).

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipata fursa ya kuujadili Muswada huu katika kikao chake kilichofanyika hapa Dodoma tarehe 08 Novemba, 2004. Aidha, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu azma yake ya kuzifanya marekebisho jumla ya sheria kumi na mbili. Kati ya hizo kumi ziko kwenye Muswada na mbili za nyongeza

zililetwa kwa maombi maalum na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye Kamati ambazo Kamati yangu ilikubali kuzijadili.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazohusika ni Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana na Sheria ya pili, ni Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya Mwaka 1996, Sheria ya tatu; ni Sheria ya Misitu ya mwaka 2002. sheria ya nne ni Sheria ya Utumiaji wa Alama za Biashara ya mwaka 1986, sheria ya tano ni Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 86, Sheria ya sita ni sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano na Utangazaji ya mwaka 2003, Sheria ya saba ni sheria ya Mamlaka ya *SUMATRA* ya mwaka 2001, sheria ya nane ni Sheria ya Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine ya mwaka 1984 na Sheria ya tisa ni Sheria ya Chuo cha Ushirika ya mwaka 1964. Sheria ya kumi ni Sheria ya Mafao kwa Watumishi wa Umma ya mwaka 1999 na sheria ya kumi na moja ni Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 na sheria ya kumi na mbili ya mwisho ni Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu ya mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imezitafakari kwa kina Sheria zote kimsingi na nakubaliana na mapendekezo yote yaliyotolewa na Serikali, isipokuwa Kamati inapenda kutoa ushauri katika maeneo machache ya sheria hizo kama ifuatavyo:-

Katika sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma ya mwaka 1999 Kamati yangu imebaini kuwa kifungu kipycha (20) kifungu kidogo cha (5) kilichofanyiwa marekebisho kikisomwa kwa pamoja na kifungu kidogo kipycha sita hususan matumizi ya neno *not with standing* hakileti mantiki ya pendekezo lililokusudiwa. Kwa sababu hiyo Kamati inashauri kuwa neno hilo liondolewe na kuwekwa neno lingine litakalo akisi lengo linalotarajiwaa.

Katika Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana ya mwaka 1974, Kamati yangu iliona kuwa sharti lililoelezwaa katika kifungu cha (15) kifungu kidogo cha (1) halionyeshi upana wa sheria uliokusudiwa na Waziri kutotoa taarifa ya mikopo misaada na dhamana inayokwenda kwa vyombo ya ulinzi na usalama.

Kutokana na upungufu huo, Kamati ilitaka kujua kama kifungu hicho kitasomwa peke yake. Hata hivyo Serikali iliifahamisha Kamati kuwa mantiki yake yatapatikana kwa kusoma na Sheria yote.

Katika Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya mwaka 1996, Kamati iliona kuwa hakukuwa na mantiki ya kukifuta kifungu cha (3) kinachowapa madaraka Wajumbe wa Tume kuchagua Mwenyekiti wa muda wa kikao endapo Mwenyekiti au Makamu watakuwa hawapo. Kamati iliona kuwa huu ndio uzoefu uliopo wa vyombo vingi vinapoendesha vikao hivi vishauri Serikali iangalie upya Kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Utumiaji wa Alama za Biashara ya mwaka 1986, Kamati inakubaliana na pendekezo la Serikali la kuongeza adhabu kwa Wahalifu kwa makosa ya utumiaji wa alama za kibiashara kinyume cha Sheria ambayo Kamati inaamini kuwa ni kuhujumu Uchumi wa Nchi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ikizingatiwa kuwa baadhi ya wahalifu hutajirika kwa kuuza bidhaa bandia na kuikosesha Serikali mapato, na ukizingatia kuwa wapo wahalifu ambao huuza hata dawa, vinywaji au hata vyakula bandia na kuhatarisha afya za Wananchi, Kamati inashauri kuwa kiwango cha adhabu kiongezwe walau ifikie kifungo cha miaka saba au faini inayofikia shilingi milioni 50 au vyote viwili kwa pamoja ili iwe fundisho kwa wale wote wanaojihusisha na biashara ya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, hizi ni Sheria ambazo Kamati yangu imetoa ushauri katika maeneo yaliyoelezwa. Aidha, kama nilivyosema awali, mapendekezo mengi ya Sheria zilizotajwa Kamati yangu inakubaliana nazo. Natumaini kuwa kama yapo maeneo ambayo nitakuwa nimeyaacha, Wajumbe wenzangu watazungumzia watakapokuwa wamepata nafasi ya kuchangia.

Mwisho napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalamu wake kwa kuwasilisha vema maelezo ya Serikali mbele ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Vile vile namshukuru Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kuwasilisha mapendekezo ya Sheria zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba nimalizie kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa michango yao ya kina iliyoboresha Muswada huu. Wajumbe hao naomba niwataje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Athuman Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Jeremia Mulyambatte, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Ramadhani Khalfan ninayewasilisha mbele ya Bunge maoni ya Kamati.

Vile vile naomba niwashukuru makatibu wetu Ndugu Ernest Zulu na Ndugu Charles Mloka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono Muswada huu na ninaomba kuwasilisha ahsante. (*Makofi*)

MHE. ADELASTELA E. MKILINDI (k.n.y MHE. DR. WILLBROD P. SLAA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA): Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa

nafasi kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43 (5) (b) (c) na 81 (1) Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, kama madhumuni ya Muswada huu yanavyosema kuhusiana na mabadiliko ya vifungu vya Sheria mbalimbali ili kurahisisha utekelezaji wake, Kambi ya Upinzani haina pingamizi lolote katika hili.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaiuliza Serikali kuwa siku zote hizi ilikuwa wapi kufanya marekebisho ambayo ni ya wazi katika baadhi sheria ambazo zilikuwa zinatoa mianya kwa Serikali kupoteza mapato halali kama vile Sheria Na. (4) inayofanyiwa Marekebisho ya *Trade na Service Marks Act* ya mwaka 1986 kuhusu kuingiza bidhaa bandia au za kughushi. Hapa Serikali imekuwa ikikosa mapato na inaendelea kukosa mapato hasa kwenye kazi za wasanii wa ndani na wa nje.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali marekebisho ya Sheria zote kama zilivyoainishwa ndani ya Muswada huu, Kambi ya Upinzani haina matatizo nazo. Ila tatizo ni kwamba Serikali inalala mno.

Mheshimiwa Spika, katika mambo kama haya Serikali isingoje matatizo yatokee ndipo Sheria zifanyiwe marekebisho. Hivyo inatakiwa isingoje uhalifu bali Sheria iwepo kwani kuna watu wanaoangalia udhaifu wa sheria kwanza na kufanya mambo yao wakiwa na uhakika Sheria inawaruhusu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Haijapata kutokea, nilikuwa na wachangiaji wawili walioomba kuchangia Muswada huu, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou na Mheshimiwa Mgana Msindai. Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou hayupo, asiyekuwepo na lake halipo. Sasa Mheshimiwa Mgana Msindai chukua nafasi yako, naye hayupo.

Mheshimiwa mtoha hoja hitimisha hoja yako. (*Makofi/Kicheko*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuhitimisha hoja yangu, hoja ya Serikali kuhusiana na marekebisho ya Muswada wa kufanya marekebisho katika Sheria mbalimbali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru wewe kwa kupokea hayo maombi ya Waheshimiwa Wabunge kuchangia lakini bahati mbaya hawapo.

Sasa nitajielekeza kwa kifupi sana kumshukuru sana Mheshimiwa Ramadhan Hashim Khalfan aliyesemea kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala, wametuunga mkono kwa maeneo yote isipokuwa alikuwa anasema kwenye hii Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma, anasema kifungu kidogo cha (5) na (6) kuna mkanganyiko.

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Kamati Muswada kama ulivyokuwa umechapishwa tuliliona na Serikali ilikiri pale na ndio maana tumekuja na *Schedule of Amendment* katika ukurasa wa tatu unaona mtiririko sasa tulivyouweka nadhani hapatakuwa na tatizo lolote katika kufikia hazima ya kuwalipa viongozi wetu hao mafao yao kwa mujibu wa Sheria. Kwa hiyo, naishukuru sana Kamati ilitusaidia sana katika ushauri na michango yake.

Kuhusiana na mchango wa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye eneo hili, Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, namshukuru kwa uelewa wake, Kambi ya Upinzani anayoisemea imeelewa. Lakini kwa hili la kucheleta na kwamba Serikali inalala usingizi, napenda niseme kwamba Serikali hailali usingizi na ndiyo maana tuko hapa. Nchi imetulia, mambo yanakwenda vizuri na umakini wa Serikali ndio huu. Pale ambapo Serikali inaona kuna kitu ambacho tunahitaji tukirekebishe ndiyo maana Serikali haisiti kuja hapa Bungeni na kuliomba Bunge lako Tukufu liweze kukubaliana na hoja ya Serikali na leo tumekuja hivyo kwa hazima hiyo hiyo na naamini watatuunga mkono kama walivyoutuunga mkono katika maeneo mengine ya Muswada huu.

Baada ya kusema hivyo nakushukuru sana, niwashukuru sana pia Waheshimiwa Wabunge kuitia kwako kwa uelewa wao walionyesha na nia ya Serikali ya kuleta Marekebisho haya mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja ni kwamba Muswada huu sasa usomwa mara ya pili.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria Ulisomwa Mara ya Pili*)

SPIKA: Hatua inayofuata Katibu, endelea.

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2004 (The Written laws (Miscellaneous Amendment Bill 2004)

MWENYEKITI: Bunge liko kwenye Kamati. Kazi ya Kamati inaanza. Katibu, endelea na taratibu za vifungu.

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Jedwali

(*Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

(*Bunge lilirudia*)

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria mbalimbali wa Mwaka 2004 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments Bill*), (No.3) 2004

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

SPIKA: Taarifa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali ya mwaka 2004 yaani *The written Laws Miscellaneous Amendment Bills No. (3)* ya mwaka 2004 pamoja na marekebishi yake kifungu kwa kifungu na kukubali. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hii sasa ikubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

SPIKA: Hoja ni kwamba Muswada huu sasa ukubaliwe na Bunge. Muswada umekubaliwa na Bunge na sasa utasomwa mara ya tatu. Katibu.

(*Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa mwaka 2004 ulisoma mara ya tatu na ulipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Baada ya kuingiza marekebishi yote yaliyofanywa na Kamati ya Bunge Zima Muswada sasa utapelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili upate kibali chake.

Naomba kutoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba kutakuwa na *Order Paper* ya nyongeza kwa kipindi cha mchana ili kusudi tukamilishe kazi ya kufikiria Maazimio mawili ambayo yalibaki wiki iliyopita na moja linahusu Ziwa Tanganyika na lingine linahusu Afrika Mashariki linaletwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje. Kwa hiyo, kipindi cha mchana bado tuna kazi ya kufanya ingawa *Order Paper* inaonyesha kwamba tumemaliza shughuli zilizopangwa kwa leo. Kutakuwa na *Order Paper* ya nyongeza kwa kipindi cha mchana.

Baada ya maelezo hayo kuna Mheshimiwa Kidawa Salehe, Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanaopambana na Ukimwi (*TAPAC*) anaomba Wajumbe wa

TAPAC wabaki hapa kwa muda mfupi mara baada ya kuhairisha Bunge kipindi cha asubuhi, anataka kuwatangazia taarifa muhimu wajumbe wa *TAPAC*. Baada ya hapo saa ya kusitisha shughuli za Bunge imekaribia kwa hiyo, tunasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni.

(Saa 06.48 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

HOJA ZA SERIKALI

MAAZIMIO

WIZARA WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tufuku lazimie Kuridhia Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika (*The Convention on the Sustainable Management of Lake Tanganyika*).

Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika unazihusisha nchi za Tanzani, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambi. Lengo la Mkataba ni kuziwesha nchi hizi kuhifadhi ziwa na bonde lake katika misingi ya uwiano na usimamizi wa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Kamati ya kudumu ya Bunge Mali Asili na Mazingira chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa wake Anne Semamba Makinda Mbunge wa Njombe Kusini. Kwa kuuchambua mkataba huu na kuukubali uletwe mbele ya Bunge lako Tukufu ili uridhiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba unatokana na mradi wa awali ambapo waandaji wa rasimu ya mkataba huo na mkakati wa Ziwa Tanganyika, zilikuwa mionganii mwa matokeo yake. Mkataba ulikamilishwa na kusainiwa na nchi zote kwenye kikao cha mawaziri wa Serikali za nchi zote nne tarehe 12 Juni, 2003 Jiji Dar es Salaam. Hadi Burundi imekwisha ridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Tanganyika ni moja ya maziwa yenyewe bionuwai ya pekee dunia. Zipo aina ya samaki zaidi ya 1300, jamii ya konokono na jongoo kwa kingereza invent bridges na mimea mbalimbali na aina 500 za viumbe hawa hazipatikani sehemu nyingine kokote duniani.

Aidha ziwa Tanganyika lina faida mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa wakazi wanaolizunguka kwa kuwapatia samaki, njia za usafiri kati ya vijiji na hata kati ya nchi na nchi na maji kwa matumizi mbalimbali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ziwa Tanganyika linakabiliwa na tatizo la uchafuzi wa mazingira kutokana na maji taka yanayomwaga na kuingia ziwani. Uharibifu wa

mazingira unaotokana na uingiaji wa tabaki ili neno jipya kiswahili, kingereza chake *sedment* na hizi tabaki zinaingia ziwani na uvuvi usio endelevu. Aidha bonde la ziwa hili linakabiliwa na uchomaji na ufyekaji wa misitu usio endelevu.

Mkataba huu unalenga kulinusuru ziwa Tanganyika kutokana na uharibifu wa ziwa lenyewe pamoja na mazingira yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu umezingatia maeneo muhimu yafuatayo:-

- (i) Kuimarisha ushirikiano katika kupanga na kusimamia shughuli mbalimbali katika ziwa na Bonde lake.
- (ii) Kuzuia na kupunguza athari mbaya katika ziwa na bonde lake.
- (iii) Kusimamaia shughuli za uvuvi.
- (iv) Kuzuia na kudhibiti uchafuzi wa mazingira.
- (v) Kuzuia uingiaji wa tabaki ziwani.
- (vi) Hifadhi ya bainuai na matumizi ya rasili mali za kijenetiki yaani *genetic resources*.
- (vii) Kusimamia matumizi ya ziwa kwa shughuli za usafiri.
- (viii) Kutekeleza mkakati wa uendezaji wa bonde la ziwa Tanganyika.
- (ix) Kufanya tathimini ya athari kwa mazingira.
- (x) Kutoa elimu kwa umma kukuza weledi na kushirikisha umma kufanya maamuzi. katika
- (xi) Kukabiliana na ajali na zarula.
- (xii) Kubadilishana habari na kutoa taarifa.
- (xiii) Kuanzishwa mamlaka *institution mechanisms* ya ziwa Tanganyika. Hili liko katika mkataba wenyewe na si kwamba mamlaka mpya itakayoazishwa. kuna
- (xiv) Majukumu ya wale wanaofanya shughuli zinazoweza kuhatarisha maeneo enderevu katika kulitumia ziwa Tanganyika.
- (xv) Wajibu na fidia yaani liability and conversations.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 40 na 41 za mkataba zimeweka utaratibu wa nchi kuridhia mkataba. Nchi inayoridhia mkataba inatakiwa kuwasilisha hati ya kuridhia kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na Mwenyekiti wa *commissioner* ya umoja wa Afrika. Mkataba unaanza kufanya kazi siku tisini baada ya nchi ya pili kuridhia.

Baadhi ya manufaa ya kuridhia Mkataba huu ni :-

- (i) Kuhifadhi mazingira ya ziwa Tanganyika.
 - (ii) Kupata ushirikiano wa kimataifa katika masuala ya hifadhi ya mazingira ya ziwa na bonde lake.
 - (iii) Kupata misaada na ushauri wa kitaalamu kutoka jumuiya ya kimataifa na hapa ningependa kutoa mifano hai, kwa upande wa Tanzania mradi wa usimamizi wa bonde la ziwa yaani *cashment management* huu unaaza kipindi cha Mwaka 2004 hadi Mwaka Machi, 2008 na shughuli zake ni kukuza weledi na kujenga uwezo wa wananchi vijiji. Kukuza mipango na matumizi bora ya ardhi na kuhifadhi itakayoshirikisha wananchi.
 - (iv) Kuondoa hii ni *reclamation* maeneo yaliyoharibiwa hususan na ujio wa wakimbizi.
- v. Kueneza teknologia bora ya matumizi ya majiko na matanuru yanayotumia kiasi kidogo cha nishati na vyanzo vya fedha kwa mfano mfuko wa mazingira duniani *global environmental fund* kwa kiingereza pana msaada wa dola za Marekani milioni 2.2 na kiasi hiki kimesha kubalika. Jumuiya ya Ulaya ni msaada pamoja na mkopo dola za kimarekani milioni mbili na nusu. Majadiliano bado yanaendelea.
Mradi wa pili ni mradi wa Usimamizi wa maji taka katika Halmashauri ya mji wa Kigoma Ujiji kwa kiingereza *West water management*. Mradi huu ni unaanza mwezi Machi, 2005 hadi mwezi Machi, 2008 na unalenga kukuza weledi wa wadau na kujenga uwezo wa taasisi zinazosimamia masuala ya maji taka.

Unaandaa mkakati wa wa usimamizi wa maji taka. Kuboresha na michoro husika yaani *system design* na kuweka utaratibu waufatiliaji wa usafi wa maji yanayoingia ziwani.

Vyanzo vya fedha mfuko wa mazingira dunia msaada dola za kimarekani 300,000/- kiasi hiki kimekubalika. *Nordic Development Fund* mkopo dola za marekani 4,500,000/-majadiliano yanaendelea na ujumbe wa *Nordic Development Fund* ulitembelea Kigoma Septemba, 2004.

Mradi wa tatu, Mradi wa maendeleo ya Ziwa Tanganyika *project to support the Lake Tanganyika integrated Region Development Program* eneo la uendelezaji wa uvuvi na hifadhi ya mazingira *Fishers Development and Environment Protection Component*

huu ni wa kipinid cha Machi, 2005 hadi Februari, 2010. Mradi huu una lengo wa la kukuza maendeleo endelevu na usimamizi wa uvuvi. Vijiji sitini vitafaidika na mradi huu.

Aidha mradi huo utaimarisha doria ya shughuli za uvuvi kwa kununa boti, genereta na vifaa nya mawasiliano. Utajenga na kuimarisha myalo na kununulia vifaa muhimu nya kuhifadhia samaki. Utahifadhi maeneo muhimu *sensitive cashment areas* yenye jumla ya hekta 50,000. Maeneo ya maji ya kunywa 125 na miradi midogo midogo ya wananchi jumla 50. Utagharamia ukarabati wa barabara za vijiji za kilomita 250 kwa kushirikisha wananchi.

Na utasidia uwazishwaji wa mfuko wa maendeleo ya uvuvi na vyanzo nya fedha katika mradi huu Benki ya Maendeleo ya Afrika ni mkopo wa dola za kimarekani milioni 7.4. Kiasi hiki kimeshakubaliwa na mkataba umesahiniwa na hazina mwezi Julai, 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pamoja yaani *regional component* shughuli za pamoja ni kuanzisha mamlaka ya usimamizi wa pamoja wa Ziwa Tanganyika kwa kuanzisha *secretariat*, Kamati ya Mawaziri na Kamati ya Makatibu wakuu na kujadili na kukubaliana Itifaki mbalimbali za mkataba na kuanzisha mfumo wa ufuatilaji wa hali ya mazingira ya ziwa ambayo ni kwa kiingereza *Lake monitoring and management system*. Vyanzo nya fedha kwa mradi huu Benki ya Maendeleo ya Afrika dola za marekani milioni 7.35 kiasi hiki kimeshakubaliwa, mfuko wa mazingira duniani msaada wa dola za marekani milioni tatu unusu haihusiani dola za marekani milioni moja kiasi kimeshakubaliwa na Finida msaada dola za marekani milioni mbili bado majadiliano yanaendelea. Shirika la Chakula na Kilimo Dunia msaada wa dola za marekani milioni moja majadiliano yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili nchi wanachama wa mkataba wa usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika, waweze kutumia fedha zilizoahidiwa au kupatikana toka kwa wahisani. Suala la kuridhia mkataba huo ni mmoja ya masharti yanayotolewa na ya idadi ya nchi mbili nimesha taja Burundi imekwisha ridhia zilizoridhia inatosha mkataba kuanza kufanya kazi kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge ambalo linasomeka kama ifuatavyo: -

Azimio la Bunge kuhusu kuridhia Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika (*The Convention on the Sustainable Management of Lake Tanganyika*)

KWA KUWA lengo la Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika ni kuiwezesha Tanzania kwa kushirikiana na nchi zinazozunguka Ziwa Tanganyika kuhakikisha kwamba panakuwepo na hifadhi na matumizi endelevu ya bionuwai ya ziwa katika misingi ya uwiano na usimamizi wa ushirikiano;

NA KWA KUWA Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika unazihusisha nchi za Tanzania, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia;

NA KWA KUWA Ziwa Tanganyika lina faida mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa wakazi wanaolizunguka kwa kuwapatia samaki, njia za usafiri kati ya vijiji na hata kati ya nchi na nchi, na maji kwa matumizi mbalimbali;

NA KWA KUWA Ziwa Tanganyika ni mojawapo ya maziwa yenye bioanuwai ya pekee duniani ikiwa ni pamoja na aina zaidi ya 1,300 za samaki, na aina mbalimbali za viumbwe wengine na kwamba karibu aina 500 za viumbwe hawa hawapatikani sehemu nyingine kokote duniani;

NA KWA KUWA Ziwa hilo linakabiliwa na tatizo la uchafuzi kutokana na majitaka yanyomwagwa kutoka maeneo yanayozunguka ziwa, uingiaji wa tabaki ziwani na uvuvi usio endelevu;

NA KWA KUWA matumizi endelevu ya ziwa yanategemea sana usimamizi bora wa nchi husika kwa mazingira ya ziwa pamoja na bonde lake;

NA KWA KUWA ipi haja ya utekelezaji wa Mkataba kuanza mapema ili kunusuru Ziwa Tanganyika kutokana na uwezekano wa uharibifu mkubwa wa raslimali ya ziwa hilo pamoja na mazingira ya bonde lake;

KWA HIYO BASI, kwa kutambua umuhimu wa kuridhia Mkataba huu na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Bunge hili tukufu katika m Kutano wake wa Kumi na Saba, sasa linaazimia Tanzania kuridhia Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika yaani: “*The Convention on the Sustainable Management of Lake Tanganyika*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADIN: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa kuamuliwa*)

MHE. JOB YUSTINO NDUGAI (k.n.y. MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI KAMATI YA MALI ASILI NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba shukrani kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika (*The convention on Sustainable Management of Lake Tanganyika*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti ya Kamati ya Mali Asili na Mazingira Mheshimiwa Anne Makinda naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni ya Kamati ya Mali Asili na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia

Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika uliowasilishwa mbele yako na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 63(3) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Bunge linapaswa kujadili na kuridhia mikataba yote ya kimataifa inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo kwa masharti inapaswa kuridhiwa.

Aidha kwa mujibu wa kanuni ya Bunge ya 88 toleo la Mwaka huu Kamati ya Bunge ya Mali Asili na Mazingira ilipata fursa ya kupitia Mkataba huu uliowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais ambaye anadhamana ya kushughulikia masuala ya mazingira Mheshimiwa Arcado Ntagazwa - Mbunge, kwenye Kamati ili kujadiliwana kupata maoni na ushauri wa kuliwezesha Bunge lako Tukufu kujadili na kuridhia Mkataba wa makubaliano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa juhudini zake mbalimbali zilizoleta manufaa makubwa kwa taifa letu katika kuleta Azimio hili mbele yetu. Aidha naishukuru pia Serikali kwa kuamua kuridhia Azimio la Mkataba huu ili kulinda mazingira ya hifadhi ya Ziwa Tanganyika. Maoni na ushauri wa Kamati;

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu inakubaliana na hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kuhusu mapandekezo ya Kuridhia Mkataba huu. Kwani kwa kufanya hivyo nchi yetu wananchi wake kwa jumla watanufaika vya kutosha na matokeo ya kutekeleza Mkataba wa Hifadhi ya mazingira ya Ziwa Tanganyika kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri hivi punde.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kamati inaishauri Serikali kuharakisha kuweka saini kama ipasavyo kwenye document husika baada ya Bunge lako tukufu kuridhia mkataba huu ili kuifanya nchi yetu kuwa ya pili kuuridhia mkataba baada ya nchi ya Burundi. Ili ni moja ya masharti muhimu ambalo linabidi litekelezwe kabla ya mkataba haujaaza kufanya kazi.

NA KWA KUWA Mkataba huu unazihusu kila nchi za Kidemokrasia ya Kongo na Zambia kama wadau wakuu wa Ziwa Tanganyika na bonde lake ni vema basi nchi zote hizi nne zikashauriana mapema kumamilisha hatua hii ya kusaini document kwa lengo la kuanza mapema kutekeleza matakwa ya mkataba wenyewe. Kwa kuzingatia hali hii nchi hizi zitaweza kwa pamoja kuhifadhi mazingira ya ziwa na bonde lake katika mazingira ya uwiano na usimamizi kwa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kuhifadhi ipasavyo mazingira ya eneo hili Ziwa Tanganyika lina faida nydingi zikiwemo za kiuchumi, na za kijamii kwa wakazi wanaolizunguka kwa kuwapatia wananchi protein itakanayo na samaki, huduma ya usafiri kati ya vijiji na hata nchi na nchi kati ya hizi nchi nne na huduma ya maji kwa ujumla.

Matatizo ya uchafuzi wa mazingira ndani na kandokando mwa Ziwa Victoria kutokana na maji taka yanayomwagwa ziwani na kuingia kwa tabaki ziwani yaani sediments uvuvi haramu na usio endelevu, uharamia inabidi yawekewe mikakati madhubuti ya kuyadhibiti kuititia mkataba huu. Ikiwa ni pamoja na kulinda doria ndani ya ziwa ni vyema nchi zote nne yaani Tanzania, Burundi, Kongo *DRC* na Zambia zisimame kidete katika kukomesha matatizo haya ili kulinda mali asili na bioanuwai zinazopatikana katika ziwa hili na bonde lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili kukuza weredi na kuushirikisha umma katika kufany maamuzi ya namna ya kuhifadhi mazingira ya Ziwa Tanganyika na bonde lake ni muhimu sana. Hata hivyo lazima nchi zote nne zinazohusika na ziwa hili ziwhamashe wananchi wake mapema kwa kuwapatia elimu sahihi ya jinsi ya kuendesha shughuli na kutunza mazingira yake ipasavyo. Hivyo basi nchi hizi kwa pamoja hazina budi kuandaa taratibu za kisheria ambazo zitatekeleza malengo yaliyokusudiwa ndani ya mkataba huu.

Aidha Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuandaa washa mbalimbali wa mkataba huu ambazo zilishirikisha wilaya na mikoa inapakana na Ziwa Tanganyika na Taasisi mbalimbali kupata maoni yao. Maana ni kwa kufanya hivyo tu ndio utekelezaji wa mkataba mzima utakuwa unakubalika kwa wananchi walio wengi kwa manufaa yao na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uzuri na umuhimu wa mkataba huu, Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha ili kuuwezesha utekelezaji wake kuto kukwama. Ikiwa ni kuufungua wigo wa ushirikiano wa kimataifa katika nyanja za uchumi na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninaomba niwashukuru viongozi na wataalam wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuandaa kwa makini Azimio la Mkataba huu na hivyo kuiwezesha kazi ya Kamati yetu kujadili na kuchambua kama ipasavyo kuwa rahisi zaidi. Vile vile nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Mali Asili na Mazingira kwa ushirikiano wao wa dhati pamoja na moyo wao wa kujituma katika kutekeleza majukumu mbalimbali likiwemo hili la kuchambua mkataba huu siku ya jumapili na hatimaye kuyaafiki mapendekezo yake yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni na ushauri huu sasa naliomba Bunge lako tukufu litajidili na kuhidhinisha Azimio hili za Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika (*The convention of Sustainable Management of Lake Tanganyika*). Ili Serikali ipate nguvu rasmi za kuanza kutekeleza mkataba huu kwa kumanufaa ya nchi na wananchi wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Mali Asili na Mazingira inaunga mkono Azimio hili na ninaomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. ALI SAID JUMA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA: Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Kuridhia Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya kambi ya upinzani naomba kuwasilisha maoni yake kwa mujibu wa kanuni za Bunge kifungu cha 43(5) BC na 81(1) toleo la Mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wote tunavyoolewa hufidhi wa mazingira na viumbe wote waishio katika Ziwa Tanganyika sio tu kwa wananchi waishio pembezoni mwa ziwa hilo tu bali ni kwa mataifa yote yazungukayo ziwa hilo katika kukuza uchumi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyotembelea katika maeneo mbalimbali ya jamii ziishizo pembezoni mwa bahari na ziwa shughuli zao za kila siku ndio chanzo kikubwa cha uchafuzi wa mazingira.

Kambi ya upinzani ina omba ufanuzi, je, jamii zinazoonekana kuwa chanzo kikubwa cha uchafunzi wa ziwa hilo. Kama vile ziwa kuwa sehemu ya kutupa taka laini na ngumu au uvuvi haramu zitahamishiwa au zitatengewa utaratibu gani ili ziendelee kuishi hapo na mazingira ya ziwa yaendelee kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kabisa chimbuko la mkataba huu ni kama yanavyosema maelezo ya Mheshimiwa Waziri, sasa kama inavyosema kuwa rasimu ya uandaaji mkataba huu ilikuwa ni mradi wa awali wa kuhifadhi

MBUNGE FULANI: Bioanuwai

MHE. ALI SAID JUMA: Bioanuwai na udhibiti wa uchafuzi wa Ziwa Tanganyika. Kambi ya upinzani inauliza katika uhai wa mradi huo ambao tunaamini hakuwa endelevu kwani kama ungelihusisha wananchi wanaozunguka ziwa hilo kwa kiwango fulani mpaka sasa ungelikuwepo. Je, Kamati hiyo ilitoa mapendekezo gani kuhusu kubadili tabia za jamii zinayozunguka ziwa hilo na matumizi endelevu juu ya ziwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na jiografia ya Kigoma na Rukwa ni moja ya mkoa inayopata mvua za uhakika kwa Mwaka. Kambi ya upinzani inashauri suala la *sediment* ni kitu kinachotoka na kwa kiasi kubwa na aina ya kilimo kinachotumika katika mikoa hiyo hivyo tunadhani tabia halisi ya hilo ni kwa Serikali kuongeza maofisa uhani katika mikoa hiyo. Ili kutoa mbinu bora za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

MHE. KANALI FTEH SAAD MGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kukushukuru kunipa nafasi ya mwanzo katika jioni hii kuchangia mada hii. Pili napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia na Mazingira kwa kutayarisha au kutuletea Bungeni Azimio hili. Nionavyo Azimio hili limekuja kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki mbili zilizopita nilipata bahati ya kutembelea mkoa wa Kigoma na katika mkoa wenye bahati ule moja kwa sababu kwanza naona mkoa mzuri na hauna njaa kabisa hakuna njaa. Ni mkoa ambao unapata mvua kwa wakati mzuri sana, ni mkoa ambao unarutuba halafu unabahati hata ya *Lake Tanganyika*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Lake Tanganyika* ni moja kubwa katika maziwa katika dunia. Ni ziwa la pili lililorefu lenye kina kirefu katika dunia hii. Ziwa la kwanza liko nchini Urusi la pili sisi katika Tanzania hii. (*Makofî*)

Ni ziwa ambalo kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika Muswada kwamba lina bahati ya samaki wa aina nyingi halafu lina bahati ya urefu katika kutembea mpaka katika nchi jirani kama nne, yaani *DRC*, Burundi, Rwanda na Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema nimpongeze Waziri kwa sababu uchumi mkubwa nategemea tutaupata katika ziwa lile na mara zote napopata nafasi ya kuchangia nazungumza jamani umefika wakati tuangaliea katika bahari zetu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahari sasa hivi zitatusaidia katika kuchangia sehemu kubwa ya pato la taifa tusikamate ardhi tu, ardhi ndio inasaidia lakini hebu tutazame upande wa pili. Yote hayo Mungu katupa kwamba tuyatumie lakini bado ndiko hatujashughulika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hasa nashukuru kwamba Waziri amesema tumepata msaada huo utakaosaidia kunyanya uchumi katika *Lake Tanganyika*. *Lake Tanganyika* kwa kweli inatumiwa sasa hivi na vyombo mbalimbali ambavyo nimeviona pale lakini kwa kweli vinakwenda kienyeji. Vinasafirishwa kienyeji kabisa hakuna hata alama moja inayosaidia ya usafiri ambayo inaweza ikasaidia kutia vile vyombo ndani na kutoa nje.

Mfano wenzangu walizungumza juzi hapa *Landmark hamna boyaz* hamna cha *Chanel boyaz* hata hiyo chart yenye we tunaita *nutekal chart* yaani *navigation chart*, hawana. Iliyoko iliundwa sijui vipi hata wakapata bahati kusafiri kienyeji wale watu.

Naamini msaada huu ambao sasa utaishughulikia *Lake Tanganyika* basi naamini tumepata kitega uchumi kweli kweli kitakacho nyanya uchumi wa taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkoaa ule unabahati ya upopo mwingu na mvua za mangurumo makubwa sana na mara nyingi kweli yanababisha vumbi hiyo tunaita *sediment* kuingia kwenye bahari au kuingia kwenye lake na baada ya *survey* itakayofanywa nategemea katika fedha zitakazopatikana pia *survey* itabidi ifanywe ili isaidie hayo niliyozungumza ya chart na mambo mengine *navigation aids*. Lakini pia panahitaji usalama wa ile bandari yenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli pale katika bandari ile iko kienyeji mno haina hali yoyote ya usalama, haina hata *rescue* boti zozote zinazoweza kuwasaidia wale watakaopatwa na maafa kule baharini. Kwa hivyo kuna haja msaada huu utumike kwa njia zote pamoja na kufikiria uchumi lakini pia tufikirie usalama wa wananchi, usalama wa maendeleo ya taifa letu.

Kwa hiyo, matumaini yangu Mheshimiwa Waziri, tutaanza kujikwamua katika uchumi kwa kulitumia pia Ziwa Tanganyika. Ziwa Tanganyika ni nzuri halafu kwa upande wa utalii kwa Hala kunako bahati nzuri sana kuna vivutio vingi sana vya kitalii. Naamini bandari hili likishatiwa katika maandalizi mazuri likiuzwa katika kutangazwa ulimwengu na hakika watalii na watu mbalimbali watakuja kuweka vitega vyao uchumi na watalii watatufulilia kwa ajili ya kutembelea kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba kuchangia machache hayo na ninategemea Mheshimiwa Waziri ataangalia kwa upande wake na ninaamini atasaidia katika kuendeleza maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo natamka rasmi kwamba ninaiunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi ili nitoe maelezo kwa Waheshimiwa waliochangia hoja hii kwa kusema na kwa maandishi.

Kwanza ningependa niwatambue Mheshimiwa Job Y. Ndugai kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Alli Said Juma msemaji Kambi ya Upinzani, pamoja na Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni na waliochangia kwa maandishi Mheshimiwa Semindu K. Pawa Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki na pia Mheshimiwa Stanley H. Kolimba Mbunge wa Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana kwa michango yao na niseme pendekezo kutoka Kamati ya Maliasili na Mazingira ya kwamba tutazame uwezekano wa bajeti iwe ya kutosha, ili shughuli zilizotamkwa kwenye Mkataba ziweze kufanyika ipasavyo kama ilivyotegemewa kwa manufaa ya Wananchi wanaolizunguka Ziwa Tanganyika na hasa tukianzia Wananchi wa nchi yetu ya Tanzania. Mimi nakubaliana na ushauri huo, lakini tulipokuwa tunafikiria kuwa na mkataba convention, tulikuwa tumejifunza kitu kutoka mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria. Kama kuna

mambo mazuri sana yanafanyika, lakini pamoja na uzuri wake na kwamba Wananchi wenyewe ndio wenyewe mradi ule wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria, ni vizuri kuwa na mkataba ambao unafanya shughuli wenyewe iwe endelevu, na hususani katika mkataba huu wa Ziwa Tanganyika. Kwa sababu tunashirikiana nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki Mheshimiwa Semindu K. Pawa. Nimesema ni vizuri katika Azimio ikasomeka hivyo. Kwa sababu kikatiba Serikali ya nchi yetu inayojulikana kama ni Serikali, lakini nchi wenyewe ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namshukuru sana kwa angalisho la kikatiba.

Kwa hiyo, ndivyo tunavyofanya tukiwa na mkataba unajihakikishia uendelevu wa suala unalolifanya. Kwa hiyo namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge Job Y. Ndugai, kwa niaba ya Kamati kutukumbusha hilo. Ila unapokuwa na mkataba unatafuta namna ya kutotegemea bajeti ya kawaida ingawa hutaki kusema usihuhsishwe katika suala hilo. Kwa hiyo, nashukuru kwa wazo hili, na kama alivyosema Mheshimiwa Job Y. Ndugai kwa niaba ya Kamati ni kweli tumeshirikiana vizuri sana na Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kweli sisi Ofisi ya Makamu wa Rais tunajihesabu tuna bahati kwa sababu Kamati hii sio tu tunashirikiana lakini kikatiba wanatushauri na wanatusimamia, na ni kazi yao kwa niaba ya Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Naibu Spika.

Kuhusu alichokisema Mheshimiwa msemani wa Kambi ya Upinzani kwamba leo tunazungumzia mkataba. Lakini ni matokeo ya mradi wa awali, tunasema inaelekeea mradi wa awali haukufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niseme mafanikio ya mradi wa awali ni mkataba huu tunaouzungumza na tuliofikisha mbele ya Bunge lako Tukufu, kama nilivyoeleza baada ya kujifunza kutoka mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria tukaona katika Ziwa Tanganyika tuwe na kitu cha kudumu. Kwa maana hiyo kwa kweli mradi ule mradi wa awali 1995 mpaka 2000 katika kuutekeleza ndio ilibainika tuwe na mkataba, ambao ni Sheria ya Kimataifa tutakapofanya shughuli za Hifadhi ya Mazingira tukilenga raslimali iliyopo Ziwani.

Kwa hiyo, ningependa nikubaliane niseme tu kwamba hili limezingatiwa ndio maana tumefika hapa kuwa na mkataba. Suala la tabaki kuingia Ziwani nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwanza Kijiografia sote tunafahamu Ziwa Tanganyika liko katika Bonde la Ufa. Kwa hiyo miinuko yake ni mikali na kama alivyosema Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni lile tunamshukuru Mwenyezi Mungu, tunapata mvua za kutosha na vilevile kuna upepo wa kutosha na hata radi ya kutosha.

Kwa hiyo, kwa Kijiografia tutaona upepo, mvua za kutosha na radi ya kuleta mitikisiko na hata wakati mwengine matetemeko ya ardhi, ni vitu vinavyochangia tabaki kuingia kule Ziwani. Sasa moja ya eneo ambalo mkataba huu unajielekeza ni suala la Hifadhi ya Mazingira kwa maana ya kuhamasisha Wananchi kupanda miti ili kuzuia kile wanachokiita kwa kiingereza *run off*. Mvua ikinyesha mnapishana na maji mengi lakini

huku yamesheheni mchanga na vitu vingine kwenda kuwa tabaki kule Ziwani, hili limezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni, kwa mchango wake, na kwanza nampongeza kusema amefika Kigoma, maana wapo wengi wanasikia Kigoma, lakini hawajafika isipokuwa uzoefu wangu Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa wale waliokuwa hawajafika Kigoma. Ni kwamba wana mawazo Kigoma iko viper? Lakini wanapofika Kigoma huwa wanatuambia na kukiri kwamba sisi hatukuwa na mawazo kwamba Kigoma ni mahali pazuri namna hii. Sasa tunawashukuru wale wanaofika Kigoma na kubadilisha mawazo waliokuwa nayo kabla ya kuffika Kigoma. Kigoma ni mahali pazuri sana na kama nilivyosema ni kweli Mkoa ule ardhi yake safi, hatujapata wala haijawahi kusikika kwamba Mkoa ule una njaa, na kwa kweli tunamshukuru Mwenyezi Mungu. Maana isingekuwa hivyo, ule umbali pengine ungetuathiri kwa mambo mengi. Lakini Kijiografia na ki-hali halisi Mkoa wetu kwa upande wa chakula kwa kweli unajitosheleza. (*Makofi*)

Ni kweli kabisa anatukumbusha Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni kwamba Ziwa Tanganyika ni la pili kwa kina Duniani la kwanza ni Baika kule Urusi. Ni kweli kama tulivyosema tuna aina nyingi ya samaki na Waheshimiwa Wabunge wengine wanatuuliza hivi umetoka Kigoma umetuletea Migebunga, hawa ni aina ya samaki wa aina ya pekee hawapatikani mahali pengine ni katika Ziwa Tanganyika tu.

Ningependa nikubaliane naye na Mheshimiwa Kanali Feteh katika suala hili tunapozungumzia ziwa Tanganyika, ziwa Victoria, bahari ya Hindi. Sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais mheshimiwa Naibu Spika tunapozungumzia juu ya Hifadhi ya Mazingira ya maeneo haya, tunacholenga ni raslimali iliyomo katika maeneo haya ya maji. Raslimali ambayo inachangia uchumi wa taifa letu na vile vile inachangia kipato cha mwanachi mmoja na kwa maana hiyo kuchangia kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tunapozungumzia juu ya Hifadhi ya Mazingira ya Pwani na Bahari, akilini mwetu Ofisi ya Makamu ya Rais tunazingatia Watanzania milioni 8. Wanaoishi kando ya Bahari na ambao shughuli zinategemea uvuvi katika maeneo ya Bahari. Kwa hiyo, napenda kumshukuru sana kutukumbushia kwamba tusione tunasema kuhifadhi mazingira tunalenga raslimali ile ambayo ina mchango mkubwa sana kwa uchumi wetu na inao mchango mkubwa katika kutuondolea umaskini.

Pia napenda kwa kugusia suala la utalii, kwamba Kigoma siku si nyingi zijazo ishala Mwenyenzi Mungu atasaidia tuwe na barabara nzuri ya lami ya kutuunganisha Mashariki, tuwe na kiwanja kikubwa cha ndege na tuwe na umeme wa uhakika utalii utashamiri.

Mheshimiwa Naibu Spika kwa upande wa utalii, kama unataka kuwaona sokwe mtu katika eneo la Afrika Mashariki yote ni lazima uende mkoani Kigoma. Kwa sababu ni katika Hifadhi ya Mahale, Kusini mwa Kigoma na Hifadhi ya Gombe, Kaskazini ya Kigoma, ndipo huku utakapokuta sokwe mtu basi, si kwingineko. Hili linatupa sifa ya kigoma kuwa kwa kingereza *tourism destination*.

Sasa kuhusu usalama mimi napenda nimkushukuru sana Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni kwamba ukiangalia hali ya Bandari ile, usalama kwa maana vifaa vya kusaidi usafiri Ziwan *navigational aids, navigational charts*. Anachokisema na kutuangalisha ni kwamba havipo hivi vitu, kwa hiyo mimi nilifarijika wakati Bunge Tukufu Mheshimiwa Naibu Spika lilipokuwa linajadili ule Muswada wa Bandari, kwamba Bandari ya Kigoma nayo itahusishwa katika Bandari hizo kulingana na Sheria mpya tuliyopitisha Muswada wake hapa jana, kwa maana hiyo suala la usalama litazingatiwa.

Mwisho labda niseme kwa Mheshimiwa Stanley H. Kolimba, mchango wake umekuja katika muda wa mwisho lakini nina hakika kwa mawazo lazima atakuwa anahusisha Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Nyasa. Kwa sababu najua ni Mheshimiwa Mbunge anatoka eneo hilo. Napenda nitoe taarifa tu Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba ni kweli tumewahi kusema katika utaratibu kama huu tuliofanya kwa Ziwa Tanganyika tutaelekea Ziwa Nyasa. Tumepata tatizo kwa sababu tulitaka mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Nyasa uwe kama hili Azimio linavyotaka kwamba nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi ya Burundi, nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na nchi ya Zambia mradi huu tuufanye kwa pamoja.

Kwa hiyo, tulipoweka azma yetu na tukasema tunataka tutekeleze Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Nyasa kwa kushirikiana na nchi ya Malawi na Msumbiji. Wahisan walifika mahali wakasema suala la Mazingira kwa mojawapo ya nchi hizi tatu, wameliondoa katika kipaumbele. Sasa kwa maana hiyo wakasema hawateendelea kuhisani mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Nyasa, hicho ndicho kimetukwamisha kwa muda ili tufkirie ni vipi tutapata uhisani wa kuhifadhi mazingira ya Ziwa Nyasa. Kwa hiyo, ni kweli itatuchukua muda, lakini si kwamba wazo hili Mheshimiwa Naibu Spika limeondoka kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwisho niseme napenda tena kurejea kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii ya Azimio la Kuridhia Mkataba wa Hifadhi Endelevu wa Ziwa Tanganyika, na tunaomba sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, wasichoke kutupa mchango wao wa mawazo na kikatiba watushauri na kutusimamia katika kuwatumikia Wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.
(*Makofii*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Kuridhia Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika liliridhiwa na Bunge)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2004 (*The Environmental Management Bill, 2004.*)

(Kusoma mara ya pili)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba unikubalie nikushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha katika Bunge hili Tukufu na mbele ya Waheshimiwa Wabunge hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*The environmental Management Act Bill, 2004*) kwa mujibu wa orodha ya mabadiliko ilioambatanishwa kwenye orodha ya shughuli sasa usomwe mara ya pili.

Awali ya yote namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Anne S. Makinda Mbunge wa Njombe Kusini. Pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ninaowasilisha Bungeni leo ni matokeo ya ushauri, usimamizi na ushirikiano wa hali ya juu kabisa kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira. Tunawashukuru na kuwapongeza kwa dhati.

Pia napenda kutambua na kusifia mchango mkubwa sana, wa wataalam mbalimbali ambao kwa namna moja au nyingine, wamechangia machakato uliotufikisha hatua ya kutoa hoja niliyoitamka hivi punde hapa Bungeni. Aidha napenda kutambua na kuwashukuru wadau mbalimbali walioshiriki kutoa mawazo na ushauri wakati wa kuandaa Muswada na baadaye kuchangi mawazo katika kuupitia Muswada wenyewe. Wote hao tunawashukuru, na kwa vile anayeshukuru maana yake ni kuwa ana kuwa anaombia tena, sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais tunaomba ushirikianao tuliuopata kutoka kwa wadau wote hao tukianzia na Kamati ya Maliasili na Mazingira uendelee na udumishwe.

Nimalize sehemu hii ndogo kwa kumshukuru na kumpongeza, ataniwia radhi kama natamka jina lake yabidi nifanye hivyo, Dr. Paramagamba Kabudi, Mhadhiri wa Sheria katika Kitivo cha Sheria, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. Dr. Paramagamba Kabudi, ndiye mshauri mwelekezaji (*Consultant*) kwa lugha ya kiingereza wa mradi kubainisha mfumo wa Kitaasisi na Kisheria katika jitihada za Taifa letu Kuhifadhi na kusimamia Mazingira kujihakikishia Maendeleo Endelevu.

Tunawashukuru Benki ya Dunia waliohisani mradi huu na kupitia kwa Dr. Paramagamba Kabudi, Tanzania tuna mahali pa kujidai kwa yakini kuwa nchi yetu tunao wataalam wazalendo wanaokidhi sifa zitakiwazo Kimataifa. Maana Dr. Paramagamba Kabudi si peke yake wapo zaidi kama yeche. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kurejea Ibara ya 27 na 28 Ibara ndogo ya 1 za katiba ya nchi yetu. Ninapenda kunukuu 27 Ibara ndogo ya 1: "Kila mtu ana wajibu wa kulinda Maliasili ya Jamhuri ya Muungano, mali ya mamlaka ya nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na Wananchi na pia kuiheshimu mali ya mtu mwingine. Watu wote watatakiwa na Sheria kutunza vizuri mali ya Mamlaka ya nchi na ya pamoja, kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu na kuendesha uchumi wa Taifa, kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya Taifa lao." Mwisho wa kunukuu Ibara ya 27.

Ibara ya 28 Ibara ndogo ya 1: "Kila raia ana wajibu wa kulinda kuhifadhi na kudumisha Uhuru, mamlaka ardhi na Umoja wa Taifa." Mwisho wa kunukuu Ibara ya 28 Ibara ndogo ya 1. Pia ningependa kunukuu kutoka chapisho liitwalo, *Human Rights and the Environment*. Hapa inasomeka hivi Mheshimiwa Naibu Spika: "*Moreover from todays, perspective it seems obvious that human rights and the environment are in inherent Interlinked, as the life and the personal integrity of each human being depends on protection the environment as the resource base for life.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha katika kitabu kiitwacho: "*In land we trust*".

*(Hapa Kitabu Husika Kilionyeshwa kwa Waheshimiwa
Wabunge Kama Kielelezo)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA: Kuna maandishi yasemayo hivi, nanukuu: "*The dangers to the environment which must be of great concern to the Government set-up have been thus summarized by Ogolla: First, irrational land use practices may result in soil erosion with adverse impact on soil fertility and water quality. Secondly the use of fertilizers and pesticides for improved agricultural production pose the danger of water pollution through chemical residue with possible debilitating impact on human health and plant and animal life. Thirdly, the process of industrialization leads to the generation of deleterious byproducts whose capacity for the environmental media degradation is immense the production of effluents without proper treatment and disposal mechanisms and their uncontrol emission of fumes and particulates by factories undermine human, plant and animal life and upset delicate ecosystems. The primary duty of regulation and policing, in respect of such activities, must lie with the state's authorities as defined in the public law, and must be conducted on the basis of detail laws and regulations founded on constitutional mandate.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya mwisho hapo juu inayohusu sheria kuwa na msingi wa kikatiba ukiacha ibara ya 27 na 28 inawiana sawia na ibara ya 8 ibara ndogo ya (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayosomeka na nanukuu: "(8) (1) (b) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii na kwa hiyo lengo kuu la serikali litakuwa ni ustawi wa wanachi. Tafrisi yangu ya kifungu hiki cha ibara ya Katiba ya nchi kwa lugha inayoeleweka kwa wingi ni neno "Maendeleo". Katika kitabu nilichokitaja "*by land we trust*" neno maendeleo au maendeleo kwa ujumla ufanuzi wake unasomeka kama

ifuatavyo; na nanukuu: “*Development which is at the very core of the environmental concern in the new nations, has been h defined:-*

- (i) *Firstly, Development is the process by which a country provides for its entire population all the basic needs of life such as good health and nutrition, education and shelter and provides everyone of its population with opportunities to contribute to that very process through employment as well as scientific and technological construction.*
- (ii) *Secondly, it is the process by which National Government authorities construct and maintain productive mechanisms and infrastructure which diversify and perpetuate the productive base of the country, such as agriculture and industries, so as to ensure that the society can overcome the pressures and necessities of the national and related economic system for the present and for all future times.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inayopendekezwa ina lengo la kutekeleza sera ya Taifa ya mazingira ya mwaka 1997 na pia matokeo ya kutungwa kwa sheria hii itakuwa ni pamoja na kufuta na kuhuisha sheria Na. (9) ya mwaka 1983, iliyoanzisha Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Muswada wa sheria ya mazingira unapendekeza kutungwa kwa sheria itayoweka mfumo wa sheria na kitaasisi kwa ajili ya usimamizi yakini na husishi wa mazingira.

Muswada umeuweka bayana na majukumu na wajibu wa kila sekta katika kila ngazi ya utendaji kuanzia ngazi ya taifa hadi ngazi ya kitongoji na itaonyesha majukumu ya wadau mbalimbali. Serikali za mitaa zitaendelea kuwa na majukumu ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kama yalivyoainishwa katika sheria ya Serikali za Mitaa mamlaka za Wilaya Na. (7) ya mwaka 1982 na sheria ya Serikali mitaa mamlaka ya miji Na. (8) ya mwaka 1982. Mambo muhimu yafuatayo yametamkwa katika muswada kwa lengo la kukidhi maelekezo yaliyomo katika sera ya Taifa ya Mazingira kama ifuatavyo:-

- (1) Kuteuliwa au *designate* kwa waratibu na washauri wa mazingira ngazi ya Serikali za Mitaa, Mikoa na Wizara.
- (2) Suala la tathimini ya athari kwa mazingira *environmental impact assessment* kwa kiingereza kuwa suala la kisheria.
- (3) Kuweka viwango vya usafi wa mazingira Kitaifa.
- (4) Kufanya elimu ya mazingira na ushirikishwaji umma katika masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kuwa ni suala la kisheria.
- (5) Kuainisha makosa mbalimbali ya uharifu na uchafuzi wa mazingira na adhabu zake. Aidha muswada unapendekeza kuweka masharti kuhusu:-
 - (1) Kuunda Kamati ya kitaifa ya Ushauri kwa masuala ya Mazingira yenyе wajumbe kutoka sekta mbalimbali muhimu kwa Hifadhi ya Mazingira na Maliasili pamoja na afya

ya binadamu. Kamati itakuwa ndicho chombo cha ushauri kwa Wizari kuhusu uratibu na masuala muhimu ya mazingira katika sekta mbalimbali.

(2) Kuunda Baraza la Rufaa la Mazingira *Environmental Appeals Tribunal* ambalo litasikiliza rufani zitokanazo na maamuzi ya Waziri anasimamia masuala ya mazingira, au chombo kingine chenye mamlaka juu ya masuala hayo kwa lengo la kupata maamuzi ya haraka. Mwenyekiti wa Baraza atakuwa mtu mwenye sifa za kuweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Baraza litakuwa na wajumbe wenyewe utaalamu katika sheria na management ya mazingira. Masuala mengine kama vile, mashauri kuhusu uchafuzi wa mazingira na uvunjaji wa mazingira yataendelea kufunguliwa katika mahakama za kawaida. Utaratibu huu ndio unaotumika katika nchi nyingi duniani na una lengo la kupunguza mlolongo wa kufungua mashauri dhidi ya maamuzi ya kiutendaji.

(3) Kuanzishwa kwa mfuko wa Taifa wa Mazingira ili kugharamia shughuli mbalimbali za wananchi zinazohusu uhamasishaji wa Hifadhi na usimamizi wa Mazingira. Viamo vya mfuko vitakuwa ni ruzuku kutoka serikalini, michango ya hiari, misaada na faini zitakazolipwa na watu watakaopatikana na hatia kwa makosa ya uchafuzi wa mazingira, na mfuko utasimamiwa na Bodi ya Wadhamini. Mwenyekiti wake atateuliwa na Mheshimiwa Rais na wajumbe watateuliwa kutoka ofisi ya makamu wa Rais (TAMISEMI), Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Taasisi za Kitaalum na Utafiti pamoja na Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Maudhui ya Muswada, kwa kuzingatia mambo yaliyoainishwa hapo juu mapendekezo yaliyoko kwenye muswada huu yamegawanyika katika sehemu kuu ishirini:-

Sehemu ya kwanza yenyeye kifungu cha 1 hadi 3 inapendekeza mambo ya awali ambayo ni jina la Sheria inayopendekezwa, tarehe ya kuanza kutumika na pia inatoa ufanuzi wa maneno na misemo muhimu itakayotumika katika Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya pili yenyeye kifungu cha 4 hadi cha 10 inapendekeza misingi itakayotumika katika usimamizi wa mazingira pamoja na wajibu wa kulinda mazingira. Sehemu hii pia inapendekeza masharti kuhusu haki ya kila Mwananchi kuishi katika mazingira safi, salama na yanayolinda afya. Haki ya kuishi katika mazingira safi, salama na yanayolinda afya inajumuisha haki ya kila mtu kutumia mazingira kwa ajili ya shughuli za burudani, starehe, elimu, afya, dini, utamaduni na uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 3 kifungu 11 hadi kifungu cha 41 inapendekeza mfumo wa kitaasisi na kiutawala katika utekelezaji wa Sheria ya Mazingira. Mfumo huo ni pamoja na uainishaji wa majukumu ya Waziri, Kamati ya Taifa ya ushauri kuhusu masuala ya Mazingira, Mkurugenzi wa Mazingira, Baraza la Taifa la usimamizi wa Mazingira, Wizara za Serikali, Taasisi mbalimbali, Secretariate za Mikoa na mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 4 yenyeye kifungu 42 hadi 46 inapendekeza utaharishaji na utekelezaji wa mipango inayozingatia masuala ya Mazingira ambayo itapaswa kuzingatia dharula ambazo zinaweza kutokea katika Mazingira. Sehemu ya tano yenyeye kifungu 47 hadi kifungu cha 80 inapendekeza usimamizi wa Mazingira kwa

kuweka masharti yanayojumuisha masuala mbalimbali, ikiwa ni pamoja na waanzishaji wa maeneo ya kipekee ya Mazingira yanayohitaji hifadhi nje ya maeneo mengine yenye Hifadhi ya Kitaifa. Sehemu hii pia ina vifungu vinavyoweka masharti juu ya mipango ya usimamizi wa mazingira kwa maeneo ya Hifadhi za Kitaifa, pamoja na ulinzi wake. Pia yapo masharti juu ya Hifadhi ya maeneo nyeti kimazingira, kingo za Mito, Bahari na fukwe zake. Maziwa na fukwe zake, ardhi yowevu Milima, mandhari na mbuga. Hifadhi ya bioanuwai, matumizi ya raslimali za kijenetiki, usimamizi na uingizaji nchini wa vinasaba vinavyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki na mazao yake. Hifadhi ya urithi wa utamaduni, Hifadhi ya usafi wa anga na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 6 yeye kifungu 81 - 103 inapendekeza masharti kuhusu tathmini ya athari kwa mazingira kwa kufuata viwango vinavyotambulika kimataifa ili kuwa sehemu muhimu katika mikataba ya kimataifa. Viwango hivyo vitakuwa ndiyo nyenzo muhimu ya utaratibu wa ukaguzi ambao hufanyika ili kufahamu kama programu, shughuli au mradi utakuwa na athari kubwa kwenvye mazingira na namna ya kuiepuka.

Sehemu ya 7 yeye vifungu 104 na 105 inapendekeza kuweka masharti ya nyenzo mpya ya kisheria juu ya tathmini ya athari kwa mazingira na kuweka masharti ambayo itahitaji miswada ya Sheria, Sera, mipango na programu mbalimbali za Serikali na Taasisi zake zifanyiwe tathmini ili maelezo ya kina yatolewe kwa lengo la kuwezesha kutambua endapo utekelezaji wake hautokuwa na athari kwa mazingira na matumizi endelevu ya maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 8 yeye kifungu 106 hadi 113 inapendekeza masharti ya hatua za kuchukuliwa ili kuzuia kuzuia uchafuzi wa mazingira na udhibiti wa uchafuzi huo pindi unapotokea. Pamoja na mambo mengine inazuia uchafuzi wa maji, utupaji wa vitu vyatirekwa na kina yatenye sumu, kemikali na umwagaji mafuta kama vile baharini pamoja na kuzuia shughuli ambazo ni hatari kwa mazingira.

Sehemu ya 9 ya kifungu 114 hadi 139 inapendekeza hatua zitakazochukuliwa katika suala la menejimenti na usimamizi wa taka sehemu hii inatenganisha kwa makusudi masharti yanayohusu usimamizi wa utupaji wa taka ngumu kuzuia utupaji hovyo wa takataka katika maeneo ya wazi majumbani, utupaji na usafirishaji maji taka, uzuiaji wa uchafuzi wa hewa na utupaji wa taka zenye sumu.

Muswada unapendekeza kuzipatia Serikali za Mitaa jukumu maalumu la kupunguza taka ngumu, maji taka, uchafuzi wa hewa na taka zenye sumu katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 10 yeye kifungu 140 hadi 150 inapendekeza masharti kuhusu utaratibu wa kutengeneza na kutangaza viwango vya ubora wa mazingira, sehemu hii inatambua umuhimu wa nafasi ya kamati ya kitaifa ya viwango vya ubora wa mazingira kama vilivyoainishwa na Shirika la Viwango Tanzania. Kamati hii ina wajibu wa kuangalia maendeleo kuitia na kukusanya mapendekezo ya kuweka viwango na kuviwasilisha kwa Waziri ili kuvitangaza kuwa viwango vya kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 11 yenyе kifungu 151 hadi 161 inapendekeza taratibu za utoaji amri ya kurudisha mazingira katika hali yake ya awali, amri hii kuhusu haki ya njia kupita na kungia katika eneo linahitaji hifadhi na vilevile amri ya kuhifadhi mazingira. Inaelekeza amri kurudisha mazingira katika hali yake ya awali ili mtu ambaye ameharibu mazingira awajibike kurudisha mazingira katika hali yake ya awali kwa kadri itakavyowezekana kama ilivyokuwa kabla ya kuharibiwa, amri kuhusu haki ya njia ya kupita na kungia katika eneo linalohitaji hifadhi itatolewa kuhusiana na ardhi inayohitaji kutuzwa ili kuhifadhi mazingira.

Madhumuni ya amri hii ni kusaidia utunzaji na uendelezaji wa mazingira kwa kuweka mkazo kuhusu matunzaji ya ardhi endapo upo ulazima wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 12 yenyе vifungu 162 hadi 171 inapendekeza utaratibu wa kushughulikia uchanganuzi na utunzaji wa kumbukumbu, yapo masharti kuhusu uteuzi wa maabara, wataalam watakao fanya uchanganuzi kwa ajili ya kuchukua sampuli ili kuhakikisha kuwa pamoja na mambo mengine viwango vya ubora wa mazingira vinafuatwa na kutiliwa nguvu.

Sehemu ya 13 yenyе kifungu 172 hadi 177 inatambua haki ya kila mwananchi kupata habari juu ya mazingira kwa mujibu wa sheria, sehemu hii pia inaotoa kwa Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira haki ya kupata taarifa na habari za mazingira kutoka kwa mtu yeoyote kwa kadri zitakavyowawezesha kutimiza wajibu na majukumu yaliyoainishwa katika sheria.

Utafiti wa mazingira, elimu ya mazingira na uelimishaji umma yameelezwaa katika sehemu hii, Mkurugenzi wa Mazingira atatayarisha na kutangaza kila baada ya miaka miwili taarifa ya hali ya mazingira ya nchi na ana wajibu wa kuwasilisha taarifa hiyo Bungeni bila shaka kupitia kwa Waziri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 14 yenyе kifungu 178 inaweka masharti kuhusu umuhimu wa utaratibu wa ushirikishwaji umma katika maamuzi juu ya masuala ya mazingira kama yalivyoelekezwa katika kanuni ya 10 ya azimio la *Rio de Janeiro*. Ushirikishwaji umma hauishii tu katika ushiriki kwenye masuala ya tathmini ya athari kwa mazingira bali pia katika nyanja na hatua nyingine za maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 15 yenyе kifungu 179 na 180 inaweka masharti kuhusu mikataba ya kimataifa inayohusu usimamizi na udhibiti wa mazingira, sehemu hii pia inazungumzia uandaaji wa mapendekezo ya kisheria juu ya utekelezaji wa mikataba hiyo, pia yapo masharti kuhusu kuanzisha mzungumzo na nchi jirani juu ya uanzishaji wa programu za pamoja za usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 16 yenyе kifungu 181 hadi 203 inapendekeza masharti ya kuheshimu na kufuata sheria ikiwa ni pamoja na amri ya utekelezaji, uteuzi wa wakaguzi unaweza kufanya kwa kutamka jina la mtu au la Taasisi pia yapo makosa mbalimbali ya uharibifu wa mazingira na adhabu zake. Sehemu

hii inatoa Mamlaka ya kutoa amri kwa mtu yeote ili kuzuia uharibifu wa mazingira na masuala yote ya dharura yanaweza kutokea ili kuweza kudhibiti hali ya ubora wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 17 yenyе kifungu 204 hadi 212 inapendekeza utaratibu wa mtu yeote kukata rufaa endapo mtu huyo hakuridhishwa na uamuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Baraza au Uamuzi wa Waziri juu suala lolote linalohusu mazingira chini ya sheria hii. Mtu ambaye hakuridhishwa na uamuzi wa Mkurugenzi Mkuu anaweza kukata rufaa kwa Waziri endapo mtu huyo hakuridhika na uamuzi wa Waziri anaweza kukata rufaa kwenye Baraza la Rufaa la Mazingira.

Sehemu ya 18 yenyе kifungu 213 hadi 216 inapendekeza kuanzishwa kwa mfuko wa dhamana wa kitaifa wa Mazingira, fedha kutoka mfuko huo zitatumika kutoa misaada midogomidogo kwa wananchi ambao wataanzisha miradi na programu za hifadhi ya mazingira. Mfuko wa dhamana ya mazingira utasimamiwa na Bodi ya Wadhamini.

Sehemu ya 19 ya Muswada yenyе kifungu 217 hadi 223 inapendekeza vyanzo vya mapato kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira uwezo wa Baraza kukopa au kutoa mikopo na uwezo wa Baraza kuwekeza, chanzo kikuu cha mapato ya Baraza kitakuwa fedha zitakazotengwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika sehemu ya 20 na ya mwisho yenyе kifungu 224 hadi 232 ina masharti kuhusu mambo ya jumla na ya kipindi cha mpito pia inapendekeza kufutwa kwa sheria namba 19 ya mwaka 83 ilioanzisha Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Pamoja na kufutwa kwa sheria hiyo ajira, amri na mambo yote halali yaliyofanywa na kuamriwa katika sheria inayofutwa yatabakia kama yalivyo hivi sasa.

Vilevile yapo masharti kuhusu malipo ya dhamana kama mwendelezaji au mwekezaji atashindwa kutekeleza masharti ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, sheria inayopendekezwa itatambua pia kuendelea kutumika kwa taratibu za sasa zilizowekwa katika sheria nyingine kuhusu ufunguzi na uendeshaji wa mashauri ya jinai au madai kwa kadri zinavyogusa mazingira.

Yapo pia masharti kuhusu ulipaji wa fidia kwa mtu atakayeathirika kutohana na jambo litokanalo na masuala ya mazingira, Vile vile yapo masharti kuhusu uwezo wa Waziri wa kutunga kanuni kuhusu ulipaji wa fidia inayohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwisho, ili kuweza kuhakikisha kuwa watu wengi wanasona na kuelewa maudhui ya sheria hii, Ofisi ya Makamu wa Rais itaweka utaratibu wa kuitafsiri sheria hii kwa lugha ya kiswahili ambayo inaeleweka na kutumiwa na wananchi wengi.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge waupitie Muswada ulio mbele yetu kwa lengo la kuuboresha na hivyo kuiwezesha Serikali kupata sheria ya kusimamia masuala ya mazingira. Hii ni kwa ajili ya kusimamia matumizi endelevu ya mazingira na maliasili za Taifa letu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana hoja imetolewa, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira Mheshimiwa Anne Makinda. (*Makofi*)

MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Maliasili na Mazingira kuhusu Muswada wa sheria ya usimamizi wa mazingira wa mwaka 2004, *The environmental Management Act 2004* naomba kutoa taarifa kuwa Kamati yangu imekutana mara nne kushughulikia Muswada huu katika kipindi cha mwezi wa Oktoba na Novemba 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendesha warsha ya siku mbili kwa kamati yangu huko Bagamoyo ili kuweza kuufahamu vizuri undani wa Muswada huu, halafu Kamati kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais iliwaalika wadau na wananchi kutoa mawazo yao ya namna ya kuboresha Muswada huu yaani Public Hearing tarehe 19 Oktoba, 2004.

Wadau kutoka Wizara mbalimbali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania , Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Taasisi na Mashirika ya Umma na yale ya Watu Binafsi Wawakilishi kadhaa wa Vikundi vya Jamii yaani *Civic Societies* ikiwa ni pamoja na Waandishi wa Habari wa Magazeti, Redio, na Televisheni walishiriki kikamilifu. Baadaye ndipo Kamati ilianza kuuchambua Muswada huu ikiwa Dar es Salaam tarehe 21 Oktoba, 2004 na kumalizia uchambuzi wake tarehe 7 Novemba, 2004 hapa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika mlolongo wa mikutano yote hiyo unaonyesha jinsi gani Kamati na Ofisi ya Makamu wa Rais tulivyotilia umuhimu wa pekee katika kuutafakari na kuujadili na hatimaye kuuchambua Muswada huu.

Muswada huu ni muhimu sana na unagusa kabisa sekta zote za kijamii na kiuchumi nchini na wananchi wote kwa ujumla kama ilivyoelezwa hivi punde katika sehemu zote 20 za Muswada na Waziri wa Nchi anayeshughulikia masuala ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Mikutano hiyo yote, Wajumbe wa Kamati yangu wamejifunza mambo mengi na kuelimika vya kutosha kuhusu namna usimamizi wa masuala mbalimbali ya hifadhi ya mazingira utakavyokuwa pindi Muswada huu utakapopita na kuwekewa kanuni za utekelezaji. (*Makofi*)

Licha ya mikutano hiyo Ofisi ya Makamu wa Rais imeiwezesha kamati kutembelea mikoa mingi nchini ikiwa ni pamoja na Zanzibar ili kujionea hali halisi ya

uharibifu wa mazingira katika maeneo mbalimbali na hivi karibuni Ofisi ya Makamu wa Rais imewezesha kamati kutembelea miji kadhaa nchini Tanzania, Kenya na Uganda iliyo kando kando mwa Ziwa Victoria kwa lengo la kujifunza na kuona jinsi gani Serikali za nchi zote tatu za Afrika Mashariki zinavyojitahidi katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kutunza mazingira ya Ziwa hilo linalohudumia takribani watu milioni 30 chini ya mpango mahsusili wa *Lake Victoria Environment Management Program (LIVEMP)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kwa mujibu wa kanuni ya 70 kifungu kidogo cha 2 ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004.

Nikianzia na maoni ya jumla ni kwamba kamati inaridhika kuwa malengo ya Muswada huu ni mazuri, ni dhahiri kuwa kama Muswada huu utapita ambapo nashauri Waheshimiwa Wabunge waupitishe ili uwe sheria itasaidia sana kuyatunza vizuri mazingira ya nchi yetu katika hali nzuri pindi sheria itakapoanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhika na dhana nzima ya Muswada huu kwa kuweka bayana majukumu na wajibu wa kila sekta katika kila ngazi ya utendaji kuanzia Taifa hadi Kitongaji. Muswada pia umeonyesha majukumu ya wadau wengine wakiwemo wananchi wenyewe kama ilivyoainishwa katika sera ya Taifa ya Mazingira hususani katika masuala ya kuteua waratibu na washauri wa mazingira katika ngazi za Serikali za mitaa, Mikoa na Wizara.

Tathmini ya athari kwa mazingira katika shughuli mbalimbali yaani (*EIA*) inapendekeza kuwa ni suala la kisheria, kutoa elimu ya mazingira na ushirikishwaji umma katika masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira pia limewekewa kuwa ni suala la kisheria. Muswada huu unatoa nafasi ya kuweka viwango vya usafi wa mazingira kitaifa pamoja na kuainisha makosa mbalimbali ya uharibifu wa mazingira na adhabu zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unagusa sana maisha ya wananchi ya kila siku mfano, matumizi ya vyoo na utupaji taka. Hivi sasa wananchi wengi sana hawana vyoo na wengine wanavyo lakini hawavitumii, Halmashauri zetu karibu zote hazina vyoo vya kutosha ambapo kila mwananchi akiwa mijini aweze kupata fursa ya kukitumia choo. Vyoo vya Halmashauri vilivyo vingi ukiacha vile vya kulipia, ni vichafu sana kiasi cha kusababisha wananchi kujisaidia hovyo mitaani (*Makofii*)

Nyumba nyingi katika miji yetu zikiwemo hata zile za Shirika la nyumba la Taifa hazina vyoo au viro lakini vibovu sana kiasi kwamba ni kama havipo, hali hii huwafanya wananchi na wapangaji kuhangaika namna ya kujihifadhi.

Aidha miji yetu karibu yote kama kuna vyombo ambavyo wanapashwa kivitumia kutupa taka za mikononi au za nyumbani basi ni vichache mno na havionekani, pale ambapo vyombo hivyo viro basi wananchi hawana mazoea ya kutupa taka kwenye

mapipa ya taka. Si jambo la ajabu kumkuta mtu anatupa ganda la ndizi au taka nyingine pale anaposimama au kurusha taka huku anatembea.

Hali kadhalika wasafiri kwa mabasi ya mijini ya yale ya safari za mbali mikoani nao pia hutupa taka hovyo madirishani bila kujali kuwa taka hizo husababisha nchi yetu kwa ujumla kuonekana kuwa ni chafu. (*Makofi*)

Yapo mabasi ambayo hutoa mifuko midogo ya *plastic* kwa abiria ili waweke humo taka za vyakula, lakini mifuko hiyo hutumika kutupia taka dirishani wakati mwengine wahudumu ndani ya mabasi wanakusanya taka hizo lakini hata wao pia huzimwaga popote pale barabarani. Watu wanaposafiri na mabasi hayo hufika mahali popote porini ambapo dereva husimamisha basi na kuwataka abiria wakachimbe dawa porini, fikiria ni mabasi mangapi yanafanya hivyo na idadi ya abiria waliomo ndani ya mabasi hayo katika nchi nzima na hayo hufanyika kila siku ya Mungu. (*Makofi*)

Lakini uzoefu wetu kutokana na nchi nyingine haya hayafanyiki hivi viro vyoo vya kutosha mahali pengi mijini aidha kila nyumba lazima iwe na choo kinachotumika pia viro vituo barabarani ambapo mabasi husimama ili abiria waende kujisaidia kwenye vyoo ambavyo ni vingi vya kutosha na hutunzwa vizuri. (*Makofi*)

Tumetoa tu baadhi ya mifano ambayo inawagusa wananchi katika maisha yao ya kila ili wafahamu, kwa sababu kutojua sheria siyo msamaha wa kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa ushauri wake kwa Serikali kuwa kutokana na mazoea yetu mabaya ya wananchi na taasisi zetu kama vile Halmashauri za Miji na Wilaya ya kutokuwa na vyoo mahali pengi muhimu kama ambayo nimeieleza muda wa kutosha utelewe kabla ya kuanza kutumika sheria hii ili hali hii iweze kurekebishiwa. (*Makofi*)

Wananchi na Serikali zao za Mitaa na vijiji wapewe elimu ya kutosha kuhusu sheria hii, endapo sheria hii ikipita imeweka kipengele mahususi kuhusu ushirikishwaji wa jamii katika kutekeleza sheria hii basi hata utayarishaji wa kanuni uwe shirikishi kadri iwezekanavyo.

Ili suala la kudhibiti uharibifu wa mazingira liweze kufanikiwa Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu ya mazingira kwa wananchi kuanzia ngazi ya kaya, hali hii itasaidia kubadili tabia ya wananchi katika suala zima la kutunza mazingira maana watakuwa wanaona faida zake wenyewe kutokana na juhudu zao zinazozingatia elimu bora ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uchafu wa mazingira kutokana na mifuko ya *plastic* Kamati imelipigia kelele kwa muda mrefu sana katika mikutano inayohusu uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoa na ndani ya Bunge lako Tukufu. Katika Muswada huu suala hili limeguswa katika kipengele cha 120 kinachotafsiri maana ya *LITA*

Vifungu Na. 121 na 122 vinaleza namna ambavyo Mkaguzi wa Mazingira atakavyowajibisha wahusika kuondoa uchafu huo zikiwemo hizo taka za mifuko ya plastic, bado kamati inaitaka Serikali kukaa na hao wenye viwanda hivyo ili watoe utaratibu wa kudumu wa kushughulikia mifuki hiyo ya plastic ambapo inatengenezwa hapa nchini na mingine mingi kuleta kutoka nchi za nje. (*Makofî*)

Tumetembelea Miji ya Kisumu, Jinja, Kampala na Entebbe wanatumia mifuko hiyo lakini mitaani hatukuiona kuzagaa kwa nini Tanzania Tushindwe, penye nia pana njia basi tuondoe aibu hii ya plastic kuzagaa nchi nzima hasa baada ya kutungwa sheria hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefurahishwa na vile Muswada huu ulivyota madaraka ya kutosha kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira yaani (*NEMC*). Sheria hii imelipa Baraza nguvu ya kisheria ya kukamata, kuwaadhibu wote wanaoharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu pia ieleweke kuwa kwa mujibu wa Muswada huu *NEMC* au Idara ya mazingira haifuti sheria nyingine za mazingira, wala haiingili idara au Sekta nyingine kama ambavyo wengine wamejaribu kueleza katika mikutano yetu na wadau. Muswada huu utakapokuwa sheria unaheshimu sheria nyingine zote za kisekta za sekta nyingine na pale ambapo sheria nyingine zipo kimya kuhusu jambo fulani basi sheria hii itafanya kazi.

Sheria hii ina lengo la kuratibu mambo ya mazingira na utekelezaji utafanywa na wahusika wa sheria hizo nyingine, kwa hiyo hauna maingiliano ila uwajibikaji ndiyo umepewa mkazo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hali ya uhifadhi wa mazingira nchini kwa ujumla si ya kuridhisha, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utayarishaji wa kanuni za kutekeleza sheria hii mara tu baada ya Muswada kuitishwa na Bunge lako Tukufu. Kazi haina budi ikaenda sambamba na zoezi zima la kutafsiri sheria na kanuni zake katika lugha nyepesi ya Kiswahili kwa lengo la kuhakikisha kuwa watu wengi wanasoma na kuelewa fika maudhui ya sheria yenyewe na kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha maoni hayo ya jumla Kamati yangu iliupitia Muswada huu ibara kwa ibara, aidha katika kufanya hivyo Kamati haikusita kutaka ufanuzi katika maeneo kadhaa, kati ya maeneo hayo ni maeleo yaliyotolewa na Serikali kuwa Muswada huu utatumika Tanzania Bara tu na kwamba Zanzibar tayari wanayo sheria ya mazingira.

Kamati yangu inaishauri Serikali kuwa Muswada huu utakapokuwa sheria na wakati wa maandalizi ya kanuni zake basi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ishirikishwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adimu pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Arcado Ntagazwa Mbunge

Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia mazingira na Mheshimiwa Edgar Maokola Majogo - Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayehusika na kuondoa umaskini na Bwana Raphael Mollel - Katibu Mkuu Mwandamizi, Bibi Marry Mushi - Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wataalamu Waandamizi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wadau wote waliohusika kwa namna moja au nyingine katika maandalizi ya Muswada huu. Wote hao walitoa maelezo ya kina na ya usafaha mbele ya Kamati yangu kwani michango yao imewasaidia sana Wajumbe wa Kamati katika kuutafakari, kuujadili na kuuchambua ipasavyo Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwisho kabisa naomba niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu kwa kutoa michango yao iliyoboresha Muswada huu hadi kufikia hatua inayoonekana hivi sasa.

Waheshimiwa Wabunge wa Kamati yangu ni pamoja na Mheshimiwa Hassan Khatib - Makamu Mwenyekiti pamoja na wajumbe wengine Mheshimiwa Aziza Said Ali, Mheshimiwa Shaib Ameir, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Ali Said Juma, Mheshimiwa Sharifa Mbarouk Khamis, Mheshimiwa Bahati Abeid, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Laizer Lekule, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Bernadine Ndamboine, Mheshimiwa Philomon Ndesamburo, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mheshimiwa Mohammed R. Soud, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Issa Suleiman, Mheshimiwa Mathew Ole-Timan na Mheshimiwa Martha Wejja. (*Makofî*)

Aidha naishukuru pia Ofisi ya Katibu wa Bunge na Katibu wa Kamati ya Maliasili ya Mazingira Bwana Sam Manamba , kwa kuihudumia vizuri Kamati kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii nikiwa na lengo la kuliomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada huu na kuupitisha ili Taifa letu liwe na msingi madhubuti wa kisheria na kitaasisi kwa ajili ya kusimamia matumizi endelevu ya mazingira na maliasili zake. Ni matumaini yetu kuwa vizazi vya sasa na vijavyo vitanufaika sana na dhana hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

MHE. ALI SAID JUMA: Maoni Ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa mazingira (*Environmentally Management Act 2004*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kutoa maoni ya kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43 (5) b, c na 81 (1) toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, kambi ya Upinzani inapongeza Waziri katika Ofisi ya Makamu ya Rais Mheshimiwa Arcado Dennis Ntagazwa kwa kuleta Muswada huu

Bungeni, Muswada huu utakuwa mhimili imara wa kulinda na kuhifadhi mazingira dhidi ya uchafuzi.

Sheria hii itatoa muongozo thabiti wa usimamiji na uratibu wa shughuli za kulinda mazingira yetu, kwa sasa Tanzania ina utitiri wa sheria nyingi za kisekta zinazolinda na kuhifadhi mazingira kama sheria inayozuia uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na viwanda ambavyo iko kwenye sekta za viwanda.

Pia kuna sheria ya mazingira inayolinda na kuhifadhi uvuvi, viumbe nya baharini, wanyama pori na kadhalika, utekelezaji wa sheria hizi ni wa kisekta ambaa hauna mwingiliano baina ya sekta moja na nyingine hivyo kufanya uratibu na utekelezaji wa kitaifa kuwa mgumu sana.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, sheria hii kama itasimamiwa vizuri italipunguzia Taifa hali ya kuwa na vifungu nya bajeti nya kuhifadhi mazingira kwa Wizara ya zaidi ya moja ambapo hakuna uratibu wa pamoja na kuhifadhi mazingira. Hali hii imekuwa ikisababisha gharama kubwa wakati kazi ni hafifu na duni sana.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, tathamini kuhusu athari za mazingira kwa kufuata viwango nya kimataifa siyo kazi za kuangalia kwa macho tu, bali nyenzo za kisasa na wataalamu wanahitajika kufanya kazi hiyo. Kama Mheshimiwa Waziri atakuwa anakumbuka wakati Bunge hili linalidhia mkataba wa *Stock home* kambi ya Upinzani ilishauri kuwa Baraza la Usimamizi wa Mazingira *NEMC* lipewe uwezo wa kuwa na maabara ya kisasa ambayo itakuwa inaharibu viwango vilivyo nya kitaifa na kimataifa vilivyowekwa zaidi ya uharibifu huu sheria inaweza kuchukua mkondo wake. (*Makofii*)

Bila baraza kuwezeshwa kiutendaji kwa hili basi litaendelea kutumia maabara za Vyuo za Taasisi na kutumia viwango ambavyo Baraza halikushiriki katika upatikanaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 10 Ibara ya 140 Muswada huu unapendekeza Kamati ya Viwango nya Mazingira chini ya Shirika la Viwango la Taifa kuwa ndiyo itakayotayarisha kupitia na kutoa mapendekezo kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu viwango vikubaliwavyo katika uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani bado inashauri kuwa Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira ndilo lenye mamlaka ya kufanya hivyo na wao wapo hapo maalum kwa ajili ya masuala ya mazingira tofauti na Shirika la Viwango la Taifa TBS.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 191 kuhusu mtu yejote anayetenda kosa lolote kuhusiana na kipengele chochote kilichoelezwa ndani ya Muswada huu anatakiwa kulipa isiyopungua shilingi 50,000/= na isiyozidi milioni 50/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tunavyoolewa waharibifu wa mazingira ni wananchi walio na kipato kisichozidi hizo shilingi 50,000/= kwa mwaka, na wengi

wanajipatia riziki zao kwa njia ambazo uhatarisha na kusababisha uharibifu wa mazingira. Kuna wengine kama wakazi wa mwambao wa bahari, mfano Mafia, Ukerewe na hasa Mafia ambao vyoo vyao ni ufukweni mwa bahari kwa mantiki hiyo kijiji kizima kinaweza kufungwa gerezani kwani watakosa hiyo faini shilingi 50,000/=.

(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada mahsusini za Serikali za kuleta Muswada huu Bungeni Kambi ya Upinzani Bungeni imegundua kuwa kuna mapungufu kidogo ambayo yanatakiwa yaangaliwe kwa makini au yarekebishwe ili sheria iweze kutekelezeka ili kuleta maana iliyokusudiwa. Mapungufu hayo ni kama yafuatayo:-

- (i) Sheria hii inaweza kuwa ngumu kutekelezeka kwa sababu ya mlolongo mrefu wa Taasisi na Mamlaka zilizopewa licha ya kuwa imehusisha wadau wengi tofauti. Hii inaweza kuleta ukiritimba kwenye utekelezaji kama juhudhi za makusudi hazitofanyika kuwaelimisha wananchi na watendaji nini kinatakiwa kifanyike. Kwa mfano, sheria kama hii ilishatungwa kwa ndugu zetu wa Zanzibar toka zamani, lakini haifanyi kazi kwa sababu wananchi na watendaji hawakuelimishwa na hakuna kanuni za uendeshaji.
- (ii) Sheria za masuala ya mazingira ni dhana mpya kwetu. Sheria hii inaweza isieleweke vizuri hata kwa Wanasheria wenyewe. Hivyo, kuna umuhimu wa Serikali kuelimisha umma juu ya Muswada huu.
- (iii) Uanzishwaji wa ngazi tofauti za uongozi katika Muswada huu inaweza kuwa ngumu kupata wataalamu wa kutosha watakaotekeliza sheria hii.
- (iv) Mamlaka, Utawala na Taasisi zilizopendekezwa na Muswada huu *Environmentally Appeals Tribunal* zitaongeza gharama kubwa za uendeshaji Serikalini.
- (v) Muswada huu unapendekeza na kumpa mamlaka makubwa Mheshimiwa Waziri anayesimamia mazingira. Hii kwa mwananchi wa kawaida inaweza kuzusha malalamiko na manung'uniko kwa Serikali. Hivyo bila kuwaelimisha wadau mamlaka ya Waziri yanaweza kuleta matatizo.
- (*Makofi*)
- (vi) Muswada umekwenda mbali na matakwa ya sera. Ingetegemewa kwanza sera ipitiwe upya, halafu ndiyo sheria ikatungwa. Sera inatungwa kwanza na si kinyume chake. Sera ya Mazingira ya mwaka 1977 maendeleo yalizaliwa mwaka 1977 yamepitwa na matukio. Ni vizuri Sheria ikaenda na wakati. Lakini vilevile lazima iwe imekubaliwa na sera. Hivyo, ndiyo Serikali inavyofanya kazi! Sasa katika Muswada huu ni kinyume kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatarajia mapendekezo tuliyoyatoa hapa Kambi ya Upinzani yatazingatiwa kwa manufaa ya wadau wote na Taifa letu kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema yote hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

(*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hapo ndiyo tumemaliza wale wasemaji wakuu. Waheshimiwa Wabunge walioomba kuchangia ni kumi na moja. Kwa hiyo, tutaanza moja kwa moja na nadhani tutaendelea mpaka kesho. Kwa hiyo, wanne wa kwanza ni Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Edson Halinga. Sasa namwita Mheshimiwa Ireneus Ngwatura.

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kama mtu wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na wasaidizi wake wote kwa kufanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu naweza kusema pengine umechelewa hasa ikizingatiwa kwamba sera ilianza mwaka 1997, leo baada ya miaka 7 ndiyo tunaleta sheria. Kwa hiyo, ni dhahiri kabisa ukizingatia masuala yaliyojitokeza katika kipindi hiki kama vile utandawazi ni dhahiri kabisa uenda katika utekelezaji wake itabidi mambo mengine yafanyiwe marekebisho hata kabla hayajaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nianze na Ibara ya 14 inayohusu kuteuliwa kwa Mkurugenzi wa Mazingira anaitwa *Director of Environment*. Lakini wakati huo ukienda Ibara ya 21 inahusu kuteuliwa kwa Mkurugenzi Mkuu. Lakini pamoja na ukweli kwamba katika sheria haijasemwa kwamba patakuwepo na Wakurugenzi mbalimbali kwenye Baraza la Mazingira. Ni dhahiri kabisa kwamba kama watakuwepo mimi naamini kabisa itakuwa ni kuchanganyachanganya tu. Kunakuwa na Mkurugenzi wa Mazingira, kunakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Mazingira katika Taasisi hiyo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri kwamba badala ya kuwa na Mkurugenzi wa Mazingira angekuwepo Kamishna wa Mazingira. Kwa sababu ukiangalia sana hii ni nafasi kubwa sana. Nasema hivi kwa sababu moja ya mambo mengi atakayofanya huyu ni ya uratibu na anaratibu sekta mbalimbali katika Wizara mbalimbali. Sambamba na hilo ukienda kwenye section 33 inazungumzia masuala ya *Environmental Coordinators* yaani waratibu wa masuala ya mazingira ambao watakuwa wanaratibu shughuli mbalimbali katika sekta zao. Sasa ni dhahiri kabisa kwamba ili pawe na mtiririko mimi nashauri kabisa na nadhani hata Mkurugenzi wenyewe atafurahi kama ataitwa Commissioner of Environmental Coordination.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo. Sasa naomba nianze na kuchangia kuhusu masuala mengine. Moja, ni suala la uchafuzi wa mazingira. Mimi naungana kabisa na wenzangu hasa Kamati kwa kuona kwamba suala la mifuko ya plastiki si suala la kuliletea mzaha. Mimi ningemwomba Mheshimiwa Waziri, nafahamu meno anayo pigeni marufuku hizo shughuli. Ninafahamu mnaogopa.

MBUNGE FULANI: Wanaogopa nini?

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mnaogopa nini kuna mkono wa mtu. Mkono anao Mzee Arcado Ntagazwa, fanya kazi. Nasema hivi kwa sababu kama tutaedelea na kiwango hiki cha uchafuzi wa mazingira kutokana na mifuko ya plastiki miaka mitano ardhi ya nchi hii itaharibiwa kuanzia Mijini mpaka Vijiji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya mazingira katika nchi hii si nzuri sana kwa kipindi cha miaka 30 iliyopita tumefanya uharibifu mkubwa sana katika mazingira yetu na katika kila nyanja. Inasikitisha kwamba Tanzania bado si nchi ya viwanda, lakini kiwango tunachotumia katika kuharibu sijui tutakapoanza na tutakapotambuliwa kuwa ni nchi sasa ya viwanda kama nchi za Magharibi itakuwaje? Mimi nadhani kama kuna kitu kinaitwa mwisho wa dunia, basi kitatokana na sababu za uchafuzi wa mazingira siyo kitu kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba tuanze na yale ambayo tunayaona. Lakini bahati mbaya tunasema kwamba tunachafua mazingira au tunaharibu mazingira kwa sababu za kiuchumi. Mimi ninadhani iko haja ya kuoanisha kati ya uchumi na mazingira kwa sababu mazingira ndiyo uhai. Sasa baada ya kusema hilo. Kwa kweli ningependa nipongeze Muswada wenyewe hasa kwa vile umeenda mpaka kwa watu binafsi, unaenda kuwashirikisha wanavijiji mpaka kwenye ngazi ya kitongoji. Lakini rai yangu mimi ni kwamba ili sheria hii iweze kutekelezeka itabidi kuanzisha Taasisi mahsusini ambazo zitaanza kuwafundisha Watanzania Elimu ya Mazingira. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hivyo tu, mitaala ya shule kuanzia shule za msingi mpaka *Secondary Schools* na hata Vyuo Vikuu ianze sasa kuangaliwa upya ili suala la mazingira liwe ni sehemu ya elimu ya Mtanzania. Vinginevyo utekelezaji wake ninauona utakuwa ni mgumu. Sio hivyo tu viongozi mbalimbali wapate elimu kuanzia ngazi ya Kijiji, kuanzia Kata mpaka Halmashauri, inaelekea mambo kwa kweli ambayo Watanzania tunafanya wakati mwingine huwezi kuamini kwamba tunaifanyia nyumba ile ambayo ndiyo usalama wetu. Mambo tunayaona hivi hivi yanakwenda tu. Si ajabu katika nchi hii na nyie wengi ni mashahidi hapa, viongozi wengi wanamatamka hadharani kwamba Tanzania ni nchi kubwa limeni tu na fanyeni mambo mnayotaka, wenzetu wanatusikia, wakimbizi wanaposikia ni nchi kubwa wanajaa hapa nchini na kila kitu wanaharibu. (*Makofî*)

Kwa hiyo, mimi nadhani kwamba hata mambo tunayozungumza viongozi tuone kwamba hakuna mtu yejote anaweza akaongeza hata kipande kimoja cha ardhi, *land is fixed* na hii ndiyo iwe hasa dhana yetu kubwa katika kumeneji mazingira yetu. Ikibidi watu tupungue ardhi ibaki hapa hapa. *Land is free* huko ndiko kunakotakiwa tuingie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo, kwa sababu mwaka 1997 tulikuwa watu milioni kumi na mbili na laki tatu, leo tunazungumzia milioni 35 na zaidi, ardhi imebaki pale pale tunaongezeka. Sasa tunafanya nini ili tuweze kutosheka katika eneo hilo. Mimi ninachotaka kusema ni kwamba kama Hayati Makat Maganeli alivyokuwa amesema wakati mmoja kwamba: “ardhi inatosha kwa kila mtu, lakini ardhi haitoshi kwa

watu wachoyo". Kwa hiyo, kama tutajenga ubinafsi uliokithiri tujue kabisa ardhi haitoshi. Lakini kama tukiona kwamba wote tunatakiwa tukae kwenye ardhi hiyo ambayo haiongezeki, basi inabidi tuangalie upya mipango yetu ya matumizi ikiwa ni pamoja na suala la tija. Lazima tutumie ardhi kidogo, lakini tuzalishe zaidi huko ndiyo tutafika.

La mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba ili sheria hii ambayo mimi naomba tuipitishe ili iweze kufanya kazi itabidi hata mfumo wa kiutawala huoanishwe. Kwa sababu ziko sekta ambazo zinagongana zenyewe kwa zenyewe. Ukiingia kwenye Sekta ya Kilimo atagongana na Sekta ya Maji na Mifugo, atagongana na Sekta ya Nishati na Madini na watagongana na Maliasili na Utalii. Sasa kama hapatakuwa na njia za kuoanisha mimi ninakuwa na wasiwasi kwamba badala ya kutumia nguvu zetu pamoja na raslimal chache katika kuhakikisha kwamba tunaoanisha matumizi yetu itafkia mahali tutatumia hizo fedha katika kugonganisha na kuogopana na matokeo yake tutajimaliza wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Mungu aliumba nchi kwa ukamilifu binadamu anaiharibu. Lakini mimi nasema kwa wale wanaoamini kama hapa duniani kuna dhambi, lakini nasema hakuna dhambi kubwa zaidi kama dhambi ya kuharibu Mazingira kwa hiyo adhabu yake iwe kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema dakika nane zitanitosha kwa sababu Muswada wenyewe umekidhi maelezo. Nilihudhuria mara mbili kwenye Kamati ya Mazingira na nilikuwa mmoja kama ni mdau wa Mazingira. *Nili-declare interest* kwamba nilikuwa mjumbe wa Baraza la Mazingira kwa muda wa miaka 4 na mimi vilevile ni katika *ma-analyst* wa nchi hii wakipanga orodha 100 bora mimi nimo. Kwa hiyo, nilikuwa najua hii *vision* ya Muswada wenyewe umekwenda *to deep analytical quality*. Nilikuwa nimefanya kosa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Muswada wa sheria ulioko mbele yetu unaohusu mazingira na udhibiti. Mimi nilidhani basi ni sheria ya Udhibiti wa Mazingira. Maana ya management kumbe sio Mazingira ni *Control* ya Mazingira ni *management*. Kumbe *management* kuna udhibiti na uangalizi na uendelezaji maeneo ili kupata mambo yaende vizuri. Ingekuwa ni udhibiti peke yake tungeunda vyombo vyaa udhibiti ambavyo vingeleta sheria ya Austria ambayo iligawanyika katika maeneo matano. Lakini kwa bahati nzuri walikuwa wameeleza sheria ambayo ilikuwa *three in one* ambayo inaelezea mambo kadhaa ambayo nitayabainisha huko mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nilipohudhuria kwenye Kamati ya Mazingira tuliamiwi kwamba kuna wadau mbalimbali walileta mapendekezo kadhaa. Walipendekeza Ibara ya 56 kufanyiwa marekebisho. Nashukuru kuliarifu Bunge hili kwamba Ibara karibuni 18 ndizo zilifanyiwa marekebisho. Katika marekebisho

mliyoyaona hivi sasa kuna *distinction* ya kuanza kuanzisha maneno ambayo yamefutwa yako saba. Kuna *additional of wealth* 22, kuna *conjunction* 3. Aidha, mkatoa off mkaweka with ili iandane pamoja na sheria kuleta mantiki ya utaratibu wa kisheria. Kwa kuwa mimi sio Mwanasheria ila ni mtungaji wa sheria bali ninaungana na taaluma zile zilizotumika katika kubaini Muswada huu. Aidha, *definitions* zilizotumika ziliwu tatu, katika *introduction wali-define* neno *Minister* ambalo nadhani liliwu bado linaendelea, lakini haku-*define Sectoral Minister* kwa sababu hazikutajwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kwenye ukurasa wa 85 kuna maneno manne tena katika Ibara ya 120 yamefanya *definition* pale pale kwenye maeneo yanapotumika, lakini nimeshtuka neno la *Laboratory* lililotumika. Katika Ibara ya 162 wakataja *the Government, Chemist Agency*, lakini kwenye Ibara ya nyuma kule wakataja kwamba *Minister anateua Laboratory, mtateua Laboratory* gani wakati ipo imetajwa tayari. Kwa hiyo, ndiyo hicho nilikuwa na wasiiasi wa vitu kama hivyo. Kwa hiyo, nadodosa Muswada baadaye nitakuja kwenye maudhui ya Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu nishukuru kwamba Muswada huu kwamba uko *self contained* kwa sababu kuna vitu kama *Forest, National Parks, River, pollution, inclusive, harbour and settlements, fire*. Kazi za *Health Officers* wametajwa kwenye sheria ya mambo ya uharibifu wa Mazingira Mijini wametajwa Bwana Afya. Sasa kuna mtu mpya anateuliwa nadhani kwenye Wilaya. Sasa yule watakuwa na *conflict* wawe kitu kimoja na wawe bega kwa bega kushirikiana kuhakikisha kwamba kila mtu anaangalie eneo lake wasiwe wanapishana kama wale makengeza wawili waliokutana wakaanza kulaumiana, kengeza mmoja akamgonga mwenzake, akamwambia kwa nini huangalii unakokwenda na mwenzie akamwambia na wewe kwa nini uende unakoangalia. Kwa hiyo, wawe kitu kimoja watekeleze majukumu yao vizuri. Mambo yanaanza sasa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kabisa usafi ni matokeo, usafi ni tabia, huwezi kumlazimisha mtu akawa msafi, lakini mtu wakati mwingine mchafu ukimkuta hata kajiandaa na sabuni na taulo anatakwambia anaenda kuoga hata kama akiwa mchafu angalau kajiandaa. Tanzania inajiandaa sasa kujiweka sawa kwa Muswada huu. Kwa sababu umeeleza sekta zote mtambuka. Wizara zote zinazohusika na hii ingawa hazikutajwa kwenye orodha, lakini naona kila Wizara inahusika hapa katika kuandaa taratibu za mazingira. Lakini lazima kuna sehemu ambayo ni ya kwenda kuhiji ili kuonyesha taratibu hizo. Kwa hiyo, lazima Wizara zibainishe wanafanya vipi kuhusu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuharibu mazingira sio peke yake miti, tulikazania sana *hundred percent* kila akisimama mtu panda mti kata mti, mazingira si miti peke yake. Mazingira yanaharibu katika rangi wajihii na harufu. Kwa sababu mazingira uweza kuyaona, kuyagusa na kuyanusa, kuona uweza kuvutia kutokana na mazingira yalivyokuwa mazuri kwa kuyaona na wakati mwingine yanatia moyo kwa kuvutia mazingira hayo kuwekwa vizuri. Kuna mazingira mengine yanatisha. Ndiyo maana Mungu kaumba giza unalionna lakini limekosa sauti ili mlale salama, na kaumba upopo mnausikia lakini hamuoni ili muweze mkatazame vizuri. Sasa ni mazingira

ambayo yanaweza yakatokea. Hayo ni matokeo hutoweka kwa sababu majaribu hujaribika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema kabisa kwamba kuna rangi, wajihii na harufu. Kwa mfano, kuna kitu kizuri kinaweza kikaletwa kwa mfano chai ya maziwa ukaweka na yai mbovu au shuka nyeupe ukalifua kwa mkaa au maziwa ukayachemsha kwa maji ya chooni. Unayataja vizuri kabisa lakini ule utaratibu na mchanganyiko wa vitu hivyo unakuta havivutii. Hivyo basi, mazingira ni matokeo ya kutoweka, lakini si majaribu yangejaribika. (*Kicheko*)

Halafu *selected Ministries* zitajwe wazi wakati Mheshimiwa Waziri anajumuisha hoja yake ataje kwamba ni Wizara gani. Mito ambayo ni safi duniani imenorodhesha, lakini muda kwa sababu hautoshi iko mito kama Misisipi *value composition* ya matukio kama Misisipi Amazon, mito kama Kagera, Ruvu Wami kwa sababu haitoki Mijini. Mito ambayo inapitia Mijini mara nyingi kuna matukio mengi ya binadamu ambao si waamini hutumia maeneo yale kutupa vitu vya ajabu ajabu ambavyo vimetajwa. Kutaja vitu vibaya kama *waste*, betri na nini na kwa hiyo, kuharibu mazingira ya mito ile na kusababisha athari kwa watu wanaotumia mito ile. Kwa hiyo, kuwe na udhibiti mkali sana katika Miji ambapo mito inapita na wananchi wanatumia maji hayo kwa kunywa. Kwa mfano, mto Ngerengere nashukuru sana Manispaa ya Morogoro wameweka Kamati Maalum kabisa. Nampongeza Mstahiki *Mayor* pamoja na *Mayor* wa zamani Mheshimiwa Oscar Mloka ambaye ni Mbunge sasa hivi waliweka Kamati maalum kusimamia ili kusafisha eneo lile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa matumizi ya mazingira tunasema *NGOs* wanazoundwa. Zipo *NGOs* zinaandikishwa kwa kuwa na Katiba nzuri tu na maelekezo, lakini *NGO* hiyo inatumika kwenda kusimamia mlima fulani ambao uko mbali na Dar es Salaam. Kwa kweli *NGOs* zitoke pale pale kwenye maeneo ambapo wananchi wanahuksika. Tusitumie mfumo tochi, tochi humulika mbali kunako giza. Zipo *NGOs* zingine ambazo hutumika wanaita kwa mfano, *Uluguru Mount Environmental Assessment* ya Mlima Uluguru iko Dar es Salaam. Sasa hiyo ni tabia mtu unanunua miwani halafu unavaa unaita miwani ya juu wakati ni ya kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli *NGOs* kama hizi mngeziangalia na kufanya assessment. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri aangalie vizuri sana kuhusu hizi *NGOs*. Tunashukuru sana katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki tuna *NGO* ambayo imeandikishwa. Napenda hapa nimpongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii mama Mushi pamoja Mkurugenzi wa Mazingira pamoja na msaidizi wake tumepata taarifa kwamba wananchi wa vijiji 13 vya Milima ya Uluguruni tumeanzisha Muungano *Environmental Group* ambayo tumeandikisha juzi tu na mimi ndiyo mlezi wa hiyo. Kwa hiyo, vile vijiji vya Luholole, Changa, Kibwaya, Mfumbwe, Logo, Uponda, Mifuru, Hewe, Bwagiro, Nyemgadu, Mkololo mpaka Tandahi, wananchi wa kule Kiloka ile kwa kweli mmefanya mambo mazuri sana. Milima ya Uluguru sasa italindwa na wenyewe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na *NGO* mmoja ilikuwa inakuja kule inakata migomba ya wananchi maeneo ya Mbamba kule. Sasa *NGO* ile ni ukombozi tutashirikiana pamoja kuhakikisha kwamba zile *NGOs* zinazoletwa kwa mfumo tochi zinatoka Dar es Salaam kuja kukata migomba wananchi. Sasa siku ya uzinduzi nitafanya huko, baada ya mwezi Mtukufu kukamilika, tukishafuturu tayari, tunakuja kule Tandahili tutaita wananchi. Tutasema pamoja na sheria yenu kufanyiwa maandalizi tutafungua *NGO* yetu wananchi watafurahi. Hapo ninawafagilia wananchi wa kule kujifagilia mimi mwakani. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ambayo yanafanywa na watu waharibifu mara nyingi tuisuse. Tuwafuatilie ili tuweze kuteketeza mambo yao. Kwa sababu Mapadri walisusa kuchora picha, waliambiwa na Baba Askofu choreni picha, wakasema picha gani, akasema choreni shetani, wakasema hatumjui, akasema shetani kila mtu afikirie alivyo, wakasema hatuna karatasi, wakapewa karatasi tatu, leo chora, kesho chora na kesho kutwa chora, wakasema kwa muda gani, akasema masaa matatu, wakasema kalamu hatuna, wakapewa kila kitu kalamu za rangi saba. Choreni shetani kwa muda gani, masaa matatu. Wakaanza kuchora, ila mmoja kachukua kalamu nyeusi akaanza kuchora papapa akampelekea mwalimu, akamwambia huyu ndiye shetani, akasema *hundred percent* waache wenzako tu. Wengine wakaremba wakampeleka mwalimu, akamwambia huyu ni shetani sifuri, shetani sio mzuri kama hivi, shetani ni mbaya. Mwalimu alichokosea akachukua ile picha ya yule mbaya akawaonyesha huu ndiyo mfano wa kuigwa, hakusema kuwa ni shetani aah, akasema mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo asubuhi Mapadri wote na wale wanazuoni wakaja na kalamu moja tu nyeusi. Sasa mwalimu akamwambia leo mnachora picha ya malaika. Kwa hiyo, wakaiga mfano wa mwenzao wa jana, wakachora nyeusi wote. Kwenda kule wakapewa sifuri wote kwamba malaika, miltakiwa mchore kama jana. Wakaona mwalimu anayumbisha ikajengwa hoja jana tulichora nzuri, tuambiwa tuchore mbaya, tumechora mbaya, tumeambiwa tuchore nzuri. Sasa leo lazima tugome, wakaamua wagome. Kwa hiyo, wote wakaja na kalamu ya kuandikia jina tu la hiyo picha halafu wasichore kabisa. Walipokuja wakaambiwa darasa limeanza leo mnachora picha ya Mungu, wakaandika majina yao wanafunzi halafu wakaandika jina la picha ya Mungu, wakarudisha vilevile bila kuchora wakapewa 100, wakaambiwa Mungu hana mfano wa kuigwa mmeepata. Nashukuru sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania Muswada huu mahali popote inapotamkwa kwamba mmeshirikishwa, mfumo shirikishi utakuwa pamoja. Kwa hiyo, tutakapoambiwa tuchore, tuchore, tukigoma kuacha basi tutapata matatizo kupata zawadi na zawadi iliyotajwa ndani ya Muswada huu ni ile faini ambayo mtatozwa na muwe wasimamizi wazuri katika maeneo yenu, mwekeni Mungu mbele uma kati mbaki nyuma katika kuendeleza Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa baada ya Mheshimiwa Semindu Pawa, shughuli zetu zinaishia hapo. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 11.54 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi
Tarehe 11 Novemba, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*